# NAFASI YA FANI KATIKA KUFANIKISHA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO

**IBRAHIM MATIN**

TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA KISWAHILI KATIKA IDARA YA LUGHA, ISIMU NA FASIHI, CHUO KIKUU CHA RONGO

**2021**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa na mtu yeyote kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Ibrahim Matin

AS/MKIS/1002/2013

Sahihi…………………………………….. Tarehe……………………………………

## IDHINI

Tasnifu hii imetolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Rongo

**Prof. Sangai Mohochi**

Profesa Mshiriki

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu Cha Rongo

Sahihi…………………………………...... Tarehe……………………………………

**Dkt. Carren Nyandiba**

Mhadhiri Mwandamizi

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Rongo

Sahihi…………………………….…. Tarehe…………………………………

## TABARUKU

Mwanzo kabisa tasnifu hii nawatabarukia wazazi wangu Kepha Matin na Emmy Matin. Wazazi wangu hadi leo bado nashangaa licha ya kisomo chenu kidogo mlijitahidi ili kunisomesha pamoja na wadogo wangu Beatrice, Amadi, Pauline, Everline na Jane. Tangu nikiwa mchanga mlisoma pamoja nami na kunielimisha. Siwezi kuwalipa bali natoa ahadi kuwalipa kupitia kwa wajukuu wenu. Asante baba, asante mama. Tuombe Yehova Mungu wetu atupe uhai ili tukamilishe tulilolianza.

## SHUKRANI

Kwanza, ningependa kumshukuru Mola kwa maisha na uhai nilio nao na afya angaa kiasi cha kuniwezesha kuona na kusoma ili kufanya upekuzi wangu. Nawashukuru pia wasimamizi wangu Prof. Sangai Mohochi na Dkt. Carren Nyandiba kwa uelekezi mlionipa wakati wa kuiandika tasnifu hii bila kuchoka. Tatu, Bw Odingo Nicholus ahsante kwa kutambua kuwa nasaha ni kama maji baridi wakati wa jua la utosini. Ahsante kwa kunitia moyo. Nne, nashukuru Mola kwa zawadi katika jina la wafuatao Ragero, Sayo, Lucy, Mboya, Masenge, Nyamweya na Ong'wen. Mmekuwa kitia moyo na nawapenda kwa dhati. Tuliketi pamoja kwa vipindi virefu bila kuchoka ili kusoma na kujadiliana. Tulicheka na kulia pamoja. Hatimaye, wahadhiri wangu Dkt. Ontieri, Dkt. Kisurulia, na Marehemu Dkt. Oyoo Weche asanteni kwa kutufunza na kutuongoza kwa mapenzi ya mzazi kwa wanawe. Dkt. Odawo, nakushukuru kwa kuhariri kazi hii na kunishauri kila nilipobisha kwako. Kadhalika, natoa shukrani kwa Chuo Kikuu cha Rongo kwa kunipa nafasi ya kusoma na kufanya utafiti.

Aidha, natoa shukrani nyingi kwa wazazi wangu kwa kunitunza na kunionyesha namna ya kutembea duniani kwa heshima na tahadhari kuu ili kufikia hapa nilipofikia. Licha ya kuwa mna kisomo cha haja tu mmejizatiti kuhakikisha kuwa ninapata yaliyo bora maishani na masomoni. Shukrani nyingi pia zimfikie mke wangu, Mama Nicole kwa kunivumilia, kunitia moyo na kujinyima wakati wote ili nifanikiwe masomoni na hatimaye kuandika tasnifu hii. Najua sitaweza kukulipa hisani hii kubwa ila nakuombea tu Mola akutunze na akupatie siku nyingi. Wanangu Nicole na Kepha Junior natambua kuwa nanyi mlinivumilia na kunipa wakati mwanana wa kusoma na kutafiti. Mlidhabihu muda wenu wa kucheza na hata kunikosa kwa vipindi virefu ili nipate nafasi ya kusoma. Yehova Mungu awajalie siku nyingi na siha njema.

# IKISIRI

Fasihi kama kipengele cha lugha ya Kiswahili imegawika katika tanzu mbalimbali. Mojawapo ya tanzu hizo ni fasihi ya watoto ambayo ina upekee wa kimtindo, kifani na hata kimaudhui. Ingawa kuna tafiti mbalimbali kuhusu fani na maudhui katika aina hii ya fasihi, hatukupata uliochunguza vipengele hivi kwa pamoja kwa kuonyesha jinsi vinavyohusiana. Hii ndiyo sababu utafiti huu ulichunguza jinsi wasanii wa vitabu vya fasihi ya watoto wamefuma kazi zao kwa kutumia fani mbalimbali ili kuibua maudhui yanayowalenga watoto. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuainisha vipengele vya fani vinavyotumiwa katika vitabu vya fasihi ya watoto; kudondoa maudhui yanayoangaziwa katika vitabu hivyo na kisha kutathmini jinsi fani zilizotumiwa zinavyofanikisha maudhui katika *Kisasi Hapana* kilichoandikwa na Ken Walibora, *Nimefufuka* kilichoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* kilichoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* kilichoandikwa na Nuhu Bakari. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure (1916). Nadharia hii inajibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja kwa nyingine katika kufanya kitu kizima. Kwa kuongozwa na nadharia hii, tulichukulia fasihi kuwa kitu kizima kinachojengwa kwa maudhui na fani. Katika ngazi ya pili, fani nayo imeundwa kwa vipengele mbalimbali vya lugha. Vipengele hivi vilitambuliwa na matumizi yavyo yakafafanuliwa na kuelezwa. Kila maudhui kwa upande mwingine pia yalichukuliwa kuwa ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii huku yale mawazo madogomadogo yanayochangia hayo maudhui makuu tukiyachukua kama maudhui madogo. Ushirikiano kati ya fani na maudhui katika kukamilisha kazi ya fasihi pia ulichunguzwa kupitia uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa njia ya kiupekuzi na uchanganuzi matini kwa kuhakiki vitabu vinne vilivyoteuliwa kimaksudi. Tulisoma vitabu hivi kwanza ili kuvielewa, kisha tukasoma tena ili kudondoa na kunakili vipengele vya fani na maudhui na kuvijadili. Vipengele vya fani vilivyodhihirika ni tashbihi, misemo, nahau, methali, picha na taswira. Maudhui yaliyojitokeza wazi yalikuwa ni familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ushawishi, ugonjwa na kifo. Hatimaye tulichanganua data hiyo kwa kuonyesha jinsi fani tulizodondoa zilivyofanikisha maudhui tuliyokuwa tumetambua katika vitabu hivyo na tukawasilisha matokeo ya utafiti wetu kithamano. Ilitarajiwa kazi hii iweze kutoa mchango katika kuhakiki fasihi ya watoto siku za usoni na kuwanufaisha waandishi kwa kuwatazamisha kazi zao ili kuona ubora na udhaifu wa kazi hizo. Walimu na wanafunzi wataweza kuona maudhui na vipengele vya fani katika vitabu tulivyohakiki ili kupata vionjo vya kazi hizo. Wakuza mitaala wanaweza kutumia matokeo ya utafiti wetu wanapoamua vitabu watakavyoteua ili kusomwa na wanafunzi. Pia, washikadau wote wanaweza kupata vionjo vya vitabu tulivyohakiki na hivyo kuwatia mshawasha wa kuvisoma au kuvifanyia utafiti zaidi. Kwa njia hii utafiti huu unatoa mchango katika kuboresha fasihi ya watoto.

# ABSTRACT

Literature as an aspect of Kiswahili language has been subdivided into various genres. One of the genres is children's literature. This genre is unique in terms of style, stylistic features and themes. Even though there are several research in this genre, there was evidence of a research done on styles and themes together. This is why this research aimed at investigating how authors of Kiswahili children's literature have structured their works by employing various stylistic features to reveal children-targeted themes. In order to fulfill this, the following objectives guided the study: to classify various stylistic features used in children's literary books; to discuss various themes in the selected books and finally, to evaluate how the various stylistic features used by the authors successfully convey themes in *Kisasi Hapana* by Ken Walibora, *Nimefufuka* by Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* by Bitugi Matundura and *Wema wa Mwana* by Nuhu Bakari. This research was guided by Structuralism Theory propounded by Ferdinand de Saussure (1916). Structuralism Theory explains the relationship that exists between one element and the other and how various parts make one complete element. Guided by this theory, literature was taken as a whole element made of several themes and stylistic features. At the second level, stylistic features is a complete element which consists of proverbs, tropes, imagery, pictures and symbolism. These stylistic features were identified and their role explained. Themes and sub themes on the other hand were also taken as a complete element. The relationship between stylistic features and themes in building literary work was investigated through data analysis. This was a library research that involved critical analysis of texts that were purposively sampled. Data was collected by in-depth reading of the texts in order to understand, identify and note down the various stylistic features and themes. The stylistic aspects that were identified were proverbs, tropes, imagery, pictures and symbolism. On the other hand, the themes that were identified were family, conviction, discipline, importance of a name, education, hard work, sickness, death and the place of women in the society. We eventually showed how the stylistic features identified help in building the said themes and the outcomes were presented qualitatively. This research will be useful in critiquing children's literature, will be beneficial to writers of children's literature by helping them see strengths and weaknesses of their works, teachers and learners can see themes and stylistic features analysed and curriculum experts can use information in this research in choosing books for children. All stake holders in children literature can be persuaded by this research to read the children books analysed in this research and research more on them. In so doing this research will help in improving children literature.

**YALIYOMO**

UNGAMO ii

IDHINI ii

TABARUKU iii

SHUKRANI iv

IKISIRI v

ABSTRACT vi

YALIYOMO vii

ORODHA YA MAJEDWALI xi

ORODHA YA VIELELEZO xii

VIFUPISHO NA AKRONIMU xiii

UFAFANUZI WA ISTILAHI xiv

SURA YA KWANZA 1

MISINGI YA UTAFITI 1

1.0 Utangulizi 1

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Suala la Utafiti 5

1.3 Madhumuni ya Utafiti 5

1.4 Maswali ya Utafiti 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada 6

1.6 Umuhimu wa Utafiti 7

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti 7

1.8 Misingi ya Nadharia 8

1.8.1 Mihimili ya Umuundo na Jinsi Ilivyotumiwa katika Utafiti 9

1.9 Hitimisho 11

SURA YA PILI 13

UHAKIKI WA MAANDISHI 13

2.0 Utangulizi 13

2.1 Maana ya Fasihi 13

2.2 Maana ya Mtoto 14

2.3 Maana na Sifa za Fasihi ya Watoto 15

2.4 Aina za Fasihi ya Watoto 17

2. 5 Manufaa ya Fasihi ya Watoto 18

2.6 Historia ya Fasihi ya Watoto 19
2.7 Vipengele vya Fani katika Fasihi ya Watoto 25
2.8 Maudhui katika Fasihi ya Watoto 28
2.9 Uhusiano kati ya Vipengele vya Fani na Maudhui katika Fasihi 30
2.10 Hitimisho 34
SURA YA TATU 35
MBINU ZA UTAFITI 35
3.0 Utangulizi 35
3.1 Muundo na Mbinu ya Utafiti 35
3.2 Eneo la Utafiti 35
3.4 Idadi Lengwa 36
3.5 Uteuzi wa Sampuli 36
3.6 Ukusanyaji wa Data 38
3.7 Uchanganuzi wa Data 38
3.8 Maswala ya Maadili katika Utafiti 40
3.9 Hitimisho 40
SURA YA NNE 41
UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO 41
4.0 Utangulizi 41
4.1 Vipengele vya Fani katika Fasihi ya Watoto 41
4.1.1 Tashbihi 42
4.1.2 Taswira 51
4.1.3 Nahau 58
4.1.4 Misemo 63
4.1.5 Methali 66
4.1.6 Picha 70
4.2 Maudhui katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto 76
4.2.1 Familia 78
4.2.2 Elimu 80
4.2.3 Nidhamu 82
4.2.4 Ushirikiano 84
4.2.5 Bidii 86
4.2.6 Nafasi ya Jinsia ya Kike 88

4.2.7 Umuhimu wa Jina 90
4.2.8 Ugonjwa na Kifo 90
4.2.9 Ushawishi 91
4.3 Jinsi Fani Inavyoendeleza Maudhui katika Fasihi ya Watoto 92
4.3.1 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Familia katika Fasihi ya Watoto 93
4.3.2 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu katika Fasihi ya Watoto 107
4.3.3 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu katika Fasihi ya Watoto 119
4.3.4 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano katika Fasihi ya Watoto 125
4.3.5 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii katika Fasihi ya Watoto 130
4.3.6 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike katika Fasihi ya Watoto 135
4.3.7 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo katika Fasihi ya Watoto 141
4.3.8 Namna Fani Inavyofanikisha Maudhui ya Ushawishi katika Fasihi ya Watoto 143
4.3.9 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Umuhimu wa Jina katika Fasihi ya Watoto 145
4.4 Hitimisho 146
SURA YA TANO 147
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO 147
5.0 Utangulizi 147
5.1 Muhtasari wa Utafiti 147
5.2 Muhtasari wa Vipengele vya Fani Vilivyotumiwa katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto 149
5.3 Muhtasari wa Maudhui Yanayopatikana katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto 151
5.4 Muhtasari wa Jinsi Vipengele vya Fani Vinavyotumiwa Kuendeleza Maudhui katika Fasihi ya Watoto 152
5.5 Hitimisho la Utafiti 154
5.6 Mapendekezo ya Utafiti 155
MAREJELEO 157
VIAMBATISHO 164

Kiambatisho A: Barua ya Utambulisho kwa NACOSTI Kutoka Chuo Kikuu cha Rongo ____ 164
Kiambatisho B: Leseni ya Utafiti Kutoka NACOSTI (Ukurasa wa Mbele) ____ 165
Kiambatisho C: Leseni ya Utafiti Kutoka NACOSTI (Ukurasa wa Nyuma) ____ 166
Kiambatisho D: Idhini ya Utafiti Kutoka NACOSTI ____ 167

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.1: Tashbihi katika Riwaya za Watoto ........ 43
Jedwali 4.2 Taswira katika Riwaya za Watoto ........ 52
Jedwali 4.3: Nahau katika Riwaya za Watoto ........ 59
Jedwali 4.4: Misemo ........ 64
Jedwali 4.5: Methali ........ 67
Jedwali 4.6: Picha ........ 71
Jedwali 4.7: Maudhui katika Fasihi ya Watoto ........ 77

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 4.1: Picha ya Watoto wa Shule Wakishauriwa na Mwalimu (Nimefufuka Uk 18)........ 72
Kilelezo 4.2: Picha ya Mtoto Taabu Akicheza na Mwanasesere (*Nimefufuka* Uk 13) ...... 73
Kielelezo 4.3: Watoto Wakicheza katika Uwanja wa Shule (*Kisasi Hapana* Uk 24)........ 73
Kielelezo 4.4: Picha ya Mama ya Lena Akiwa kwa Mganga ( *Nimefufuka* Uk 7)............. 74
Kielelezo 4.5: Picha ya Mkwea Mlima (*Nimefufuk*a UK 17)........ 75
Kielelezo 4.6: Picha ya Musa, Haki na Ukwa. Musa Anaonekana Akiwa na Nywele Ambazo Hazijachanwa *(Sitaki Iwe Siri* Uk 5)........ 75
Kielelezo 4.7: Picha ya Juma Akishauriwa na Baba Yake (*Wema wa Mwana* Uk 3)...... 116
Kielelezo 4.8: Picha ya Juma Akishauriwa na Mama Yake (*Wema wa Mwana* Uk 4).... 116
Kielelezo 4.9: Picha ya Mwalimu Mkuu Akiwalaki Ngoyoni na Baba Yake (*Wema wa Mwana* Uk 13)........ 117
Kielelezo 4.10: Picha ya Ngoyoni Akishauriwa na Mwalimu Mkuu (*Wema wa Mwana* Uk 18)........ 117
Kielelezo 4.11: Picha ya Ngoyoni Akivalishwa Nembo ya Mwanafunzi Bora *(Wema wa Mwana* Uk 19)........ 118
Kielelezo 4.12: Picha ya Kido na Nyanyake Wakila na Kutambiana Hadithi (Kisasi Hapana Uk 3)........ 118
Kielelezo 4.13: Picha ya Kido na Wenzake Wakicheza (*Kisasi Hapana* Uk 26) ............ 124
Kielelezo 4.14: Picha ya Kido akiwa amebebwa na nyanya, mama na Lukoko (Kisasi Hapana Uk 10) ……………………………………………………………….……128

## VIFUPISHO NA AKRONIMU

| | | |
|---|---|---|
| **ALSTBOIMPS** | **:** | Appoved List of School Text Books and Other Instructional Materials for Primary Schools |
| **CKS** | **:** | Christian Knowledge Society |
| **Dkt** | **:** | Daktari |
| **KBEA** | **:** | Kenya Basic Education Act |
| **KGS** | **:** | Kenya Gazzete Suppliment |
| **NACOSTI** | **:** | National Commission For Science, Technology and Innovation |
| **Prof** | **:** | Profesa |
| **UNICEF** | **:** | United Nations Childrens Fund |
| **Uk** | **:** | Ukurasa |

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Mtoto:** Binadamu aliye kati ya miaka 6 na 18 na aliye katika shule ya msingi.

**Fasihi ya Watoto:** Vitabu vyote vilivyoandikwa kwa ajili ya watoto walio katika shule za msingi.

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imewekea utafiti huu msingi kwa kubainisha usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti na mipaka ya utafiti. Tulifanya hivi ili kuonesha pengo lililohitaji kuzibwa na umuhimu wa utafiti wetu. Pia tumeonyesha nadharia iliyoongoza utafiti wetu, maendeleo yake, mihimili na namna tulivyoitumia katika utafiti wetu.

## 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ya watoto si kongwe sana katika ulimwengu wa fasihi andishi ikilinganishwa na ile ya watu wazima. Upya huu unatokana na sababu kuwa hapo awali hasa kabla ya Karne ya 18, watoto walikuwa wanajumuishwa katika kazi za fasihi za watu wazima. Kwa mujibu wa Cart (2005), akinukuliwa na Andrea (2011), kabla ya kipindi cha kuanguka kwa soko la dunia haikuwepo dhana ya kuangalia watoto au vijana katika jamii. Waandishi waliandika bila kujali uwepo wa makundi hayo yaani watoto na vijana. Bakize (2014) anasema kuwa hali ilianza kuwa tofauti hasa katika karne ya 18 ambapo jamii ilianza kuona kuwa kazi za fasihi zinazowahusu watoto zijitegemee kwani hadhira hiyo ni ya kipekee. Hili liliwezekana mapema katika nchi za kimagharibi kwa sababu asilimia kubwa ya watoto ilikuwa na elimu na uwezo wa kusoma vitabu walivyoandikiwa. Katika sehemu nyingine duniani, mtazamo kuhusu fasihi hii ulichukua muda mrefu. Kwa mfano, Verma (2019) anakiri kuwa katika mwaka wa 2011 alipoanza kufanya uhakiki katika fasihi ya watoto nchini India, kulikuwa na waandishi wachache sana na vitabu vichache mno vilivyokuwa vimeandikwa kwa ajili ya watoto. Hata hivyo, hali hii imezidi kubadilika ambapo waandishi wanaume na wanawake wanazidi kujitokeza katika uwanja huu.

Kuhusu fasihi ya watoto Barani Afrika, Traore (2010) anasema ni katika miaka ya 1980 ambapo fasihi ya watoto ilianza kuota mizizi barani humu. Fasihi andishi ya watoto ya kabla ya kipindi hiki ilitolewa kutoka nchi za Magharibi na Wazungu, na wao ndio walioamua cha kusomwa na hivyo fasihi ya watoto ya Kiafrika haikunawiri wala kupewa kipaumbele. Tatizo lilikuwa kwamba vitabu hivi vilikusudiwa tu kuweka wazi ujinga na ushamba wa Mwafrika au mtu mweusi na kuonyesha kuwa Waafrika walikuwa sawa na wanyama (Khorana, 1994). Alembi (2007) anasema kuwa fasihi ya kipindi hiki ilikuwa na lengo la kumpotosha mtoto Mwafrika kwa sababu ilipuuza tajriba ya mtoto Mwafrika na ulimwengu wake. Ilinuia kuua utamaduni na lugha ya Mwafrika kwa kupendekeza ya Wazungu. Hili lilitia mshawasha katika wasomi wa Kiafrika kuanza kubuni na kujitungia kazi zao wenyewe zilizoakisi utamaduni wao zaidi (Chakava, 1998; Alembi, 2007).

Fasihi ya watoto ya Kiafrika, ilikuwa ni kazi ya fasihi iliyobuniwa kwa kutumia malighafi zinazotokana na mwonoulimwengu wa Kiafrika na iliyoandikwa kwa njia inayoeleweka kwa mtoto wa Kiafrika. Fasihi hii ndiyo inayokuza utamaduni wa mtoto wa Kiafrika na kumwezesha kuthamini mazingira yake na kumburudisha (Osazee, 1991). Waandishi wa Kiafrika wanachukulia hili kwa uzito. Kwa mfano, Heale (1992), akishughulikia uchapishaji na uuzaji wa vitabu vya fasihi ya watoto nchini Afrika Kusini, anataja kuwa katika mwaka wa 1990, vitabu 172 vya fasihi ya watoto vilichapishwa ambapo 76 viliandikwa katika lugha ya Afrikana huku 96 vikiandikwa katika Kiingereza. Mwaka uliofuata wa 1991 vitabu 145 pekee ndivyo vilivyoandikwa. Hata hivyo, baada ya sera ya elimu kubadilishwa, pesa zaidi zilitolewa ili kuchapisha na kununua vitabu vya fasihi ya watoto. Vitabu vingi vya watoto viliandikwa katika lugha za wenyeji kwa sababu watoto katika shule za msingi wanafurahia kusoma katika lugha zao ambazo wanazielewa zaidi.

Wenyeji wanasihiwa kuandika vitabu katika lugha hizi. Hili bila shaka litafanya vitabu vinavyofaa jamii za Kiafrika katika Afrika Kusini kuandikwa (Vuuren, 1994).

Katika Afrika Mashariki, kulingana na Lyimo na wenzake (2018), uandishi wa bunilizi za watoto kwa Kiswahili umeanza kupewa umuhimu baada ya mwaka wa 1960 na kuanza kuongezeka miaka ya 1970 na 1980 kabla ya kushika kasi zaidi katika miaka ya 1990. Nchini Tanzania, hili liliwezekana hasa baada ya mradi wa Vitabu vya Watoto kuzinduliwa mwaka wa 1991. Mradi huu ulifanya fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania kupata mwamko mpya kwa kuwa kulikuwa na michakato rasmi ya kuandaa fasihi kwa ajili ya watoto.

Baada ya Waafrika wakiwemo Wakenya kuamua kuanza kutunga kazi zao za fasihi, eneo lingine tena likafunguliwa ambalo lilihitaji uangalizi. Eneo hili ni uchambuzi na uhakiki wa kazi hizo. Kulingana na Mpesha (1996), fasihi ya watoto inahitaji uhakiki wa kina zaidi hata kuliko ilivyo katika fasihi ya watu wazima kwa kuwa watoto bado wako katika ngazi muhimu zaidi ya kukua. Hata hivyo, hili halijafanyika kwa kiasi kikubwa kwa sababu kulingana na Musau na Ngugi (1997), kati ya tafiti zilizowahi kufanywa katika Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kati ya mwaka wa 1970 hadi 1996, hakuna hata moja iliyohusu fasihi ya watoto. Fasihi ya watoto haikuwahi hata kutajwa na yeyote kuwa ni eneo muhimu la kufanyia utafiti. Tatizo lilikuwa ukosefu wa sera mwafaka ya lugha, ukosefu wa wasomaji au wasomi katika eneo hili na ukosefu wa vitabu (King'ei, 2000). Hata hivyo, kumekuwa na mwamko mpya ambapo kati ya mwaka wa 1990 na 2004, tafiti chache zilifanywa katika fasihi ya watoto (Ngugi, 2011). Miaka saba baada ya utafiti wa Ngugi (Keshatajwa), Lyimo na wenzake (2018) wanasema kuwa tafiti ambazo zimefanywa katika miongo miwili iliyopita ni kumi tu. Hili lilikuwa kama tokeo la waandishi wa fasihi kujikuta wakiandika zaidi kuhusu fasihi ya watoto na vijana kwani kipindi hicho walikuwa

na mwamko wa usomaji sana kutokana na elimu waliyokuwa wanapata. Hata hivyo, hii bado ni kazi kidogo sana katika nyanja hii muhimu kwa sababu Gatere (2020) akiwanukuu Miricho na wenzake (2019) anahoji kuwa maendeleo ya fasihi ya watoto katika karne ya ishirini na moja yamepiga hatua kubwa kiasi cha kukiuka kanuni za fasihi hii kimaudhui kama zilivyowekwa na kuzoeleka katika kazi za miaka ya nyuma na kuwa hili limechangiwa na sera na mifumo ya elimu kuhusu somo la Kiswahili nchini Kenya. Ukilinganisha madai haya na zile tafiti ambazo zimefanywa kuhusu somo hili, basi ni dhahiri kuwa bado tahakiki zaidi kuhusu fasihi ya watoto zinahitajika.

Waandishi wengi pia wameibuka na wametunga kazi nyingi na wanazidi kutunga nyingine mpya za fasihi ya watoto kila uchao. Hili linamaanisha kuwa kazi inazidi kuongezeka kwa wahakiki. Kama asemavyo Mukami (2005), uhakiki wa fasihi ya watoto hauna mipaka, yaani haufanywi wakati mmoja na kuisha kabisa. Mukami (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa hii ni shughuli inayohitaji kuendelea kila wakati muradi kazi za watoto zinazidi kubuniwa. Hili linamaanisha kuwa utafiti katika nyanja hii hauna budi kuendelezwa. Mbuthia na Miricho (2017), wanadokeza uhitaji mwingine kwa kusema kuwa vitabu vya watoto vinapaswa kuhakikiwa kabla ya kuwachagulia watoto wavisome kwa sababu usomaji wa fasihi ya watoto unaweza kuwaathiri watoto kama wasomaji kwa njia chanya au hasi kutegemea wanachosoma, kinavyosawiriwa na kinavyosaidia kujenga uelewa na mitazamo kimaisha. Hii inamaanisha kuwa uhakiki wa kazi hizi una dhima ya kuzitathmini ili kutoa mwangaza na mwongozo wa kuziteua kwa watoto. Kwa hiyo, kazi hii ya kuhakiki fasihi ya watoto haina kikomo mradi vitabu vinazidi kuandikwa. Licha ya jukumu hili muhimu, Wamitila (2010: 324) analalamika kwa kusema kuwa utanzu wa fasihi ya watoto umepuuzwa kwa miaka mingi katika maandishi ya kihakiki huku kazi nyingi

zikishughulikia fasihi ya watu wazima kutokana na imani kuwa fasihi ya watoto haistahiki kuchunguzwa kinadharia au pengine inahusu tu ngano za chura na sungura.

Kulingana na Lyimo na wenzake (2018) tafiti kumi zimefanywa kuhusu fasihi ya watoto. Baadhi ya tafiti hizi zimelenga fani na maudhui. Hata hivyo, kati ya zile zilizochunguza fani na maudhui, zilichunguza vipengele hivi bila kuvitangamanisha ambapo fani imechunguzwa kivyake na vilevile maudhui. Hata katika kazi zilizochunguza vipengele hivi kwa pamoja, kwa ufahamu wetu, hakuna iliyoonesha uhusiano uliopo kati yazo. Hii ndiyo sababu utafiti wetu unanuia kuziba pengo hili kwa kuchunguza jinsi vipengele vya fani vinavyofanikisha maudhui katika fasihi ya watoto. Kwa kufanya hivi, utafiti huu unapiga hatua katika kuendeleza tafiti za awali.

## 1.2 Suala la Utafiti

Fasihi ya watoto ni sehemu muhimu sana ya fasihi kwa ujumla. Fasihi hii inahitaji utafiti zaidi kwa sababu kupitia kwayo watoto wanarithishwa maadili na amali muhimu ambazo nao pia watazipitisha kwa vizazi vinavyofuata (Ogechi na Ogechi, 2002). Kwa hivyo, utafiti wa fani na maudhui katika fasihi ya watoto unahitaji uangalizi zaidi ili kuhakikisha kuwa fasihi waliyoandikiwa ina athari chanya kwa watoto hawa. Tafiti kadhaa zimefanywa kuhusu fani na maudhui katika eneo hili la fasihi. Hata hivyo, tafiti hizi zimeainisha fani na maudhui katika vitabu mbalimbali bila kuonyesha namna fani zinavyofanikisha maudhui. Kwa hiyo, utafiti huu ulifanywa ili kuonesha jinsi fani inavyotumika katika kupitisha maudhui katika fasihi ya watoto.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza madhumuni yafuatayo:

i. Kubainisha vipengele mbalimbali vya fani katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya.

ii. Kujadili maudhui yanayoangaziwa katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya.
iii. Kutathmini jinsi vipengele vya fani vinavyofanikisha maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kujibu maswali yafuatayo:

i. Ni vipengele gani vya fani vilivyotumiwa katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya?
ii. Ni maudhui yapi yanayoangaziwa katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya?
iii. Ni kwa njia gani vipengele vya fani hufumwa ili kufanikisha maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Fasihi ya watoto ni sehemu muhimu ya fasihi. Haviland (1973) anasema fasihi ya watoto inapaswa kutiliwa maanani na wazazi, walimu na washikadau wote kwa sababu wanaweza kuchangia katika kuiendeleza kwa namna mbalimbali. Kwa hiyo, ni muhimu sana fasihi hiyo ifanyiwe utafiti ili kuikuza zaidi. Pia kumetokea waandishi wengi mahiri katika eneo hili la fasihi ya watoto na hivyo kuongeza uhitaji wa kuzihakiki kazi hizi pindi zinapoandikwa ili kufuatilia maendeleo ya eneo hili katika fasihi ya Kiswahili. Umuhimu wa kufanya hivi unatiliwa mkazo na Hunt (2006) na Miricho (2017) ambao wanakazia kuwa ipo haja ya kuchunguza mambo yanayowasilishwa kwa watoto. Kwa hiyo, kuna haja ya kuhakiki vitabu vya hadithi za watoto ili kubaini ni nini kinachosomwa na watoto, kama watoto wanasoma mambo yanayofaa kwa ajili ya kuwajenga kimaadili na kuwapa mielekeo inayofaa ili jamii iwe na vizazi bora vya siku zijazo.

Kati ya tafiti tulizoweza kupata kuhusu fasihi ya watoto, hatukupata iliyochunguza jinsi fani hutumiwa kwa utaalamu ili kufanikisha maudhui katika fasihi ya watoto. Kwa hiyo utafiti huu ulinuia kuweka bayana vipengele mahususi vya fani vinavyotumiwa katika fasihi ya watoto na jinsi vipengele hivyo vya fani huchongwa kwa namna inayofanikisha maudhui katika kazi hizo mahususi.

Mwisho, tulichagua mada hii tukiwa na lengo la kutambua vipengele vya fani na maudhui yanayopatikana katika fasihi ya watoto haswa ile inayotumiwa katika shule za msingi nchini Kenya ili kung'amua kama yanafumbata hali halisi ya mahitaji katika jamii ya kisasa.

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Inatarajiwa kazi hii iweze kutoa mchango katika kuhakiki fasihi ya watoto siku za usoni. Utafiti huu pia unawanufaisha waandishi kwa kuwatazamisha kazi zao ili kuona ubora na udhaifu wa kazi hizo. Walimu na wanafunzi wataweza kuona maudhui na vipengele vya fani katika vitabu tulivyohakiki ili kupata vionjo vya kazi hizo. Wakuza mitaala wanaweza kutumia matokeo ya utafiti wetu wanapoamua vitabu watakavyoteua ili kusomwa na wanafunzi. Washikadau wote wanaweza kupata vionjo vya vitabu tulivyohakiki na hivyo kuwatia mshawasha wa kuvisoma au kuvifanyia utafiti zaidi. Kwa njia hii utafiti huu unatoa mchango katika kuboresha fasihi ya watoto.

**1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Uchunguzi huu ulijikita katika uchanganuzi wa jinsi vipengele vya fani vinavyofanikisha maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufundishia katika shule za msingi. Kwa kuwa vitabu vya fasihi ya watoto ni vingi, tulitafiti tu vile vinavyotumiwa katika shule za msingi nchini Kenya. Aidha, japo kuna vitabu vingi vya fasihi ya watoto, tulichunguza vinne tu ambavyo navyo ni: *Kisasi Hapana* (2014) kilichoandikwa na Ken Walibora; *Nimefufuka* (2011) kilichoandikwa na Rebecca Nandwa; *Sitaki Iwe Siri* (2008) kilichoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* (2012) kilichoandikwa na Nuhu

Bakari. Kutokana na upana wa fani, tulijikita katika vipengele sita vya fani ambavyo ni, methali, nahau, misemo, tashbihi, taswira na picha. Na pia tulishughulikia maudhui na uhusiano kati ya maudhui na fani tulizochagua kutafiti.

## 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuundo. Mwasisi wa nadharia hii, Saussure (1916) akinukuliwa na Koerner (1971), alipendekeza mtazamo mpya kuhusu lugha. Kinyume na wataalamu wengine walioshughulikia historia na sura maalum za lugha fulani, Saussure alivutiwa na miundo inayohimili lugha zote, huku akijaribu kuonyesha kwamba lugha zote za ulimwengu zinaweza kutathminiwa kwa kaida maalum za Umuundo. Alizua dhana za lugha na mfumo lugha kueleza maoni yake.

*Parole* (lugha) au utendaji ni lugha katika matumizi na hiki ndicho walichozingatia wanaisimu wa awali. Lakini Saussure alivutiwa na mfumo wa kinadharia unaounda lugha zote au *langue* (mfumo lugha). *Langue* ni masharti au kaida zinazoiwezesha lugha kuwepo na kuweza kufanya kazi. Mawazo haya yaliendelezwa na Levi-Strauss (1963) katika Koerner (1971), mwanaisimu Roman Jakobson na mwanasaikolojia Jacques Lacan (1970). Kazi ya Saussure ilikuwa imetengewa wanaisimu pekee. Hata hivyo, katika miaka ya 1950, mtazamo huu wa Saussure ulianza kusambaa katika masomo mengine hasa wakati mawazo yake yalipozingatiwa na mwanaanthropolojia Claude Levis Strauss. Kwa kuchukua maoni ya Isimu ya Saussure na kuyaingiza katika Sayansi za Jamii, Claude alitaka kuendeleza dhana kuwa pana viwango viwili katika kuelewa maisha ya jamii, Isimu, Lugha na chochote kingine kile. Viwango hivi ni kiwango cha juujuu na kiwango cha ndani. Mkondo huu wa mawazo ya umuundo kuhusu Sayansi za Jamii ulianza Ulaya na kuathiri mtazamo wa elimu mbalimbali kama vile wa Falsafa, Anthropolojia, Historia, Sosholojia na Uhakiki wa fasihi (Wamitila, 2003; Ntarangwi, 2004).

Kulingana na Wamitila (2003), Umuundo ni aina ya uhakiki unaochunguza kaida zilizopo katika uundaji wa kazi fulani. Ni nadharia inayojibainisha kwa kuangalia ujumla wa uhusiano wa sehemu moja na nyingine katika kufanya kitu kizima. Kwa mfano, muungano wa maneno hufanya sentensi na sentensi zikiungana zinaunda aya huku aya zikiunda sura ambazo hatimaye huunda riwaya.

Chimbuko la Nadharia ya Umuundo ni Urusi kama wanavyosema Fokkema na Ibsch (1995). Wanasema kuwa asili ya Nadharia ya Umuundo ni urasimu wa Kirusi ulioanza kutumika katika uhakiki mnamo mwaka wa 1920. Msimamo wao una uhusiano na madai ya Scholes (1974) anayesema kuwa Nadharia ya Umuundo ina uhusiano wa karibu na Urasimu. Wamitila (2002) anaunga mkono mawazo ya Scholes (1974) kwa kueleza kuwa Nadharia ya Umuundo inahusishwa na wanaisimu wa Shule ya Prague.

Kwa hiyo wafuasi wa Umuundo wanatilia mkazo kwenye umuundo wa kazi yenyewe na kuwa mwandishi hana nafasi. Wanaiona fasihi kuwa imepangwa kama lugha ambayo ina viwango mbalimbali ambavyo kwa ujumla huzaa mfumo wa lugha hiyo. Wanaamini kuwa kazi ya fasihi haihitaji urejelezi wa nje ili kupata maana kwani sawa na lugha, fasihi ina mfumo unaojitosheleza na kuwa neno halihitaji urejelezi ili lipate maana. Nadharia hii humpuuza mwandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mifumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokea katika kazi hiyo. Kulingana na wanaumuundo, viashirii vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa. Wanavutiwa zaidi na jinsi maana inavyoibuliwa au kukuzwa kuliko maana yenyewe (Wamitila, 2003).

### 1.8.1 Mihimili ya Umuundo na Jinsi Ilivyotumiwa katika Utafiti

i. Kulingana na nadharia hii, tunaweza kuangalia jamii katika muundo wake wa kijuujuu na kuielewa. Lakini tukitaka kupata maana mwafaka lazima tuchunguze muundo wake wa ndani, yaani mfumo wake wa lugha ambao hupatikana katika kila

jamii ya wanadamu. Kulingana na mhimili huu, kuangalia fani kivyake na maudhui pia kivyake ni kama kuiona kijuujuu tu. Tuliongozwa na mhimili huu ili kuhakiki madhumuni ya kwanza kwa kudondoa vipengele vya fani ambavyo ni muundo wa ndani wa kazi ya fasihi. Mhimili huu pia ulifaa katika kuhakiki madhumuni ya tatu ya utafiti wetu kwa kuoanisha fani na maudhui ili kuonyesha uhusiano uliopo. Kwa jinsi hii tulipata maana au maudhui yanavyojengwa au kufanikishwa na vipengele mbalimbali vya fani.

ii. Nadharia ya Umuundo inashikilia kuwa katika kupata maana, lazima kuwe na uhusiano wa kipembe tatu, yaani dhana, alama na kitajwa. Kama vile muundo wa lugha ulivyo mfumo, muundo wa fasihi pia una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Katika kazi ya fasihi kuna kitengo cha sanaa kama vile maudhui, ploti, wahusika, muktadha na lugha. Hakuna kipengele cha fasihi kati ya hivi kitakachoelezwa katika upekee wake bali lazima kielezwe kwa kuzingatia kuwepo kwa jukumu la vipengele vingine kwa sababu vipengele vinavyounda kazi hushirikiana, kujengana na kukamilishana ili kuwa kitu kizima. Kwa mfano, katika kueleza ploti, wahusika watashirikishwa na lugha yao kuzingatiwa. Katika utafiti huu mhimili huu umetumiwa kuonyesha kuwa maudhui na fani ni dhana zinazotegemeana na kukamilishana. Pia ushirikiano uliopo baina ya vipengele hivi na unaovikamilisha unaweza kuchunguzwa. Tuliongozwa na mhimili huu kutathmini madhumuni ya tatu ya utafiti kwa kuchanganua data na kuchunguza ni vipi msanii husuka vipengele vya fani ili kuweka wazi maudhui yake katika fasihi ya watoto. Pia inaeleweka wazi kuwa maudhui yanayokusudiwa ndiyo huongoza katika uteuzi wa vipengele vya fani vitakavyotumiwa katika kazi fulani ya sanaa (Wafula na Njogu, 2007).

iii. Nadharia ya umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa na jinsi vinavyohusiana

hadi kuikamilisha kazi hiyo. Huangalia namna sehemu mbalimbali za kazi za sanaa zilivyofungamana. Hata hivyo, sehemu hizo mbalimbali huweza kutenganishwa na kuchunguzwa. Katika utafiti huu, mhimili huu ulitumiwa kuchunguza madhumuni ya kwanza na ya pili kwa kutenganisha fani na maudhui kwa lengo la kuchunguza vipengele hivi kindani. Kila kipengele cha fani kilichoainishwa kilichukuliwa kuwa kitu kizima kinachojisimamia na hivyo kuhakikiwa. Tulichukulia pia kuwa kila maudhui ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii huku yale mawazo madogomadogo yanayochangia hayo maudhui makuu tuliyachukulia kama maudhui madogo. Kwa jinsi hii, maudhui na vipengele vya fani vilichukuliwa kama kitu kizima kinachojisimamia.

iv. Wahakiki wanaoegemea mkondo wa Saussure huzingatia kwamba matini husika ni mfumo unaojisimamia na hivyo basi huwa hamna haja ya kutumia mambo ya nje ili kuhakiki kazi ya fasihi. Wahakiki wanaotumia nadharia hii huzingatia matini kama kiungo kamili kinachoweza kuhakikiwa kivyake na hivyo kupuuza dhana ya jadi kuhusu kile matini hiyo huweza kutueleza kuhusu maisha. Hivyo basi mhakiki hufanya mtindo wa kazi yenyewe kiini cha uhakiki wake. Kwa mujibu wa mhimili huu, tulichukulia fani inayoangaziwa katika madhumuni ya kwanza kuwa kitu kizima ambacho kimeundwa kwa vipengele mbalimbali vya lugha kama vile methali, nahau, misemo, taswira, picha, na tashbihi. Vipengele hivi vya fani (lugha) vilitambuliwa na matumizi yavyo yakafafanuliwa na kuelezwa.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia mambo ya kimsingi katika utafiti huu kwa kuonesha usuli wa mada kwa kutoa mwelekeo wa jamii na historia fupi kuhusu fasihi ya watoto. Imeonesha pengo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na pia sababu za kuchagua mada.

Imeangazia pia upeo na mipaka ya utafiti wetu, umuhimu wa utafiti na nadharia ya Umuundo, mihimili yake na jinsi ilivyotumika katika utafiti.

# SURA YA PILI
# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imeangazia kazi za watafiti wengine katika taaluma ya fasihi zinazohusu maana ya fasihi, dhana ya mtoto, fasihi ya watoto, fani na maudhui. Ingawa utafiti wetu unaangazia fasihi ya watoto na hasa riwaya, hili halikutuzuia kupitia fasihi ya watu wazima na tanzu nyingine za fasihi mbali na riwaya. Kwa kufanya hivi tulinoa uelewa wetu katika nyanja za fasihi ya watoto, fani na maudhui ili kutupatia mwanga zaidi katika taaluma hii ya fasihi ya watoto.

## 2.1 Maana ya Fasihi

Wamitila (2003), Mulokozi (1996, 2017) na Haji (1983) wanakubaliana kuhusu maana ya fasihi kwa kusema kuwa fasihi ni kazi zinazotumia maneno au lugha kisanaa ili kuwasilisha suala fulani kuhusu mwanadamu akiwa maishani mwake, mahusiano yake na viumbe wengine, migogoro yake na mazingira, raha yake, matumaini yake na jinsi anavyopiga hatua katika maendeleo yake. Kazi ya fasihi husukwa kupitia ubunifu na ubunilizi ili kuathiri, kugusa na kuacha athari fulani kwa hadhira. Wanazidi kueleza kuwa fasihi ina tanzu kuu mbili ambazo ni fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi andishi ni fasihi ambayo kimsingi huhifadhiwa kwa njia ya maandishi na ina tanzu kama novela, riwaya, hadithi fupi, tawasifu, insha, mashairi na tamthilia. Ufafanuzi wa wataalamu hawa unaonyesha kuwa fasihi hulenga binadamu na watoto ambao fasihi yao inachunguzwa katika utafiti huu ni sehemu ya hao binadamu wanaorejelewa. Pia, utafiti huu ulihakiki riwaya ambayo ni utanzu mmoja kati ya hizi zinazotajwa na wanafasihi hawa, hususan riwaya za watoto. Vitabu hivi ni muhimu kuchunguzwa kwa vile tunachukulia fasihi asomayo mtoto humwongoza na kumkuza ili kukabiliana na mazingira yake anapoelekea utu uzima.

## 2.2 Maana ya Mtoto

Kulingana na Bakize (2014) na Hunt (1994) dhana ya mtoto ni tata mno hasa inapohitajika kuweka mipaka kwa kutegemea umri, tamaduni mbalimbali na vipindi tofautitofauti vya kihistoria. Dhana hii ya mtoto inaweza kufafanuliwa kwa njia mbalimbali kwa kutegemea Sheria, Dini, Baolojia na hata Saikolojia. Kulingana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Maoni haya pia yanaendelezwa na (Bakize, keshatajwa). Wafula (2011) kwa upande wake anagawanya watu katika makundi manne makuu. Utoto ni kuanzia miaka 0-17, ujana ni kuanzia miaka 18-34, utu uzima ni kuanzia 35 hadi 52 na uzee ni kuanzia 53 kuenda juu. Maoni haya yanaweka umri wa juu wa mtoto kuwa miaka 18 huku wa chini ukiwa sufuri. Hata hivyo Tucker (1981) ametufaa zaidi kwa kuweka umri hususa wa mtoto katika shule za msingi kwa kusema kuwa mtoto ni binadamu ambaye ana umri wa miaka sita aanzapo masomo katika shule ya msingi na miaka kumi na mitatu anapobaleghe. Kwa kusisitiza hili shirika la UNICEF (2009) linaeleza kuwa mtoto katika shule za msingi nchini Kenya anapaswa kuwa kati ya miaka 6 na 13.

Katika utafiti huu tunachukua msimamo kuwa mtoto ni binadamu kati ya miaka sita anapomaliza chekechea na kuingia shule ya msingi hadi miaka kumi na nane kwa sababu tunachunguza fasihi ya watoto inayosomwa na watoto wa shule za msingi na ambao kwa kawaida huwa kati ya miaka sita na kumi na mitatu. Hata hivyo kuna uwezekano wa mtoto kurudia madarasa kadhaa na hivyo kumaliza shule baada ya miaka kumi na mitatu. Hii ni kulingana na K B E A (2012) na K G S (2017), zinazosisitiza kuwa mwanafunzi atakubaliwa kusajiliwa katika shule ya msingi iwapo mwaka anapoanza atakuwa kati ya miaka sita na kumi na mitatu. Kwa maoni yetu basi mwanafunzi huyu anaweza kuwa na umri wa zaidi ya miaka 13 anapohitimu darasa la nane. Maoni haya yanaungwa mkono na Bakize (2018)

anayesema kuwa hadhira ya fasihi ya watoto ni watoto walio kati ya miaka 6-17 kwa sababu hawa ndio wanaoweza kusoma kazi za fasihi inayowalenga na kuzielewa.

### 2.3 Maana na Sifa za Fasihi ya Watoto

Hakuna njia moja mwafaka inayoweza kutumiwa kufafanua maana ya fasihi ya watoto. Kwa hiyo, kuna mikabala anuwai inayoeleza maana ya fasihi ya watoto. Inaweza kufafanuliwa kwa ujumla kuwa chochote kinachoweza kusomwa na watoto na kinaweza kuwa riwaya, ushairi, drama inayokusudiwa watoto au watu wadogo au wachanga kiumri. Pia tunaweza kueleza fasihi ya watoto kama sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe unaowahusu watoto. Anderson (2006) anaeleza fasihi ya watoto kama vitabu vyote vilivyoandikwa kwa ajili ya watoto. Kwa hivyo fasihi ya watoto ni sanaa maalum inayoandikwa kwa ajili ya watoto, hadhira yake ni watoto na msingi wake kidhamira huwarejelea watoto (Wamitila, 2003).

Maoni mengine kuhusu fasihi ya watoto ni kuwahusisha watoto wenyewe katika kubuni kazi zao za fasihi. Kuhusu hili, Bakize (2014) na Miricho (2015) wanasema fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa au kusimuliwa na watoto wenyewe na inahusu watu wa umri wa chini ya miaka 18. Fasihi hii huweza kujumuisha hadithi za watoto, visakale, vitabu vya picha, vibonzo vyenye wahusika watoto na hata drama ambazo zimetungwa kwa ajili ya watoto wadogo na vijana. Fasihi hii ni lazima iwe na dhamira rahisi, lugha yake iwe sahili na nyepesi kuelewa. Kwa hivyo, katika utafiti hu tulichukulia fasihi ya watoto kuwa ni sanaa itumiayo lugha sahili kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo na umri wa kati ya miaka 6 na 18. Ingawa fasihi tuliyochunguza haikuandikwa na watoto, ufafanuzi huu ulitusaidia kujiwekea mipaka kuhusu vitabu tulivyoteua ili kutafiti.

Katika uandishi wa fasihi ya watoto vigezo maalum vinatumika katika kuainisha kitabu na kukiita kitabu cha watoto. Mvuto na upokezi wa mtoto kwa kitabu ni miongoni mwa vigezo

muhimu katika fasihi ya watoto. Hili linapaswa kuzingatiwa na mwandishi wa fasihi ya watoto kwa sababu jinsi mwandishi anavyoiandika kazi ya mtoto huweza kuwa na athari kubwa kwa mtoto ambaye anasoma kazi hiyo (Mukami, 2005). Ili kutimiza hili fasihi hii lazima iwe na mhusika mkuu akiwa mtoto au kijana, dhamira iwe inayowahusu watoto, iwe na mtazamo wa watoto, iwe na wahusika mashujaa wakiwa watoto, iwe na wahusika wema na waovu, wahusika wanyama wapewe uhai kama binadamu, lugha iwe rahisi, sentensi ziwe sahili, mada iwe ya kuwavutia, kazi yenyewe iwe fupi na ya kiutendaji. Kwa hivyo ikiwa mwandishi ataandika kazi inayoendana na fikira zao basi atakuwa amefanikiwa kuiteka saikolojia yao kwa sababu mtazamo wao ni tofauti na ule wa watu wazima (Davies 1973, Wamitila 2002). Maelezo haya yalitusaidia katika utafiti wetu kwa kutuonyesha sifa za fasihi ya watoto na tukahakikisha kuwa vitabu tulivyoteua vilistahili kuingia katika kundi la fasihi ya watoto.

Pearson (2012) na Bakize (2014) wanasema kuwa kazi za fasihi za watoto sharti ziwe na michezo kwani watoto hupenda sana michezo. Fasihi hii ya watoto inapaswa kuwa na picha na michoro hasa ya rangi, hili hufanya watoto kutosahau kwa urahisi na kuhusisha matukio katika hadithi na ulimwengu halisi. Ni muhimu pia fasihi hii kuwa na taharuki na fantasia kwa sababu fantasia huleta mvuto wa pekee na kuwafanya kufurahia sana. Mwega wa fasihi hii kidhamira ni watoto wenyewe, huwa na lugha nyepesi, zina motifu ya safari, huwa fupi, huwa na wahusika bapa, wahusika wakuu huishia katika ushindi, huwa na muundo sahili na huwa na mwingiliano tanzu.

Wamalwa (2015) anaongezea sifa za fasihi ya watoto ambazo ni pamoja na kuwa na msuko mwepesi ili kumwezesha kufuata matukio yenyewe, maandishi huwa makubwa yanayoweza kuonekana, maandishi hutiwa rangi ili yavutie macho ya watoto, kuvuta makini na kuwachochea kusoma kazi teule. Wamalwa anaendelea kudai kuwa fasihi ya watoto

aghalabu huhusiana na tungo fupi, husheheni vielelezo, picha au michoro yenye rangi, hutumia wahusika wakuu watoto na wahusika wanyama wanaozungumza na kutenda kama wanadamu.

Wataalamu hawa walitusaidia kupata sifa zaidi za fasihi ya watoto na hivyo tukalinganisha sifa walizotaja na vitabu tulivyoteua ili kuhakikisha kuwa vilifaa na kustahili kuwekwa katika kundi la fasihi ya watoto (Vuuren, 1994). Kutokana na maelezo haya pia tulipata kuwa picha zina umuhimu mkubwa katika kazi za watoto na tukaziteua kati ya vipengele vya fani tulivyokuwa tunachunguza. Hata hivyo tulitoa maelezo kuzihusu na kisha tukaonyesha zinavyochangia kufanikisha maudhui.

## 2.4 Aina za Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ina migawanyo mbalimbali kwa kutegemea maoni ya mtaalamu. Breitsprecher (2005) na Kelley (2014) wanagawa fasihi ya watoto katika aina zifuatazo: vitabu vya picha ambavyo huweza kufunza alfabeti na hata kutoa hadithi fulani kwa kutumia picha tu bila maandishi. Aina nyingine ni vitabu vya picha zinazoandamana na hadithi. Pia, kuna fasihi ya kimapokeo ambayo ni vitabu vinavyotoa hadithi fulani kutoka kizazi kimoja hadi kingine na zinatia ndani ngano, visasili, mighani na kadhalika. Kuna vitabu vya futuhi ya kihistoria ambavyo huwa na wahusika ambao huwa halisi na huzungumzia matukio halisi maishani na kutoa historia kwa mkabala wa kitoto. Kuna vitabu vya ujuzi ambavyo havitumii ubunilizi bali hutoa habari ya kweli jinsi ilivyo. Vitabu vya wasifu na tawasifu hutoa habari za kweli kuhusu watu wengine. Vitabu vingine vya fasihi ya watoto ni kama komedia, vitabu vya kijasusi, komedia ya kijasusi, ushairi na drama.

Kulingana na LibApp (2018), aina za fasihi za watoto ni kama wasifu, tawasifu, ushairi wa watoto, hadithi za watoto, hadithi za wanyama, riwaya za kifantasia, riwaya, fasihi simulizi, riwaya za kihistoria, historia, bunilizi za vijana, riwaya za kisayansi na riwaya za vijana.

Cullinan na Galda, (2002) nao wanagawa fasihi ya watoto katika makundi kama vitabu vya picha, ushairi, fasihi simulizi, fantasia, bunilizi za kisayansi, bunilizi za kihalisia, bunilizi za kihistoria na wasifu. Uainishaji huu ulitufaa katika utafiti wetu kwa sababu ulitusaidia kutambua na kuainisha vitabu kwa misingi na mapendekezo ya wataalamu hawa. Vitabu tulivyoteua ili kuvifanyia uhakiki ni *Kisasi Hapana*, *Nimefufuka*, *Sitaki Iwe Siri*, na *Wema wa Mwana*.

**2. 5 Manufaa ya Fasihi ya Watoto**

Kulingana na Odaga (1985), fasihi huwasaidia watoto kutamalaki hulka nzuri na kuwaepusha na tabia mbaya. Kwa hivyo fasihi ya watoto humpatia mtoto nafasi ya kutoa maoni yake kuhusu kazi fulani ya fasihi na hivyo kukuza uwezo wake wa kiakili. Jambo la pili ni kumpatia mtoto nafasi ya kujua utamaduni wa jamii yake na ule wa jamii nyingine na hivyo kuboresha mtagusano. Fasihi hii pia huwapatia nafasi ya kukua katika uwezo wao wa kihisia na kiadili, husaidia mtoto kuwa mbunifu, kukuza utu wake binafsi na kisha kumsaidia kurithishwa utamaduni wa kusoma (Norton, 2010).

Hunt (1994) na Ngugi (2011) wanasema kuwa dhima ya fasihi ya watoto ni pana kwa kuwa inategemea mahitaji husika na kwa vipindi tofauti na kuwa baadhi ni nzuri kwa kupitisha muda, vingine ni vizuri kwa kupata elimu, kupanua uwezo wa kufikiri, kurithisha tamaduni na maadili ya jamii, kupambana na masuala au matatizo mbalimbali kama magonjwa, kujiburudisha, kuchachawisha ubunifu, kusaidia watoto kujielewa, kuwaelewa watu wengine na kupata uzoefu wa kuelewa umbo la lugha. Kwa njia hiyo mtoto hupata maonyo, mawaidha, mila za jamii, makatazo na maelekezo ili kuyaendeleza, kuyadumisha na kuyahifadhi.

Matundura na wenzake (2013) wanasema kuwa fasihi ya watoto ni swala nyeti kwa sababu fasihi hiyo hutoa mchango mkubwa katika kukuza taswira ya watoto kuhusiana na maisha yao wenyewe na ulimwengu pindi watakapokuwa watu wazima. Fasihi hii pia huwapa watoto maarifa na ukweli kuhusu hatua za maendeleo yaliyofikiwa katika jamii zao, kuelewa mazingira ya nyumbani, jamii zao na ulimwengu kwa ujumla. Kwa upande mwingine, Anderson (2012) na Gatere (2020) wanasema fasihi ya watoto humpatia mtoto raha ya kusafiri katika ulimwengu wa kibunifu, hukuza utamaduni na mwelekeo unaofaa wa kusoma, kuimarisha uhusiano kati ya mtoto na yule anayemsomea, hukuza uwezo wa mtoto wa kufikiri, humpatia mtoto msamiati mpya na kaida. Pia, wanaongezea kuwa fasihi hii hupanua ubunifu wao, hupanua upana wa umakinifu wao, huwasaidia kuwa na hisia mwenzi, kuwafunza namna ya kushughulikia matatizo yao, kupanua mwonoulimwengu wao, kukuza hamu katika mambo mapya, na kufanya historia kuwa halisi zaidi kwao.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, ni wazi kuwa fasihi ya watoto ni uwanja mkubwa na ina manufaa makubwa kwa watoto wenyewe wanapozidi kukua na hivyo kuwaandaa kukabiliana na changamoto za utu uzima. Kwa hivyo, hili lilizidisha azimio letu la kuitafiti kwa sababu kufanya hivyo kuna faida.

## 2.6 Historia ya Fasihi ya Watoto

Kwa muda mrefu fasihi ya watoto ilikuwa ni hadithi za kusemwa, nyimbo na mashairi ambayo yalitumiwa kuelimisha, kuelekeza na kuwatumbuiza watoto. Kufikia Karne ya 18 wakati neno utoto lilipoanza kutumiwa ndipo fasihi ya watoto ilipoanza kujitokeza ikiwa na migawanyo yake, matarajio yake na kaida zake. Aries (1962) anasema kuwa dhana ya utoto ilitokea tu katika enzi za hivi karibuni na kwa kipindi kirefu watoto hawakuonwa kuwa tofauti sana na watu wazima na hivyo hawakupewa fasihi zao za kipekee. Kwa sababu hiyo, fasihi za watoto zilizokuwapo ni zile zilizoandikwa na makasisi. Hakukuwapo fasihi

mahususi iliyokuwa inalenga watoto kabla ya Karne ya 18. Wazo hili linaungwa mkono na Vuuren (1994) na Bakize (2014) wanaosema kuwa fasihi ya watoto bado ni ngeni na ugeni huu unatokana na hali kwamba hapo awali kabla ya karne ya 18 watoto walikuwa wanajumuishwa katika kazi za fasihi za watu wazima kwa jumla. Watunzi na wachambuzi wa kazi za fasihi walikuwa wanamchukulia mtoto kama hadhira au msomaji mwingine tu. Hali hii ilianza kuwa tofauti hasa katika karne ya 18 ambapo jamii ilianza kuona kuwa kazi za fasihi zinazowahusu watoto zijitegemee kwani hadhira hiyo ni ya kipekee. Fasihi ya watoto kabla ya karne ya 18 ilikuwa na lengo la kuendeleza maadili kupitia kwa elimu na masomo ya kidini. Katika kuendeleza lengo hili, kila utamaduni ulikuwa na ngano zake zilizotumiwa kutimiza mahitaji haya mbali na kutumbuiza na kuelimisha. Wahindi walikuwa na hadithi za *Panchontantra*, Wapersia walikuwa na Ngano za *Asurik Tree* huku Wagiriki pia walikuwa na hadithi za *Iliad* katika Karne ya Tano. Watoto Waroma na Wagiriki walifurahia kusikiliza hadithi za akina *Odyssey* na *Esopo* zilizoandikwa na Hommer hata ingawa zililenga watu wazima.

Katika karne ya 18 dhana ya utoto ilianza kuchipuka kule Ulaya ambapo watu walianza kuona watoto kuwa viumbe tofauti wasio na hatia na waliohitaji ulinzi na mazoezi kutoka kwa watu wazima waliowazunguka. Hunt (1994) anasema kuwa mwasisi wa fasihi ya watoto John Locke alishikilia kuwa akili ya binadamu ni ombwe tupu wakati wa kuzaliwa na haina sheria zozote za kuongoza mifumo ya kuandaa data. Sheria hizo huongezwa kila anapoongezeka katika tajriba yake. Kwa kuwa akili ya mtoto ni ombwe tupu, John Locke alipendekeza kuwa ni jukumu la mzazi kujaza ombwe hili na habari zinazofaa. Ili kutimiza hili wazazi wanapaswa kuwaandalia watoto wao vitabu vilivyo rahisi kusoma na vinavyopendeza ili kukuza akili zao badala ya kutumia nguvu kuwafundisha. Kwa hivyo

Locke ndiye aliyekuwa wa kwanza kupendekeza fasihi za picha ziandaliwe kwa ajili ya watoto. Kuanzia wakati huo fasihi ya watoto imekuwa ikiboreshwa hadi sasa.

Kulingana na Njoroge (1978), fasihi ya watoto ya kabla ya ukoloni hapa Afrika ilikuwa ni fasihi simulizi na ndiyo iliyopatikana kwa watoto kwa urahisi. Charo (1976) na Mbure (1997) wanasema kuwa usimulizi wa hadithi ulikuwa ndiyo njia ya pekee iliyotumiwa kutolea elimu kabla mataifa ya kigeni kuvamia Afrika. Waliopewa jukumu hili walikuwa wazee. Fasihi hii simulizi ndiyo iliwafunza watoto kaida za jamii kama ustahimilivu, uaminifu, utiifu, bidii, ukarimu na kadhalika. Pia iliwakanya dhidi ya uchoyo, kutotii, kusema uongo na madhara yake. Kwa jinsi hii mtoto alijifunza yale yaliyoonwa kuwa mazuri na mabaya, namna ya kuhusiana na wengine na pia kutunza mazingira. Kwa hivyo fasihi hii ilikidhi mahitaji ya watoto vya kutosha.

Osazee (1991) anasema kuwa fasihi ya watoto ya Kiafrika ni kazi iliyobuniwa kwa kutoa malighafi yake kutokana na mwonoulimwengu wa Kiafrika na iliyoandikwa kwa njia ya kwamba mtoto Mwafrika anaweza kuielewa. Inapaswa kukuza utamaduni wa Kiafrika unaomwezesha mtoto au kijana Mwafrika kuthamini mazingira yake na impatie raha. Hii ndiyo sababu katika utafiti huu tulishughulikia fasihi ya watoto nchini Kenya kwa sababu kwa njia fulani itamsaidia Mtoto Mkenya kujielewa na kuelewa mazingira yake.

Heale (1992), akishughulikia uchapishaji na uuzaji wa vitabu vya fasihi ya watoto nchini Afrika Kusini, anataja kuwa katika mwaka wa 1990, vitabu 172 vya fasihi ya watoto vilichapishwa ambapo 76 viliandikwa katika lugha ya Afrikana huku 96 vikiandikwa katika Kiingereza. Mwaka uliofuata wa 1991 vitabu 145 pekee ndivyo vilivyoandikwa. Hata hivyo baada ya sera ya elimu kubadilishwa, pesa zaidi zilitolewa ili kuchapisha na kununua vitabu vya fasihi ya watoto. Vitabu vingi vya watoto viliandikwa katika lugha za wenyeji kwa

sababu watoto katika shule za msingi wanafurahia kusoma katika lugha zao ambazo wanazielewa zaidi. Wenyeji wanasihiwa kuandika vitabu katika lugha hizi. Hili bila shaka litafanya vitabu viandikwe vinavyofaa jamii za kiafrika katika Afrika Kusini (Vuuren, 1994).

Kulingana na Lyimo na wenzake (2018), nchini Tanzania uandishi wa bunilizi za watoto kwa Kiswahili umeanza kupewa umuhimu baada ya mwaka wa 1960 na kuanza kuongezeka miaka ya 1970 na 1980 kabla ya kushika kasi zaidi katika miaka ya 1990 hasa baada ya mradi wa Vitabu vya Watoto kuzinduliwa mwaka wa 1991. Mradi huu ulifanya fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania kupata mwamko mpya kwa kuwa kulikuwa na michakato ya kuandaa rasmi fasihi kwa ajili ya watoto. Hata hivyo maendeleo yalikuwa ya polepole sana kwa kuwa Bakize (2013) anasema kuwa kufikia mwaka wa 2013 kazi za watoto kama mashairi, riwaya na tamthilia zilikuwa bado hazijajulikana sana katika maeneo mengi nchini Tanzania.

Historia ya fasihi ya watoto nchini Kenya ina awamu tatu: kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni (Odaga, 1985). Kabla ya ukoloni kama ilivyokuwa katika tamaduni zote Afrika watoto walifundishwa maadili kupitia kwa Fasihi Simulizi. Katika kipindi cha majilio ya wageni kulikuwapo na mkusanyo wa vitabu vya hadithi za Kiswahili vilivyokusanywa na wageni. Vitabu hivi vilikuwa *Swahili Tales as Told by Natives of Zanzibar* kilichoandikwa na Edward Steere mwaka wa 1870 na *Kibaraka Swahili Stories* kilichoandikwa na University Mission Zanzibar katika mwaka wa 1885. Vitabu vingine vilivyotafsiriwa ni kama *Hekaya za Abunuwasi* katika mwaka wa 1935 na *Alfu Lela Ulela* katika mwaka wa 1922 vilivyoandikwa na Johnson na Bren. *Mashimo ya Mfalme Sulemani* na *Safari za Guliver* vilivyoandikwa na F Johnson katika mwaka wa 1929, *Safari za Msafiri* kilichoandikwa na Bunyan katika mwaka wa 1888 (Bertoncini, 1998). Wakati huu wa

ukoloni pia vitabu vya watoto katika Kiswahili viliandikwa kuanzia 1901 na vilikuwa vya shule za Jumapili na hivyo vilikuwa fasihi ya kidini. Mfululizo wa vitabu vya *Kusoma kwa Watoto Siku ya Jumapili* viliandikwa na C K S. Baadaye vitabu vya watoto visivyokuwa vya Kikristo kama vile *Paka Jimi* (1945) na *Mbwa Tom* (1946) viliandikwa na Isabela Fremont.

Tatizo lilikuwa kwamba vitabu hivi vilikusudiwa tu kuweka wazi ujinga na ushamba wa Mwafrika au mtu mweusi na kuonyesha kuwa Waafrika walikuwa sawa na wanyama (Khorana, 1994). Alembi (2007) anasema fasihi ya kipindi hiki ilikuwa na lengo la kumpotosha mtoto Mwafrika kwa sababu ilipuuza tajriba ya mtoto Mwafrika na ulimwengu wake. Ilinuia kuua utamaduni na lugha ya Mwafrika kwa kupendekeza ya Wazungu. Sababu ilikuwa kwamba fasihi ya kipindi hiki ilitolewa nje na Wazungu na wao ndio waliamua cha kusomwa na hivyo fasihi ya Kiafrika haikunawiri na haikupewa kipaumbele. Hili lilitia mshawasha katika wasomi wa Kiafrika kuanza kubuni kazi zao wenyewe zilizoakisi utamaduni wao zaidi. Vitabu vya mwanzoni kuandikwa katika lugha ya Kiswahili ni kama *Adili na Nduguze* kilichoandikwa mwaka wa 1952 na Shaaban Robert , *Kurwa na Doto* kilichoandikwa 1960 na Mohamed Saleh Farsy. Vitabu hivi viliandikwa nchini Tanzania na vilitumiwa pia nchini Kenya. Ni kweli kuwa vitabu vya kipindi hiki havikukusudiwa watoto ingawa vimekuwa vikitumiwa na watoto (Chakava, 1998).

Ngugi (1981) anasema baada ya uhuru kulikuwa na fasihi za Kiingereza kutoka kwa waandishi kama vile Aeschylus, Sophocles, Montaigne, Shakespeare, Tolstoy na Ibsen. Vitabu vyao vilikuwa na utamaduni wa kigeni na hivyo watoto walihitaji kusoma utamaduni wa kigeni. Hata hivyo waandishi wa Kiafrika walijitokeza sana katika kipindi hiki cha baada ya uhuru. Wataalamu kama Grant Kimenyu, Van Zivimu, Ezekiel Mphalele, Taaban Lo Liyong, Okot P'Bitek, Owuor Anyumba na Ngugi wa Thiongo walipigania kuondoa

kasumba ya uzungu katika fasihi ya Kiafrika (Nandwa, 1994). Mukami (2005) anawataja waandishi wa fasihi ya watoto kama Matindi (1968), aliyeandika kitabu *Jua na Upepo*, Ndung'u (1967), aliyeandika kitabu *Hadithi* chenye mkusanyo wa hadithi na Amir (1982), aliyeandika *Hadithi za Wahenga.* Gachukia na Akivaga (1978) wanasema vitabu vingi vya kipindi hiki viliandikwa katika Kiingereza na vichache katika Kiswahili. Vitabu hivi vilikuwa na maudhui kama madhara ya ukoloni, kujikomboa na ukoloni, miji na madhara yake, maadili ya Kiafrika na kadhalika. Lengo lilikuwa ni kufanya Waafrika kuwa na mwonoulimwengu wa Kiafrika ili wajielewe vizuri zaidi.

Fasihi ya Kiswahili kwa jumla pamoja na ile ya watoto ilipata pingamizi kubwa kutoka kwa kampuni za uchapishaji za kigeni ambazo hazikupendelea fasihi za Kiafrika. Kampuni hizo zilikuwa Oxford, Macmillan, Longhorn, Heineman, na Evans Brothers. Hata hivyo Heinman na Longhorn zilitwaliwa na Waafrika na kisha East African Publishers ikaanzishwa mwaka wa 1982. Kampuni hizi zilihakikisha kuwa zilikuwa na vitabu vya fasihi ya watoto. Kwa mfano mfululizo wa *Phoenix Young Readers* na *Hadithi za Kikwetu* ni vitabu vya watoto kutoka kampuni ya Phoenix. Longman nao walianzisha vitabu kama *Utamu Kolea* na *Sasa Sema*. Vitabu hivi vina utamaduni wa Kiafrika zaidi.

Matatizo mengine yaliyokabili fasihi hii yalikuwa kutofunzwa kwa fasihi hii shuleni katika viwango vyote, kutungwa kwa kazi zao na watu wazima, ukosefu wa uhalisia katika kazi walizotungiwa, watoto kupenda mambo ya teknolojia kuliko kusoma vitabu walivyotungiwa, upungufu wa maktaba, baadhi ya kazi walizotungiwa zilikuwa ngumu kuelewa, ugumu wa kuweka mipaka kati ya fasihi ya watoto na ya watu wazima, ukosefu wa mwitikio wa wazazi kuendeleza vipaji vya wanao (Vuuren, 1994). Licha ya matatizo mbalimbali, fasihi ya watoto imepiga hatua kubwa. Kuanzia miaka ya 1990 kumeibuka na kukuwa kwa waandishi wa kazi za fasihi ya watoto na vijana. Kwa mfano, *Ngome ya Mianzi*

*(1990*) na *Mtoto wa Mianzi (1996)* vilivyoandikwa na Mulokozi, na *Mwendo* (1998) kilichoandikwa na E. Lema. Hata hivyo bado kuna haja ya kuimarisha fasihi hii zaidi kwa kuihakiki na kuitathmini. Utafiti huo unafaa kulenga nyanja zote za fasihi ya watoto, fani na maudhui kwa sababu kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili kurithisha watoto maadili yanayofaa (Ogechi na Ogechi, 2002).

Ilikuwa muhimu kuchunguza historia ya fasihi ya watoto kwani kufanya hivyo kulitudhihirishia kuwa fasihi hii imepiga hatua kubwa na kwa sasa kuna vitabu vingi vya nyanja hii. Ndiposa lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchangia katika kuboresha fasihi hii ya watoto kwa kuhakiki namna fani zinazotumiwa zinavyochangia katika kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.

## 2.7 Vipengele vya Fani katika Fasihi ya Watoto

Fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazotumia mwandishi kuiwasilisha dhamira na maudhui yake kwa msomaji. Mwandishi hawezi kusema analotaka kulisema bila ya kuitumia lugha. Lugha hiyo huwa na sifa fulani. Kwa mfano, ina vikolezo au vitia ladha fulani, imesheheni au kujaza mbinu za kila aina na kadhalika. Vipengele muhimu vya fani ni kama muundo, mtindo, mandhari, mtiririko, tamathali za usemi, matumizi ya lugha, wahusika, uhusika, takriri, kuchanganya ndimi, majazi, taswira, picha na michoro (Wamitila, 2010). Huck (2001) na Wamitila (2010) wanapiga hatua na kusema kuwa mtindo anaotumia mwandishi lazima uwe na uwiano na hadithi yake katika upande wa ploti, maudhui, wahusika, mandhari na tamathali za usemi. Tamathali hizo pia zinafaa ziendane na umri wa watoto na zitumiwe kwa hadhari ili zisiwe nyingi kiasi cha kumfanya mtoto kutoelewa ujumbe. Hii ina maana kuwa fani hutokea kama wenzo wa kudhihirisha maudhui. Kwa hiyo, ni lazima fani zichaguliwe kwa makini ili kumfaa mtoto.

Kulingana na Mulokozi (1989), tamathali za usemi ni tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya jamii. Tamathali za usemi zinapotumiwa katika kazi ya fasihi huibusha taswira mbalimbali katika akili ya msomaji na kumwezesha kuelewa ujumbe kikamilifu. Tamathali hizi ni tashbihi, sitiari, tashihisi, taniaba, taashira, majazi, lakabu, tabaini, tashtiti, tanakali za sauti, chuku, kinaya, dhihaka, methali, nahau, misemo, taswira, taharuki, mvutano na kadhalika (Njagi, 2002). Katika fasihi ya watoto, mwandishi hapaswi kutumia tamathali nyingi za usemi kwa sababu watoto hupenda mambo watakayoelewa kwa urahisi na kufurahia (Huck, 1967). Hii ndiyo sababu Wambua (2001) anasema kuwa mambo yanayoamua uteuzi wa tamathali ni kama vile umri, tabaka, kiwango cha elimu cha walengwa, uana, imani na itikadi za jamii. Hii ina maana kuwa mwandishi wa fasihi ya watoto ana mipaka katika mbinu atakazotumia katika kazi yake. Anapaswa kutumia mbinu ambazo ni nyepesi, zinazoeleweka na zinazorejelea mambo yanayopatikana katika mazingira anamoishi mtoto anayelengwa. Ili kutimiza hili, Bakize (2014), anapendekeza kuwa mbinu zinazotumiwa kutunga fasihi ya watoto ni kama matumizi ya vielelezo, michoro, picha, mwingilianotanzu, taharuki, motifu ya safari na msako, mambo ya kitoto kama michezo ya watoto, fantasia na kadhalika.

Swala la fani limeshughulikiwa katika fasihi simulizi inayowalenga watoto. Kwa mfano, Gituku (1990) ameshughulikia maigizo ya kiutamaduni ya watoto nchini Kenya kama mbinu ya kufundishia. Yeye ametafiti fasihi simulizi na kuonesha jinsi maigizo yanavyoweza kuwa wenzo mwafaka wa kufundisha watoto. Katika kazi hii pia ameonesha namna fani mbalimbali hujitokeza katika maigizo na hivyo kuwa wenzo mwafaka wa kufunza fani hizo. Kazi hii inahusiana na yetu kwa sababu ametazama fani ambayo sisi pia tunahakiki. Tofauti na kazi hii ya Gituku (keshatajwa), utafiti wetu ulitazama fani katika fasihi andishi hasa ya watoto na ukaonyesha namna fani hufanikisha maudhui.

Alembi (1991) na Okhoba (1995) wamefanya utafiti wa mtindo na kuonesha fani zinazotumiwa katika mashairi ya watoto. Utafiti wao unafanana na wetu kwa sababu wameshughulikia fani ambayo utafiti wetu pia unaangazia. Hata hivyo, utafiti wetu ulitofautiana na huu kwa sababu tulichunguza fani katika riwaya huku wao ukichunguza ushairi. Pia, utafiti huu unapiga hatua na kuonyesha jinsi fani hizo zinavyofanikisha maudhui.

Katika kutafiti mvuto, upokezi na athari ya fasihi kwa watoto, Weche (2000) ameshughulikia fani katika fasihi simulizi na jinsi fani zinavyosaidia watoto kuipokea fasihi simulizi. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu yeye ameshughulikia namna fani zinavyosaidia katika upokezi lakini katika utafiti huu tulitazama jinsi fani zinavyofanikisha maudhui. Ingawa ametaja vipengele fulani vya kimtindo, vipengele hivyo ni katika fasihi simulizi huku katika utafiti huu tumeshughulikia fasihi andishi ya watoto.

Matundura (2007) ameshughulikia taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto. Yeye ameshughulikia jinsi wahusika wa kike na kiume wanavyosawiriwa katika vitabu vya fasihi ya watoto na iwapo wamesawiriwa kwa jinsi sawa. Hata ingawa ameshughulikia kwa kina kipengele cha uhusika, kazi yetu ni tofauti na yake kwa sababu tunaangazia vipengele kama methali, misemo, nahau, taswira, picha na tashbihi. Hata hivyo, kazi hii ilitusaidia kusuka uhusika katika kazi yetu. Katika utafiti huu pia tumepiga hatua na kuonesha jinsi vipengele vya fani tulivyotea vinavyofanikisha maudhui katika fasihi ya watoto.

Pearson (2012) alifanya utafiti kuhusu fasihi ya watoto nchini Uingereza na ameshughulikia maswala kama umuhimu wa fasihi ya watoto, aina za fasihi ya watoto, muundo, maudhui, migogoro, ploti na usimulizi katika fasihi ya watoto. Kazi hii ilitusaidia katika maswala ya fani kwa sababu ameonesha kuwa muundo katika fasihi ya watoto unapaswa kuwa sahili.

Tulitumia maoni yake na kutoa mifano ya fani kutoka kwa vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa na watoto katika shule za msingi nchini Kenya.

Mutua (2014) ameshughulikia fani za fasihi zinazoibua fantasia katika hadithi za watoto za "Nyambura Mpesha." Katika kazi hii, ameonesha matumizi mengi ya fantasia na jinsi fantasia hizo zinavyojengwa kupitia mandhari mbalimbali. Tofauti na yeye, katika utafiti huu tumeshughulikia maudhui na vipengele mbalimbali vya fani kama methali, misemo, nahau, taswira, picha na tashbihi. Kisha, tukaonesha jinsi vipengele hivyo vya fani vinavyosaidia katika kueleza maudhui katika fasihi ya watoto.

## 2.8 Maudhui katika Fasihi ya Watoto

Ntarangwi (2004) anasema kuwa maudhui ni kile kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maaudhui pia yanaweza kufafanuliwa kuwa yaliyomo au jumla ya mambo yote yanayozungumzwa katika kazi yoyote ya fasihi na hutumiwa kwa upana kujumlisha dhamira, falsafa, itikadi, maadili na msimamo (Msokile, 1992; Wamitila 2002; Wamitila, 2003).

Njogu na Chimera (1999) na  Cass (1967) nao wanasema kuwa maudhui ni jumla ya mawazo mapana yanayoshirikishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelea. Mawazo haya huweza kuwa ya kila aina kutegemea lengo la mwandishi na hadhira anayotaka kuifikia. Kwa sababu hii, mwandishi wa fasihi ya watoto anaposhughulikia maudhui katika kazi yake anapaswa kushughulikia masuala yanayoleta burudani kwa watoto, yanayowaletea manufaa na yenye azma kwao. Kwa  upande wao, Syambo na Mazrui (1994) wanapendekeza maudhui katika kazi ya fasihi yawe ya kuonya, kutahadharisha, kukashifu, kuburudisha, kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo miongoni mwa mambo mengine.

Maelezo ya wataalamu hawa wa fasihi yalitupatia mwanga wa jinsi ya kutambua maudhui katika kazi za fasihi na tukatumia mapendekezo hayo katika kuainisha maudhui kati fasihi ya watoto tuliyokuwa tunachunguza. Kisha, tukapiga hatua kwa kuchunguza jinsi fani mbalimbali zilizotambuliwa zinavyofanikisha maudhui hayo.

Mukami (2005) ameshughulikia uhalisi na mtindo unavyoendelezwa katika vitabu vya Ken Walibora vya *Ndoto ya Amerika* (2001), *Mgomba Changaraweni* (2003) na *Mtu wa Mvua* (2003). Ameorodhesha maudhui kama haki, utu, ukweli, busara, msamaha, utovu wa adabu, unafiki, uongo, uasi, wizi, utii, uhusiano mwema na ukweli. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa kuwa amechunguza maudhui na fani katika kazi za Ken Walibora, msanii ambaye utafiti huu pa unaangazia. Hata hivyo, katika utafiti huu tulitafiti maudhui katika kazi za waandishi wanne. Maudhui tuliyoshughulikia pia ni tofauti ambayo ni familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, ushawishi, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo. Tumetofautiana na mtafiti huyu pia kwa kuonyesha jinsi fani zinavyotumiwa ili kueleza maudhui hayo tuliyohakiki katika vitabu vya watoto tulivyoteua.

Utafiti wa upokezi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto katika shule za msingi nchini Kenya umeshughulikiwa na Karuga (2005). Mtafiti huyu ameshughulikia vigezo vinavyofaa kuangaliwa wakati wa uteuzi wa fasihi ya watoto. Ametaja vigezo kama wahusika, maudhui, ploti, mtindo, umbo na mandhari katika fasihi ya watoto. Utafiti huu unahusiana na wetu kwa sababu amegusia maudhui ambalo ni swala tunaloshughulikia na ulitusaidia kuona jinsi maudhui katika fasihi ya watoto yanavyopaswa kusawiriwa. Hata hivyo, Tofauti na Karuga (keshatajwa) utafiti huu umesonga mbele na kuonesha jinsi maswala ya maudhui na fani yanavyohusiana na kujengana.

Gatere (2020) ameshughulikia usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya. Katika kazi hii amechanganua maudhui kwa kutazama aina za familia

zinazosawiriwa katika fasihi ya watoto, ametathmini usawiri wa familia kama taasisi katika fasihi ya watoto na pia amechunguza uhalisi wa familia unavyoakisiwa katika hadithi za watoto. Utafiti wa Getere (keshatajwa) unafanana na wetu kwa njia mbili. Kwanza, anashughulikia vitabu vilivyoandikwa nchini Kenya. Pili, ameangazia maudhui ya familia. Mawazo haya yalitusaidia kusuka maudhui ya familia. Kwa upande mwingine kuna tofauti kati ya kazi yake na yetu kwa sababu amechunguza vitabu tofauti na vile tulivyohakiki; amechunguza maudhui ya familia pekee na hajagusia vipengele vya fani ambavyo tumeshughulikia. Tumepiga hatua na kuonyesha vipengele vya fani vilivyochangia maudhui ya familia na maudhui mengine.

### 2.9 Uhusiano kati ya Vipengele vya Fani na Maudhui katika Fasihi

Fani na maudhui ni dhana mbili ambazo haziwezi kutenganishwa. Kuna mitazamo miwili ambayo inajaribu kuangazia uhusiano wa fani na maudhui katika kazi za fasihi andishi. Mitazamo hiyo ni ya kidhanifu na kiyakinifu. Katika mtazamo wa kidhanifu, Matteru (1983) anasema fani na maudhui ni kama mwili na nguo, hivyo anatoa maoni kuwa fani na maudhui ni dhana ambazo zinaweza kutenganishwa kama vile mwili unavyoweza kutenganishwa na nguo. Kwa hiyo, Matteru anasema maudhui ni mwili ambao ndilo umbo la ndani la kazi ya fasihi, nguo ikiwa fani ambayo ni umbo la nje la kazi ya fasihi. Kwa upande wao, Muhando na Balisidya (1976) wanasema kuwa fani na maudhui ni kama sahani na chakula. Sahani inaaweza kutengwa na chakula pale ambapo chakula hicho kitaondolewa. Hii inamaanisha kuwa chakula ndiyo maudhui yaani umbo la ndani la kazi ya fasihi na sahani ndiyo fani ambayo ni umbo la nje la kazi ya fasihi. Hivyo, yeye anaona kuwa fani na maudhui ni dhana mbili ambazo zinaweza kutenganishwa bila athari yoyote. Naye Sengo (1987) anasema kuwa fani na maudhui ni kama chungwa na ganda, akiwa na maana kuwa chungwa ndiyo maudhui na ganda ndilo fani. Hapa, Sengo anatoa msimamo kuwa fani na maudhui vinaweza kutenganishwa bila ya athari, kwani chungwa linaweza kutengwa na ganda lake.

Mtaalam mwingine anayeegemea mtazamo wa kidhanifu ni Nkwera (1978), anayesema kuwa fani na maudhui ni kama kikombe na chai ambapo chai ndiyo maudhui na fani ndiyo kikombe. Kwa kusema hivi, anamaanisha kuwa chai inaweza kunywewa kwenye kikombe na kikombe kubakia kitupu, hivyo fani yaweza kutengwa na maudhui kama vile chai inavyoweza kutengwa na kikombe (Njagi, 2002). Maelezo ya wataalamu hawa yalitusaidia katika utafiti wetu kwa kuunga mkono nadharia ya umuundo inayokubali kutenganisha vipengele katika dhana ili vichunguzwe kwa kina kwa madhumuni ya kueleweka. Kwa sababu hii, tulitenganisha uchambuzi wa fani na maudhui ili kuvichunguza. Kwanza, tulitenganisha fani kwa kudondoa na kuhakiki vipengele vyake kama tashbihi, misemo, nahau, methali, picha na taswira. Pili, tulitambua na kuchambua maudhui mbalimbali kama familia, elimu, nidhamu, ushawishi, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo. Hatimaye, tulionyesha namna fani tulizotambua zilivyofanikisha maudhui.

Katika mtazamo wa kiyakinifu, Senkoro (1984) anasema kuwa fani na maudhui ni sawa na sarafu. Hapa anamaanisha kuwa fani na maudhui ni dhana mbili zisizoweza kutenganishwa kama vile pande mbili za sarafu moja. Anasisitiza kuwa fani na maudhui havitenganishiki bali hutegemeana ili kazi ya fasihi iweze kuwa bora zaidi. Kazi ya fasihi ambayo maudhui yamezidi fani huwa chapwa au fani ikizidi maudhui, kazi hiyo ya fasihi huwa chapwa, hivyo maudhui na fani ni dhana ambazo hutegemeana. Fani na maudhui lazima vilingane na kushabihiana ili kazi yenyewe iweze kuwa bora na yenye mvuto zaidi.

Mtazamo mwingine unadai kuwa fani na maudhui hulinganishwa na roho na mwili ambapo viwili hivi haviwezi kutenganishwa kwani kwa kufanya hivyo athari itakayotokea ni kwamba mwili hautaweza kufanya kazi ipasavyo pasipo roho. Vilevile tunaweza kufananisha fani na maudhui kama gari na injini ambapo gari haliwezi kutenda bila injini.

Katika njia hii pia fani na maudhui ni dhana mbili zisizotenganishwa kwani huleta athari zinapotenganishwa na vilevile fani na maudhui hutenda kazi pamoja. Maoni haya yanashikiliwa pia na Wamitila (2003) anayesema kuwa aghalabu wahakiki hupenda kutofautisha kati ya fani na yaliyomo au maudhui. Anaendelea kusema kuwa fani ni mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui na kuwa dhana za maudhui na fani huchangiana na hatuwezi kuzitenganisha. Kwa hiyo, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na ufahamu mzuri wa lugha ambayo hutumiwa kuieleza, ni muhimu kueleza uhusiano uliopo kati ya lugha ya kifasihi na ujumbe wa mwandishi (Leech, 1969).

Ngugi (2018) ameshughulikia maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto kwa kuchanganua *Utenzi wa Haki za Watoto na Mashairi ya Bulbul*. Katika utafiti huu, Ngugi kwa kuongozwa na nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Kimtindo ameshughulikia maudhui yanayojitokeza katika ushairi wa watoto na akataja maudhui kama haki, mazingira, dawa za kulevya, teknolojia, maadili, adabu, bidii, wivu, elimu na maarifa. Baadhi ya maudhui haya kama vile bidii na elimu yamejitokeza katika kazi yetu. Hata hivyo, utafiti wetu kwa kuongozwa na nadharia Umuundo ulibaini maudhui zaidi kama familia, nidhamu, ushirikiano, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo. Katika madhumuni ya pili, Ngugi alishughulikia mbinu za kimtindo zilizotumiwa katika mashairi ya watoto na akabaini kuwa kuna matumizi ya mishororo mifupi, msamiati sahili, matumizi ya vielelezo na picha. Mbinu hizi zimejitokeza katika ushairi huku utafiti wetu unashughulikia riwaya za watoto. Katika madhumuni ya tatu, ameshughulikia umuhimu wa maudhui aliyotambua huku katika utafiti wetu tunashughulikia jinsi fani zinavyofanikisha maudhui hasa katika riwaya.

Oiko (2017) ametafiti uhakiki wa mtindo katika tamthilia za Arege na amebaini kuwa mtindo ni taji ya maudhui na kueleza kuwa vipengele hivi vinaumana na kuingiliana katika

kazi za mwandishi wa tamthilia Timothy Arege. Mtafiti huyu anasema kuwa ni vigumu kutenga mtindo na ujumbe, yaani kinachosemwa na namna kinavyosemwa. Ametambua mbinu kama usimulizi, kinaya, kejeli, usambamba, kuchanganya ndimi, mdokezo na balagha. Pia amebaini tamathali za usemi kama tashbihi, tashhisi, methali, tabaini, kwelikinzani, taswira, takriri na nahau. Kwa upande wa maudhui, ameshughulikia maudhui kama uongozi wa kiimla, ahadi za uwongo, ufisadi ukandamizaji, maendeleo, msiba wa kujitakia hauna kilio, ukoloni mkongwe, ukoloni mamboleo na muungano wa wanyonge ili kujikomboa na viongozi dhalimu.

Utafiti wa Oiko ni sawa na wetu kwa kuwa ameshughulikia vipengele vya fani na maudhui kwa pamoja kwa kuwa haviwezi kutenganishwa. Ameonesha jinsi mtindo unavyofanikisha maudhui. Hata hivyo, yeye ameshughulikia tamthilia za watu wazima lakini katika utafiti wetu tunashughulikia riwaya za watoto. Katika utafiti wake ameshughulikia mtindo na maudhui pamoja lakini katika utafiti huu tumeainisha vipengele vya fani kama tashbihi, misemo, nahau, methali, picha na taswira. Pia tumeeleza maudhui yaliyojitokeza kama familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo. Kisha tumeonyesha jinsi vipengele vya fani vilivofanikisha maudhui hayo.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, tulifikia maamuzi kuwa kuna uhusiano wa karibu sana kati ya maudhui na fani hivi kwamba kipengele kimoja hakiwezi kuchunguzwa bila kile kingine. Hata tulipotenganisha vipengele hivi viwili, ilikuwa ni lazima kimoja kichunguzwe katika muktadha wa kile kingine. Kwa hiyo, tulitenganisha fani na maudhui na kuvichunguza kwa undani. Hata hivyo, baadaye tulionyesha namna fani inavyofanikisha maudhui katika kazi ya fasihi ya watoto inayotumiwa katika kufundishia wanafunzi katika shule za msingi nchini Kenya.

## 2.10 Hitimisho

Katika sura hii tuliangazia uhakiki wa maandishi yanayohusiana na utafiti huu ambapo tuliangalia tafiti mbalimbali kuhusu fani hasa katika fasihi ya watoto. Pia tumechunguza watafiti mbalimbali ambao wameandika kuhusu maudhui katika fasihiya watoto. Tafiti hizi tulizochunguza zimeonyesha kuwa fasihi ya watoto ina maudhui na hutumia fani inayowalenga watoto. Aidha kuna tafiti chache zilizochunguza jinsi fani na maudhui vinahusiana. Hata hivyo, kazi hizo ni katika fasihi ya watu wazima. Uhakiki huu bila shaka umetusaidia kubainisha na kuweka wazi pengo ambalo utafiti huu ulinuia kuziba kwa kudhihirisha wazi kuwa kuna ufinyu wa tafiti kuhusu namna fani zinavyofanikisha maudhui katika fasihi ya watoto.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mbinu za utafiti kwa kuonyesha hatua tulizopitia katika utafiti. Tulionesha muundo wa utafiti tuliotumia, eneo la utafiti, idadi jumla, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo na kisha maswala ya maadili katika utafiti wetu.

## 3.1 Muundo na Mbinu ya Utafiti

Huu ni utafiti wa uchanganuzi matini na ulifanywa maktabani. Katika njia hii ya uchanganuzi matini mambo yanayohusika ni kusoma kwa undani vitabu, magazeti, matini, makala, tasnifu, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizomo maktabani na mtandaoni. Kwa kufanya hivi, mtafiti hupata habari za kina kupitia kusoma maandiko na kuangalia taarifa kutoka vyanzo mbalimbali (Kothari, 2013). Utafiti huu ulifanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Rongo, Chuo Kikuu cha Kenyatta na katika mtandao. Maktaba hizi zilitusaidia kupata mapitio mbalimbali katika vitabu, tasnifu, makala, magazeti na maandishi mbalimbali yaliyohusiana na mada yetu ya utafiti. Katika kupitia maandiko haya tuliweza kufahamu kilichosemwa na watafiti na wataalamu wengine kuhusu mada yetu na hivyo tukaweza kuchunguza, kuchanganua na kuhakiki vitabu vya fasihi ya watoto tulivyoteua kwa mujibu wa maswali na madhumuni ya utafiti.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Katika utafiti wa kisayansi kuna maeneo mawili ya kitafiti ambayo ni eneo la kijiografia na kitaaluma. Utafiti huu ulijikita katika eneo la kitaaluma ambalo ni la fasihi na ulifanywa maktabani kwa kusoma vitabu, majarida na tasnifu kuhusu fasihi ya watoto. Tulisoma vitabu tulivyokuwa tumechagua kwa undani ili kupata data tuliyohitaji. Vitabu hivyo vilikuwa *Sitaki Iwe Siri*, *Kisasi Hapana*, *Nimefufuka* na *Wema wa Mwana*.

### 3.3 Vifaa vya Utafiti

Katika utafiti huu kompyuta ilikuwa ni kifaa cha msingi. Tuliitumia katika kutafuta matini kutoka katika tovuti na wavuti. Pia ilitumiwa katika kunakili na kuhifadhi taarifa mbalimbali zilizohusiana na utafiti wetu. Mbali na kompyuta tulitumia kalamu na karatasi kunakili na kuchanganua data tuliyokusanya.

### 3.4 Idadi Lengwa

Idadi jumla ya utafiti wetu ilikuwa ni vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa katika kufundisha watoto walio katika shule za msingi nchini Kenya. Fasihi hii inajumuisha mashairi, tamthilia na hata riwaya. Idadi kamili ya vitabu hivi haijulikani kwa uhakika. Katika utafiti huu, tulichunguza riwaya nne pekee ambazo ni *Kisasi Hapana (2008), Nimefufuka (2011)*, *Sitaki Iwe Siri (2008)* na *Wema wa Mwana (2012).*

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni kitu au vitu kati ya vingi vya aina ileile vinavyochukuliwa kama mfano mzuri wa vitu hivyo kwa sababu si rahisi kutafiti kundi zima (TUKI, 2013; Brayman, 2004). Kulingana na Kothari (2013) na Marshall (2006), uteuzi wa sampuli ni mchakato wa kuamua idadi itakayoteuliwa kutoka kwa idadi jumla ili kufanyiwa utafiti. Katika sayansi ya jamii, sampuli huteuliwa ili kuokoa muda, gharama na nguvu kazi wakati wa kufanya utafiti. Kwa hivyo, katika utafiti huu, uteuzi wa sampuli ulikuwa ni zoezi muhimu kwa kuwa ilikuwa ni vigumu kutafiti vitabu vyote vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunzia fasihi katika shule za msingi nchini Kenya. Idadi ya vitabu vya fasihi ya watoto vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu Nchini Kenya ili kutumiwa katika shule za msingi ni 497 (ALSTBOIMPS, 2015).

Ili kupata data bora zaidi, tulitumia uteuzi sampuli kimakusudi. Kulingana na Kothari (keshatajwa) na Gall na wenziwe (1996) uteuzi sampuli kimakusudi ni mbinu inayomruhusu

mtafiti kutumia tajriba yake kuchagua sampuli anayohisi kuwa inafaa kujibu maswali ya utafiti. Kwa kuongozwa na maoni haya, tuliteua riwaya zinazotumiwa kufundishia fasihi katika shule za msingi nchini Kenya na ambazo zimewahi kushinda tuzo za Jommo Kenyatta. Hizi ni tuzo maarufu zaidi nchini Kenya kwa kuwa zilianzishwa 1974 na hushindaniwa na waandishi wengi zaidi. Vitabu vilivyowahi kushinda tuzo hii tangu zianzishwe ni 11. Katika mwaka wa 2003, *Ndoto ya Amerika* kilichoandikwa na Ken Walibora ndicho kilichoshinda, mwaka wa 2005, *Kofia ya Kadogo* cha Ruth Wairimu na katika mwaka wa 2007 kitabu cha Nyambura Mpesha *Hanna na Wairimu* ndicho kilichoshinda. Katika mwaka wa 2009, kitabu kilichoshinda nafasi ya kwanza kilikuwa ni *Kisasi Hapan*a cha Ken Walibora, nafasi ya pili kilikuwa ni *Sitaki Iwe Siri* cha Bifungu Matandura. Katika mwaka wa 2011, nafasi ya kwanza ilichukuliwa na *Wema wa Mwana* chake Nuhu Z Bakari, nafasi ya pili ilichukuliwa na kitabu *Msichana Aliyeokoa Watu* chake Enan Mwakoti na ya tatu ilitwaliwa na *Sungura na Mbwa* kilichoandikwa na Florence Nyakari. Hatimaye katika mwaka wa 2013, kitabu *Nimefufuka* kilichoandikwa na Rebecca Nandwa kilishinda tuzo. Kwa kuongozwa na vigezo hivi, tuliteua riwaya nne za *Kisasi Hapana* (2008) kilichoandikwa na Ken Walibora, *Nimefufuka* (2011) kilichoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* (2008) kilichoandikwa na Bitugi Matundura na *Wema wa Mwana* (2012) kilichoandikwa na Nuhu Bakari.

Gall na wenziwe (wameshatajwa) wanashikilia kuwa mbinu hii ya uteuzi wa kimakusudi humwezesha mtafiti kupata data inayohitajika hasa katika utafiti wa kithamano. Mbinu hii ilitufaa kwa sababu ilitusaidia kupata sampuli bora, iliyotupatia data ya kutosha na iliyofaa utafiti wetu. Wazo hili linakubaliana na maoni ya Neuman (keshatajwa) anayesema kuwa mbinu hii humpa mtafiti uhuru katika kuteua sampuli inayomwezesha kujibu maswali ya utafiti.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulihusisha usomaji wa kina wa machapisho mbalimbali. Kothari (2013) anasema kuwa ukusanyaji data unajumuisha kusoma, kuangalia taarifa, uchambuzi wa maandiko na kuangalia maarifa kutoka vyanzo mbalimbali kama vile vitabu, magazeti, makala, hotuba, picha, matangazo na matini. Uchambuzi huu hufanywa kwa ajili ya kuangalia ujumbe muhimu uliomo kwenye matini husika.

Tulikusanya data kwa hatua kadha kama ifuatavyo: kwanza, tulisoma vitabu kwa mara ya kwanza ili kuelewa hadithi. Hatua ya pili tulisoma tena na kutambua data iliyooana na madhumuni ya kwanza kwa kudondoa vipengele vya fani: nahau, methali, jazanda, picha, taswira na tashbihi. Hatua ya tatu ilikuwa ni kusoma tena huku tukidondoa data iliyohusiana na madhumuni ya pili ambapo tulitambua mawazo makuu yaliyojenga maudhui. Mawazo haya makuu tuliyachukulia kuwa maudhui makuu na mawazo madogo kuwa maudhui madogo. Data hii tuliinakili kwenye daftari la nyanjani ili itufae katika uchanganuzi.

Katika hatua ya nne tulitathmini jinsi vipengele vya fani: nahau, methali, jazanda, picha, taswira na tashbihi vilivyotumiwa katika kueleza maudhui katika vitabu tafitiwa ili kuonyesha nafasi ya fani katika kufanikisha maudhui katika fasihi ya watoto inayotumiwa kufundishia katika shule za msingi nchini Kenya.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Kulingana na Kothari (2013), uchanganuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupanga data zilizokusanywa vizuri kwa njia ambayo inamsaidia mtafiti kujibu maswali ya utafiti. Kwa kuchochewa na maoni haya, tulichanganua data kupitia hatua sita Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuorodhesha vipengele vya fani vyote tulivyopata kulingana na utokeaji wake na idadi kutoka kwa kila kitabu. Hatua ya pili, tuliorodhesha katika jedwali maudhui yote tuliyopata katika vitabu hivyo. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuchuja data tuliyopata kwa

kuchagua vipengele vya fani tulivyokuwa tumeamua kuchunguza. Vipengele hivyo ni tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Katika hatua ya nne tulichuja maudhui tuliyopata kuwa yanaoana na yanahusiana na lengo kuu la utafiti huu, maswali ya utafiti na madhumuni ya utafiti.

Hatua ya tano ilikuwa ni kuchanganua maudhui na vipengele vya fani kwa kina ili kuonyesha waziwazi jinsi kila kipengele cha fani tulichokuwa tumetambua kilivyokuwa kinasaidia kufanikisha maudhui mahususi tuliyokuwa tumetambua katika vitabu hivyo. Tulitoa ufafanuzi kuhusu jinsi vipengele hivyo vya fani vilivyofanikisha hayo maudhui kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Umuundo na malengo ya utafiti.

Katika hatua ya sita, tuliainisha maudhui na vipengele vya fani vilivyojitokeza kwa wingi na tukaonesha ruwaza mpya na mielekeo mipya katika uhusiano wa vipengele vya fani na maudhui kisha tukafafanua ruwaza hizo kulingana na madhumuni na maswali ya utafiti yaliyoongoza utafiti huu. Mugenda na Mugenda (1999) wanasema kuwa katika utafiti wa kithamano, data huweza kuwa matini au picha ambazo hueleza matukio. Wanaendelea kusema kuwa mara nyingi katika utafiti, ukusanyaji na uchanganuzi wa data hufanywa kwa mwambatano wa moja kwa moja. Kwa kuwa vitabu vya watoto vina picha tulizichanganua moja kwa moja bila kwanza kuzichora mahali fulani. Hata hivyo, tumeweka picha kadhaa kama vielelezo.

Tuliyachanganua maudhui katika vitabu hivi kwa kutazama namna yalivyokuwa yanaendana na vipengele vya fani vilivyotumiwa na waandishi wa vitabu hivyo. Tulitoa maelezo kuhusu ni vipi vipengele hivyo mbalimbali vya lugha kama nahau, methali, tashbihi, taswira na picha hushirikiana ili kuendeleza maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunzia fasihi katika shule za msingi nchini Kenya.

Tuliwasilisha data ya mwisho kithamano kwa kuzingatia maoni ya Truex (1996) ambaye anaeleza kuwa uchanganuzi matini kithamano humpa mtafiti nafasi ya kuhakiki kwa makini vipengele vya uumbaji wa sanaa na maana inayojitokeza katika vipengele vya sanaa hiyo. Katika muktadha huu, vipengele vya uumbaji wa sanaa ni fani huku maana inayojitokeza ikiwa ni maudhui. Kwa hiyo, tulionesha jinsi fani inavyofanikisha maudhui katika vitabu hivyo. Hatimaye tukawasilisha matokeo ya utafiti kinathari.

### 3.8 Maswala ya Maadili katika Utafiti

Mukuthuria (2009) anaeleza kuwa maadili katika utafiti ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote tunaotangamana nao katika utafiti, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Kwa kuwa huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani, hatukuhitaji kukusanya data kutoka nyanjani. Hata hivyo, tulihakikisha kuwa wataalamu na waandishi tuliowanukuu katika kazi yetu wametambuliwa na kazi zao kuoneshwa katika marejeleo. Tulihakikisha kuwa data tuliyokusanya ni sahihi, kwa kuinakili kwa usahihi na kuihifadhi vizuri na ikatufaa katika utafiti. Kabla ya kuanza utafiti tulijitahidi kupata kibali kutoka kwa Chuo Kikuu cha Rongo na pia Baraza la Kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (NACOSTI). Kwa kufanya haya yote, tulikuwa tunatimiza maadili ya utafiti.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza njia na mbinu za utafiti kwa kuonyesha muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa, uteuzi wa sampuli yetu, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo na hatimaye tukaonyesha maswala ya maadili katika utafiti wetu.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Kwanza, tumetanguliza kwa kutambua na kueleza maana ya kila kipengele kati ya vipengele hivyo vya fani ambavyo ni tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Kisha, tulitambua vipengele hivyo vya fani kama vilivyotumiwa katika riwaya za fasihi ya watoto tulizotafiti kisha tukaviorodhesha katika majedwali na kuonesha idadi iliyotumiwa na kila mwandishi wa riwaya  tulizotafiti. Hatimaye, tulihakiki fani hizo kwa kuonesha mazingira zinamotumika na ruwaza mpya tulizotambua. Katika hatua ya pili, tulitambua maudhui makuu na madogo yaliyojitokeza, tukayaorodhesha na kuyajadili. Maudhui tuliyotambua ni ya familia, elimu, nidhamu, ushawishi, ugonjwa na kifo, bidii, ushirikiano na nafasi ya mwanamke.

Hatimaye, katika hatua ya tatu tumejadili kwa kina jinsi vipengele mbalimbali vya fani tulivyatambua kama tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha vilivyosaidia katika kuendeleza maudhui ya familia, elimu, nidhamu, ushawishi, ugonjwa na kifo, bidii, ushirikiano na nafasi ya mwanamke.

## 4.1 Vipengele vya Fani katika Fasihi ya Watoto

Tuliona katika 1.8 kuwa Nadharia ya Umuundo husisitiza jinsi vipengele vya kazi ya sanaa vinavyohusiana na kufungamana hadi kuikamilisha kazi hiyo. Inazidi kushikilia kuwa sehemu hizo mbalimbali huweza kutenganishwa na kuchunguzwa na kuwa kazi yenyewe ilivyoundwa ndiyo hutoa maana. Yaani, maana inavyoumbwa ina dhima kubwa kuliko maana yenyewe. Tulitumia mhimili huu kuchunguza madhumuni ya kwanza kwa kuainisha vipengele mbalimbali vya fani katika kazi tulizochunguza. Tulichukulia kuwa kila kipengele cha fani tulichokuwa tunahakiki ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii. Kwa kuongozwa na mawazo haya, utafiti huu uliweza kutambua vipengele

mbalimbali vya fani vilivyotumiwa katika fasihi ya watoto. Miongoni mwa vipengele vilivyogunduliwa ni tashbihi, taswira, methali, misemo, nahau na picha. Vipengele hivi vilichunguzwa na kuchanganuliwa ili kuona mfanano na tofauti zilizopo katika matumizi yavyo katika riwaya hizo nne. Hatimaye tukaonesha jinsi vipengele hivyo mbalimbali vya fani vimetumiwa kuendeleza maudhui tofautitofauti katika riwaya hizi.

### 4.1.1 Tashbihi

Tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulinganishwa kwa njia waziwazi. Tashbihi hutambulishwa na matumizi ya viungio kama, mfano wa, sawa na, mithili ya, ja, kama vile, kama kwamba na kadhalika (Wamitila, 2003; Senkoro, 2011). Msokile (1992) na Wamitila (2011) wanaongezea kuwa tashibihi pia huweza kuelezwa kuwa ulinganisho wa moja kwa moja na ulinganisho huo unadhamiriwa kusisitiza sifa fulani akilini na kuwa mtunzi hutumia ulinganisho huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumu zaidi. Wataalamu hawa wote wanaafikiana kuwa tashbihi hulinganisha watu au vitu kwa kutumia vilinganishi kwa nia ya kusisitiza sifa fulani na kujenga picha akilini mwa msomaji.

Katika sehemu hii, tumetambua tashbihi katika riwaya zote nne na kuorodhesha idadi iliyopatikana katika kila riwaya katika Jedwali 4.1. Uchanganuzi wetu ulihusu kuonesha idadi ya tashbihi katika kila riwaya, tashbihi zilizojitokeza kwa wingi, miundo yake na matumizi yake katika riwaya tofautitofauti.

**Jedwali 4.1:** ***Tashbihi katika Riwaya za Watoto***

| Riwaya | Idadi ya Tashbihi |
|---|---|
| *Wema wa Mwana* | 8 |
| *Kisasi Hapana* | 24 |
| *Nimefufuka* | 9 |
| *Sitaki Iwe Siri* | 42 |
| **Jumla** | **83** |

Kutokana na jedwali 4.1, imebainika kuwa kwa ujumla, tashbihi tulizotambua katika riwaya hizi ni 83, ambapo *Sitaki Iwe Siri* inaongoza kwa idadi ikiwa na 42, *Kisasi Hapana* inafuata kwa tashbihi 24, *Nimefufuka* tashbihi 9 na kisha *Wema wa Mwana* ikiwa na 8. Hii ndiyo fani iliyotumiwa kwa wingi zaidi katika kazi tulizochunguza. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia tashbihi kwa wingi kuliko waandishi hawa wengine kwani ametumia zaidi ya nusu ya tashbihi hizi zote, akifuatiwa na mwandishi wa *Kisasi Hapana* ambaye ametumia tashbihi 24. Waandishi wa *Nimefufuka* na *Wema wa Mwana* wana tashbihi chache ikilinganishwa na hao wengine.

Kwa kuwa "kama" ni kipengele muhimu cha uhakiki katika tashbihi, imebainika kuwa waandishi hawa wote wamekitumia katika kuendeleza tashbihi zao. Hata hivyo, katika *Wema wa Mwana*, "mithili ya" imetumiwa mara moja. Waandishi wa *Kisasi Hapana* na *Nimefufuka* hawajatumia "mithili ya" hata mara moja. Mwandishi wa Sitaki *Iwe Siri* ametumia mithili ya mara 4. Riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* ni ndefu kuliko riwaya hizi nyingine na imetumia pia tashbihi kwa wingi kuliko riwaya hizo nyingine tatu. Tashbihi "kutunza kama mboni ya jicho" imetumiwa na watunzi wawili kwa njia sawa yaani *Sitaki Iwe Siri* katika ukurasa wa 10 na *Kisasi Hapana* katika ukurasa wa 2. Pia tashbihi "mzito kama

nanga" imetumiwa kwa njia sawa katika *Nimefufuka* ambapo imetumiwa kurejela shida ya kumtunza Jose huku katika *Sitaki Iwe Siri* ikitumiwa kurejelea mzigo wa kuandika insha ambayo ilionekana kuwa kazi ngumu kwa Musa.

Kipengele kingine kilichotumiwa katika uhakiki wa tashbihi ni kile kinachohusu sehemu za mwili kama mboni ya jicho, mikono, nywele, mgongo, meno, mitulinga na kadhalika. Katika *Sitaki Iwe Siri,* mwandishi Bitugi Matundura ametumia tashbihi kama:

i. Hujachana nywele Aisee! Zinaonekana kama za mwendawazimu (Uk. 3)
ii. Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji (Uk. 7)
iii. Mgongo wake ulikuwa umepinda kama uta…(Uk. 7)
iv. Aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho (Uk. 10)
v. Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa. (Uk. 22)
vi. Alifurahi kama kibogoyo aliyetunukiwa jino ombi lake lilipokubaliwa. (Uk. 27)
vii. Mwenye macho makali yaliyopenya kama miale ya jua. (Uk. 36).

Katika tashbihi mbili zinazohusu nywele za Musa na Nyanya Mwalongo: "Hujachana nywele zinaonekana kama za mwendawazimu" na "Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji" (Uk. 3, 7) dhana inayojitokeza ni kuwa mwendawazimu huwa hana kichana na ni muhali kwake kwenda kwa kinyozi kunyolewa na hivyo nywele zake huwa hazina mpangilio na ndivyo nywele za Musa na Mwalongo zinavyoonekana.

Katika *Wema wa Mwana,* mwandishi ametumia tashbihi inayosema: "Macho yalilegea kama ndulele", "Mwili ulilegea kama aliyezaliwa jana" na "alianza kutetemeka kama kuti la mnazi" (Uk. 11). Tashbihi hizi zinarejelea mwitiko wa Juma baada ya kugunduliwa na babake kuwa ameiba vipande vya nyama na kuviweka mfukoni. Macho kulegea ni kumaanisha kuwa ana haya kutokana na kitendo hicho. Mwili unatetemeka kwa sababu ya woga wa kugunduliwa. Kwa njia hii tunapata taswira kamili kutuonesha kuwa Juma anajuta kwa kitendo hiki cha kuiba nyama na kuitia mfukoni mwake.

Tashbihi zinazohusu wanyama na viumbe wengine ni kipengele kingine muhimu kilichotambuliwa katika utafiti huu. Viumbe na wanyama kama tausi, nyuki, nzi, malaika, kuku, siafu, chiriku, chura na ninga wametumiwa katika tashbihi hizi. Mifano iliyotumiwa na Bitugi Matundura katika *Sitaki Iwe Siri* ni:

i. Milio ya jogoo ambao sasa walikuwa wanawika kwa majibizano kama washairi…(Uk. 1)
ii. Walikuwa wamekwamilia blanketi kama siafu wanaokwamilia nyama (Uk. 2)
iii. Je! Mbona wajukuu hawa wana maswali mengi kama ya chiriku? (Uk. 5)
iv. Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia. (Uk. 14)
v. Muda una mbawa kama ndege. (Uk. 22)
vi. Wanafunzi walikuwa wamekusanyika huku wakipiga kelele kama bumba la nzi. (Uk. 25)
vii. Utingo naye alikazana kama siafu kukusanya nauli kutoka kwa abiria. (Uk. 28)
viii. Kituo cha biashara cha Mwembe Tayari kilikuwa na shughuli nyingi kama za nyuki mzingani. (Uk. 28)
ix. Kulikuwa na kimya cha kaburi kama shetani alikuwa anapita. (Uk . 37)
x. Chumba kidogo cha takriban mita kumi na sita mraba mithili ya kuku aliyetoka kutaga yai. (Uk. 47).

Tashbihi katika *Sitaki Iwe Siri* katika ukurasa wa 2 inasema "alitandika kitanda chake haraka kama umeme" inatoa dhana kuwa umeme unajulikana kufanya kazi haraka na hivyo Musa inaonekana alitandika kitanda kwa haraka isiyo ya kawaida. Dada za Juma kwa upande mwingine walikwamilia blanketi kama siafu kumaanisha ilikuwa blanketi moja na walihitaji kung'ang'ania jinsi siafu hung'ang'ania chakula. Katika *Nimefufuka* mwandishi Ken Walibora ametumia tashbihi zinazohusu viumbe kama:

i. Lena alikuwa mrembo kama malaika. (Uk 2)
ii. Lena alikuwa mwingi wa maringo kama tausi. (Uk. 2).

Tashbihi hizi zimetumiwa kurejelea msichana Lena ambaye ana sura nzuri kwelikweli na uzuri wake unamsukuma kuwa na maringo. Tausi anajulikana kuwa ndege mwenye sura nzuri na maringo makubwa. Malaika nao ni viumbe wanaoaminiwa kuwa wasio na dosari na hivyo kuwa mfano mzuri wa kulinganishwa na mwanamke mrembo. Kujisemea kama mwenye mahoka ni tashbihi inayomrejelea mama ya Lena ambaye anazungumza kama

kichaa au anajisemea mwenyewe kwa kulemewa na mawazo ya kupotea kwa binti yake Lena ambaye amejiingiza katika anasa.

Kipengele kingine kilichojitokeza katika uhakiki wa tashbihi ni kile kinachohusu vifaa kama mshale, mlingoti, chungu, nanga, msalaba na gari. Kwa mfano, tashbihi "kufyatuka kama mshale" imetumiwa na Nuhu Bakari katika *Wema wa Mwana* na Bitugi Matundura katika *Sitaki Iwe Siri* kwa njia sawa kuashiria kukimbia. Tashbihi inayohusu mlingoti imetumiwa katika *Wema wa Mwana* kuhusu kunyooka kwa tabia huku katika *Kisasi Hapana* ikihusu kunyooka kwa miti ya stima. Tashbihi kuhusu gari imetumiwa mara kadha na waandishi wawili na zinahusu kuendeshwa kwa haraka na kukwama na hili linafaa kwa sababu watoto hupenda sana magari. Mwandishi wa *Wema wa Mwana* Nuhu Bakari ametumia tashbihi isemayo:

> "Mfuko wa suruali yake ulikuwa unatoa mvuke kama mtu aliyebeba chungu kinachotokota mfukoni". (Uk. 7).

Tashbihi hii inamrejelea Juma baada ya kuiba nyama kutoka katika chungu kilichokuwa mekoni. Kwa kutumia tashbihi hii, mwandishi huyu anatuchorea picha kwa njia ya chuku kuwa nyama ile inaendelea kutoa mvuke ikiwa mfukoni mwa Juma kama ambavyo ingekuwa inaendelea kupikwa mekoni na hivyo kumchoma Juma vibaya. Mfano mwingine wa kipengele kinachohusu kifaa ni tashbihi inayosema "atanyooka kama mlingoti" ambayo inamrejelea Ngoyoni ambaye babake anahisi kuwa akitoka katika shule ya kurekebishia tabia atakuwa na tabia njema. Tabia hii njema ndiyo inayorejelewa kuwa inanyooka kama mlingoti. Katika maisha ya kawaida tunajua milingoti ni miti inayotokana na mikonge na huwa imenyooka kwelikweli. Kwa hiyo tashbihi hii inatuchorea uwezekano kuwa Ngoyoni atakuwa amenyooka kimaadili baada ya kutoka katika shule ya kurekebishia tabia.

Katika *Wema wa Mwana* kuna tashbihi nyingine inayosema:

“Alifyatuka mithili ya mshale”. (Uk 16).

Tashbihi hii inarejelea kufyatuka kwa mama ya Ngoyoni akikimbia kwenda kumlaki mwanaye akitoka shuleni baada ya kuwa mbali naye kwa muda fulani. Katika *Wema wa Mwana* pia kuna tashbihi inayohusu gari: “Pote hapo ni pahali ambapo maisha ya watu yanaendeshwa kama gari na watu wengine” na “Dereva wa mkuu wa wilaya kaendesha gari kama vile walimu wanavyotuendesha sisi wanafunzi shuleni” (Uk.13). Gari limetumiwa kuonesha kuwa halina hiari na anayeliendesha ndiye anayeamua litakapotoka, litakapoelekea na litakaposimama. Hivyo ndivyo watu wanavyoendeshwa na viongozi na pia walimu kwa wanafunzi wao. Wanafunzi hao huwa wanatenda mambo kwa sababu wameambiwa tu, hawana hiari yoyote kama gari linapoendeshwa huwa halina hiari nalo huenda apendapo dereva. Pia matumizi ya gari katika tashbihi hii ni jambo la busara kwa sababu watoto hasa vijana hupenda magari nao hupenda kujinasibisha na magari na madereva. Mfano kama huu ni rahisi kwa watoto kuelewa na kukumbuka.

Tashbihi nyingine inasema: “Jose ni msalaba mzito kama nanga” (uk. 13). Tashbihi hii inaonesha kuwa kumtunza Jose ni jambo la kulazimishiwa kwani ni mtu mzima anayefaa kujitunza mwenyewe, hata hivyo hajiwezi kutokana na uraibu wake wa vileo. Nanga ni chuma nzito inayozuia meli kupeperushwa na upepo na hubebwa kwa kulazimishwa kwa sababu itasaidia tu wakati wa kusimamisha meli, vinginevyo manahodha wangeiacha ili kupunguza mzigo unaobebwa na meli husika. Kwa njia hiyohiyo kumtunza Jose kunamnyima Sikitu nafasi ya kufanya mambo yake. Ni mzigo wa kulazimishiwa ambao kama ingekuwa hiari yake angeudondosha.

Mapenzi ni kipengele kingine kilichotumiwa katika kuhakiki tashbihi. Katika *Kisasi Hapana* mwandishi *Ken Walibora* ametumia tashbihi zinazohusu mapenzi yaliyo kati ya washiriki wa familia. Tashbihi hizo ni:

i. "Humwona kama, sijui niseme, mtoto mdogo au aliyefiwa." (Uk. 1).
ii. "Naye alinipenda kama mboni ya jicho." (Uk. 2)

Tashbihi ya kwanza "Humwona kama, sijui niseme, mtoto mdogo au aliyefiwa" inarejelea mama ya Kido ambaye analia kila siku kwa kumkosa mume wake mzee Mkulu ambaye amefungwa huku ya pili ikirejelea mapenzi ya nyanya ya Kido kwa mjukuu wake. Kwa kawaida, si rahisi kuguza mboni ya jicho kwa sababu inalindwa kutokana na madhara yoyote. Kwa hiyo, huu ni mfano mzuri wa ulinzi unaotokana na mapenzi ya nyanya kwa mjukuu wake.

Tashbihi nyingine inayohusu mapenzi ni:

> "Alitamba huku anaimba beti za mashairi na kuimba nyimbo kwa sauti nzuri kama ya ninga" na "Hadithi zake zilikuwa tamu kama chakula chake" (Uk. 3).

Tashbihi hizi zinarejelea hadithi ambazo nyanya ya Kido alikuwa akimtambia. Chakula ni muhimu na kinapendwa na watu wote na hivyo nyimbo kulinganishwa na chakula inamaanisha hadithi hizi zilimpendeza sana mhusika huyu mwenye umri mdogo ambaye kwa kawaida chakula ni kila kitu. Tashbihi nyingine aliyotumia mwandishi inahusu ukosefu wa mapenzi kutoka kwa baba ya Kido na inasema:

> "Mambo ambayo yanafanya tuone umetutupa kama maganda ya miwa" (Uk. 13).

Tashbihi hii imetumiwa kumaanisha kuwa baba ya Kido alikuwa amekosa kuja nyumbani kwa muda na ni kama amewatupa na hawana faida yoyote kwake. Ganda la miwa huwa halina maana kwa mlaji baada ya kupata yale majimaji matamu kwenye muwa wenyewe, hutupwa na hukanyagwa tu na ndivyo Kido anavyohisi baada ya kupuuzwa na babake. Kwa njia hii anahisi kuwa hathaminiwi kamwe. Katika *Nimefufuka*, tashbihi nyingine inayohusu mapenzi ni: "Kuzikwa kama mnyama asiyekuwa na wa kwao" (Uk. 8). Inarejelea Lena ambaye kulikuwa na mpango wa kumzika Mwambao kwa kukosa pesa za kuleta mwili wake nyumbani. Wanyama wafapo hakuna ambaye huwatafutia watu wao wa ukoo au hata

kwao ili wakazikwe huko na ndivyo ilivyokuwa inaelekea kufanyika kwa Lena baada ya wazazi wake kushindwa kupata pesa za kumleta nyumbani ili azikwe. Mapenzi yanahusika ambapo majirani wanaamua kuchanga pesa ya kumleta mwanao nyumbani katika ufu.

Kuna tashbihi kuhusu elimu. Nazo ni:

i. Kwake yeye kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala. (Uk 17).
ii. Ningependa shule kama ninavyopenda peremende na nyama ya kuku, na vinginevyo kwangu mimi shule ni kama dawa chungu ambayo mtu analazimishwa kumeza (Uk. 17).

Tashbihi hizi zimetumiwa kueleza jinsi watoto wanavyoona elimu hasa kati ya Kido na dadake. Kufumba macho hakuhitaji nguvu yoyote kwa hivyo dada ya Kido alikuwa mwerevu tu hata hakuhitaji kusoma sana ili kupita mtihani. Kido yeye analazimishiwa shule kama vile mtu hulazimika kumeza dawa chungu kwa kuwa ni mgonjwa vinginevyo angeiepuka.

Katika uchanganuzi wa tashbihi pia tulipata zile zinazohusu ugonjwa na kifo. Tashbihi hizi ni kama: “Mgongo wake ulikuwa umepinda kama uta”, “wakakonda kama ng’onda”, “akiwa ameganda kama kigaga pale nje na kuyakazia macho makaburi”, “kuepukwa kama mgonjwa wa ukoma”, “mitulinga ilikuwa inaonekana huku mwili wake mzima ukinyong’onyea kama mkufu kwa sababu ya kuishiwa na nguvu” (Uk. 7). Tashbihi hizi zimetumiwa kuonyesha hali ya uzee na ugonjwa wa nyanya Mwalongo na Yuri mhusika katika hadithi ya kubuni aliyotunga Musa.

Kipengele kingine ni tashbihi zinazohusu watoto wakiwa katika mazingira tofautitofauti. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia tashbihi zinazohusu watoto kama:

i. “Mbona wajukuu hawa wana maswali mengi kama ya chiriku” (Uk. 13).
ii. “Aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho” (Uk. 10).
iii. “Walikuwa wamebeba mikoba ya vitabu vyao kama watalii” (Uk. 12).
iv. “Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia” (Uk. 14).
v. “Wanafunzi walikuwa wamekusanyika huku wakipiga kelele kama bumba la nzi” (Uk. 25).

Tashbihi hizi ni za moja kwa moja kwani zinagusia mazingira ya watoto hasa wakiwa nyumbani na shuleni na zinawasilisha ujumbe kwa urahisi kuhusu masuala yanayowahusu watoto. Kwa njia hii zinaweza kuwa rahisi kueleweka hasa kwa hadhira ya watoto ambao wanalengwa na kazi hii.

Katika utafiti huu pia ilibainika kuwa kuna tashbihi zinazohusu bidii kama:

i. Kituo cha biashara cha Mwembe Tayari kilikuwa na shughuli nyingi kama za nyuki mzingani (Uk. 28).
ii. Utingo naye alikazana kama siafu kukusanya nauli kutoka kwa abiria, huku akigonga gari kwa mkono wake ulioonekana kukauka kama kibanzi cha ukuni (Uk. 31).
iii. Na magari hayo yaliingia kwa kasi kama umeme kupitia lango kuu la hospitali (Uk. 31).

Tashbihi inayohusu nyuki inatuonyesha kuwa ingawa nyuki ni wadudu wadogo, huwa wanavamia kazi yao kwa pamoja na hakuna ambaye huonekana kuzembea kazini. Magari ya kusafirisha wagonjwa huenda kwa haraka ili kunusuru maisha ya wagonjwa na hivyo ni sawa kulinganisha mwendo wa magari haya na umeme.

Imebainika katika utafiti huu kuwa kazi hizi zilizotungiwa watoto zimetumia tashbihi kwa kiwango kikubwa kwani kuna jumla ya tashbihi 83 ambazo zimetumiwa na waandishi wanne. Tashbihi hizi pia ni rahisi na zinaweza kueleweka na watoto. Katika *Wema wa Mwana* kuna tashbihi nyepesi kama “alianza kutetemeka kama kuti la mnazi”, “alinyooka kama mlingoti”, na “mwili ulilegea kama aliyezaliwa jana.” Tashbihi hizi zilizotumiwa kueleza mwonekano wa Juma baada ya kugunduliwa kuwa kaiba nyama kutoka jikoni si ngumu kwa mtoto kuzielewa na hazihitaji kufikiria mno. Katika *Kisasi Hapana* kuna tashbihi kama “Nyanya alinipenda kama mboni ya jicho lake na hadithi za nyanya zilikuwa tamu kama chakula chake.” Tashbihi hizi zinatoa picha ya hali husika kwa urahisi katika akili ya walengwa. Katika *Nimefufuka* mwandishi wake anatumia tashbihi kama “Lena alikuwa mrembo kama malaika” na “Lena alikuwa mwingi wa maringo kama tausi.” Ni rahisi kwa tashbihi hizi kueleweka na watoto kwani zinachota vilinganisho kutokana na

mazingira halisi anayokumbana nayo mtoto kila siku. Hatimaye katika *Sitaki Iwe Siri* kuna tashbihi kama “alitandika kitanda chake haraka kama umeme” na “mgongo wake (Mwalongo) ulikuwa umepinda kama uta.” Hizi tashbihi zinazotoa picha ya Musa na nyanyake zinaweza kuwa rahisi kwa mtoto kuelewa. Mbali na uwezekano wa kueleweka kwa urahisi, tashbihi hizi pia zinaweza kufanya mtoto kupata funzo mara moja na kumsaidia katika kumbukumbu.

### 4.1.2 Taswira

Taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Kulingana na Wamitila (2003), taswira ni dhana inayotumiwa kuelezea neno, kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji. Pia, Wamitila (2011) anasema kuwa taswira ni picha ambazo humjia msomaji akilini anapoisoma kazi fulani ya fasihi na picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazotumia. Sababu ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana na pia kutoa msisitizo fulani. Msanii hutumia maelezo ambayo huweza kufanya hadhira ipate aina tofautitofauti za hisi kama hisi za kunusa, kusikia, kuona, kuonja, na hata kugusa. Matokeo ya mbinu hii ni kugusa hisia za msomaji na kumfanya azame katika usomaji. Katika utafiti huu, imebainika kuwa ni vigumu kuhesabu idadi kamili ya taswira kwa sababu maelezo yoyote yale hujenga picha fulani akilini mwa msomaji na maelezo fulani huweza kutokeza taswira tofauti kwa wasomaji tofauti kwa kutegemea tajriba yao maishani. Katika sehemu hii tumedondoa taswira kuu tulizohisi zinakidhi mahitaji ya utafiti huu kisha tulijadili taswira hizo kwa misingi ya idadi yake katika kila kazi na hisi zinazojengwa na taswira hizo kama vile hisi za kunusa, kusikia, kuona, kuonja, na hata kugusa (Wamitila, keshatajwa). Baadaye katika 4.3 tumeonyesha jinsi taswira hizi zinavyochangia kufanikisha maudhui katika kazi zenyewe. Taswira tulizopata kitakwimu ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 4.2:** ***Taswira katika Riwaya za Watoto***

| **Riwaya** | **Idadi ya Taswira** |
|---|---|
| *Wema wa Mwana* | 6 |
| *Kisasi Hapana* | 11 |
| *Nimefufuka* | 9 |
| *Sitaki Iwe Siri* | 10 |
| **Jumla** | **36** |

Ingawa kuna taswira nyingi, katika utafiti huu tumeainisha na kuchanganua taswira 36. Kati ya hizi 36, mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia taswira nyingi zaidi zikiwa 11, zikifuatiwa kwa wingi na *Sitaki Iwe Siri* zikiwa 10 na katika *Nimefufuka* tulidondoa taswira 9. Hatimaye katika *Wema wa Mwana* tulipata taswira 6. Ingawa kuna uwezekano wa kutambua taswira nyingi zaidi, hizi ni zile taswira zilizojitokeza kwa uwazi zaidi. Ilibainika kuwa taswira zilizojitokeza ni zinazohusu uoni, kusikia na kuhisi. Hata hivyo ni wazi kuwa waandishi wote wamebobea sana katika taswira ya uoni.

Mojawapo ya vipengele muhimu katika uchanganuzi wa taswira ni uoni. Taswira hizi za uoni zinachora picha za mazingira mbalimbali. Nuhu Bakari Katika *Wema wa Mwana* anatuchorea taswira ya uoni ya namna Juma anavyotetemeka kama matawi ya mnazi anapoitwa na babake akiwa na nyama moto mfukoni. Juma alikuwa amekimbia kutoka jikoni babake anapomwona akiwa sebuleni na kumwita. Taswira nyingine ya uoni ni ile ya furaha ya Ngoyoni alipoenda kuchukuliwa na babake kutoka shuleni akiandamana na baba Juma baada ya shule kufungwa. Ngoyoni mwenyewe anaelezwa kuwa anamkimbilia babake wakiwa na baba Juma baada ya kukaa mbali naye kwa muda akiwa shule ya bweni. Baada ya Ngoyoni na mzazi wake kufika nyumbani kuna taswira nyingine ya uoni inayohusu furaha ambapo tunaelezwa kuwa nyumba ya akina Ngoyoni imejaa furaha kwa

kurudi kwa mwanao Ngoyoni kutoka shuleni. Kila mmoja anataka kuzungumza na Ngoyoni ili aelezwe hali ilivyo katika shule yao.

Kupitia kwa maelezo tunaona kuwa kuna taswira ya uoni kuhusu mazingira ya shuleni ambapo tunapata tofauti ya kimasomo katika Shule ya Masomoni na Shule ya Msingi ya Mitini. Katika shule ya Masomoni walimu wanatia bidii kusaidia watoto. Kila mtoto anasaidiwa kibinafsi na watoto wana nidhamu. Maendeleo ya kila mtoto yanatambuliwa na kuzawadiwa ili kuwatia motisha.

Taswira ya uoni inayohusu mazingira ya shuleni katika *Kisasi Hapana* ni ya uchezaji wa mpira. Uwanja wa akina Kido unaelezwa kitaswira kuwa umekanyagwa kiasi cha kukosa nyasi. Wakati wa mvua unakuwa na matope kama kinamasi na wakati wa kiangazi unakuwa na vumbi kama jangwa. Katika uwanja huu pia kuna taswira ya namna Kido na watoto wenzake walivyogawana kucheza na jinsi walivyocheza mpira wa kandanda kwa madaha na furaha tele. Ili kutengeneza timu mbili pinzani, wanapanga laini kisha kila mmoja anakwenda upande wa kulia au kushoto. Hatimaye kuna taswira ya uoni ya jinsi Kido alivyocheza mpira kwa ustadi kuliko watoto wengine wote kwa kuwachenga na hata kufunga mabao ambayo hangeweza kuhesabu na kisha kupata ajali akicheza mpira na kuvunjika mguu.

Katika *Kisasi Hapana,* tunapata taswira ya uoni pale ambapo kupitia maelezo tunaona foleni ndefu ya wagonjwa katika hospitali ya Mito Mitatu wakisubiri zamu yao ifike wahudumiwe. Pia kuna makabiliano ya nyanya ya Kido na askari anapojaribu kuingia kwa daktari kwa nguvu bila ruhusa baada ya kugundua kuwa wagonjwa wengine wanaingia tu ndani na kumwona daktari bila kufuata utaratibu uliowekwa. Daktari anaingilia kati na kumruhusu nyanya ya Kido kuongea naye.

Mwandishi wa *Nimefufuka* kwa upande wake anatuonesha taswira ya uoni inayohusu ugonjwa wa Lena aliyekuwa amekonda na kukondeana na tunaelezwa kuwa anaendesha kwa ugonjwa usiojulikana huku akiwa na mimba. Kila njia ya matibabu inatumiwa lakini hakuna nafuu inayopatikana hadi anapokufa. Taabu, mwana wa Lena naye amekondeana na hata kuendesha kwa maradhi yasiyojulikana. Maelezo yanatufanya tuamini kuwa lazima ugonjwa huu wa Taabu ulikuwa ni ugonjwa hatari sana ambao unatishia kumuua jinsi ulivyomuua mamake. Kupitia kwa taswira tunapata hali mpya ya kuimarika kwa kiasi fulani kwa afya ya Taabu na Jose. Baada ya Taabu kubadilishiwa jina na kuitwa Shujaa, anakoma kukojoa kupita kiasi na anaonekana mwenye afya njema na tabasamu usoni. Akili za Mama Lena pia zinaelezwa kuwa zimeganda kwa kufikiri kupita kiasi na sasa akili zake hazifanyi kazi vizuri. Taswira hii ya kuganda kwa akili imetiwa chumvi mno kwa vile ni kana kwamba Mama Lena sasa hawezi kufikiri lolote.

Katika *Kisasi Hapana* kunatokea taswira nyingine ya uoni ambapo ni usiku na nyanya ya Kido anajaribu kusimamisha gari fulani ili wasindikizwe kisha dereva anasimama na kumpiga nyanya ya Kido vibaya kwa mshipi. Riwaya ya *Nimefufuka* pia ina taswira ya uoni ambapo tunaona urembo wa Lena unaolinganishwa na urembo wa tausi uliowavutia wanaume kwa wingi na namna Lena alivyobadilibadili wanaume kama nguo. Wanaume hawa ni Wazungu, Wahindi na Weusi. Pia, kuna taswira ya jinsi Lena na mpenzi wake wanavyoonekana na kujipamba wakati walipopatikana na Mama Lena. Walikuwa wameshikana nyonga na mpenzi wake huku wamevaa nguo zisizoficha uchi wao vizuri. Kupitia kwa taswira hii tunapata picha kamili ya maisha ya anasa ya Lena akiwa kule Pwani. Taswira ya uoni ya kuchanganyikiwa kwa Mama Lena akiwa kule Pwani inaangaziwa ambapo hakujua popote na ilibidi Musa kuandamana naye kumwonesha alikotaka kuenda. Hata ikabidi Musa kuomba ruhusa kutoka kazini ili kumsindikiza Mama Lena kumtafuta

binti yake. Baada ya kumpata mwanawe, tunaoneshwa taswira ya uoni namna Lena anavyowatazama mamake na Musa kwa madharau kwa kuigilia faragha yao. Anawaona kama vinyaa na vinyangarika waliokuja kumharibia starehe zake.

Katika *Sitaki Iwe* Siri, kuna taswira ya uoni ya jinsi Mwalongo anavyomwamsha Musa asubuhi na mapema na kisha Musa kuzinduka kutoka usingizini na kupapasa juu ya meza ili kupata taa yake ya kibatari na kuiwasha. Baadaye kuna taswira ya uoni Musa anapowaamsha dada zake Haki na Ukwa ambao walikuwa katika usingizi mzito wa pono. Kuna taswira nyingine ya uoni inayotokana na ufafanuzi wa shule ya akina Musa asubuhi ile wanafunzi wakiingia shuleni katika makundimakundi huku wengine wakipiga gumzo. Wamebeba begi zao mgongoni kama watalii na wako nadhifu sana kwa sababu ni siku ya kwanza ya wiki. Baada ya kufika shuleni, tunaoneshwa taswira ya uoni jinsi wanafunzi walivyokuwa wakicheza pale shuleni asubuhi ile. Kulikuwa na makundi mbalimbali ya wanafunzi wakicheza michezo tofautitofauti kama mpira, mwajificho na kuruka kamba huku wakiwa na furaha kubwa kabla ya kuenda gwarideni na kuingia madarasani. Pia tunaoneshwa wanafunzi wakiwa kwenye gwaride wakikaguliwa na Mwalimu Ochuka anayepita kati ya safu za foleni zao na kuangalia usafi wa nywele, kucha na sare zao. Kisha wanapandisha bendera na kuimba wimbo wa taifa. Hatimaye wakiwa bado wako pale gwarideni kuna taswira ya uoni ya mwalimu mkuu Bwana Selemani ambaye alikuwa mnene, mweusi na mwenye upara kichwani. Alikuwa mcheshi na alipendwa na wanafunzi wote shuleni. Anawahutubia wanafunzi hawa kabla ya kuwaruhusu waingie madarasani.

Taswira nyingine ya uoni katika *Sitaki Iwe Siri* ni ya umbo la utingo na inaelezwa kuwa ni wa umri wa makamo, macho mekundu na mikono iliyokauka kama vibanzi. Pia kuna taswira ya uoni ya mwonekano wa Daktari Ataya ambaye anaelezwa kuwa mwenye macho makali yaliyopenya kama miale ya jua alipowatazama akina Musa, Haki na Ukwa. Alikuwa

amevalia koti jeupe kama maziwa. Taswira hizi ni za kisitiari kwani zinadokeza kuhusu kazi ya hawa wahusika. Kwa mfano, Bwana Ataya anahitaji macho ya kutazama kwa undani ili kutambua ugonjwa wa watu na hivyo kuelezwa kuwa ana macho yanayopenya kama miale ya jua.

Katika *Wema wa Mwana* kuna taswira ya kuhisi na inahusu namna Juma anavyotenda anapozidiwa na kuchomwa na nyama iliyoko mfukoni mwake. Anaonekana kusakamwa na maumivu ingawa anajikaza sana ili isigunduliwe na baba yake. Taswira hii imetiwa chuku ili picha ya mwonekano wa Juma isimtoke msomaji akilini na pia kusisitiza funzo hasa kwa msomaji mtoto kuwa wizi si tabia nzuri. Katika *Kisasi Hapana* kuna taswira ya kuhisi inayohusu safari ya Kido, mamake na nyanyake kutoka hospitalini kurudi nyumbani ambapo mamake na nyanyake wanasaidiana kumbeba Kido kwa kupokezana. Ni jioni sana kuelekea usiku na kuna giza kwa kiasi fulani na safari pia inaonekana kuwa ndefu. Wanaposhindwa na uzito wa Kido na uchovu kuwaingia wanaketi chini kupumzika kidogo. Pia katika *Nimefufuka* kuna taswira ya kuhisi inayohusu hasira ya mama Lena kwa kukosa kumpata mwanawe kule Mombasa.

Katika kazi ya Ken Walibora ya *Kisasi Hapana,* tulipata taswira ya kusikia kutokana na kilio cha kila siku cha mama ya Kido baada ya babake kuondoka na kuwekwa korokoroni. Mama huyu analia kama mtoto mdogo kwa sababu ya upweke unaomkabili. Pia kuna taswira ya kusikia ya uganaji hadithi na mashairi wa nyanya ya Kido. Uganaji huu ni wa makini na wa kufurahisha hivi kwamba unaonwa na Kido kuwa kama chakula. Kido alifurahia vipindi hivi kila jioni.

Kuna taswira mbili za mguso ambazo zimejitokeza katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri*. Kwanza ni ya jinsi Mwalongo anavyomwamsha Musa asubuhi na mapema na kisha Musa kuzinduka

kutoka usingizini na kupapasa juu ya meza ili kupata taa yake ya kibatari na kuiwasha. Taswira ya umbo la utingo inaelezwa kuwa ni wa umri wa makamo, macho mekundu na mikono iliyokauka kama vibanzi. Hapa kukauka kwa vibanzi hudhihirika kupitia kwa kuguswa.

Kutokana na mjadala huu basi ni wazi kuwa taswira ambazo zimetumiwa na waandishi hawa zimejengeka katika mandhari ambayo watoto wanaweza kukumbana nayo katika maisha yao ya kila siku na hivyo kujinasibisha nazo. Taswira hizi pia zimesheheni uhalisi unaofanya iweze kuwa rahisi kwa watoto kuelewa. Waandishi wote wametumia maelezo ya kina na kutokeza taswira hizi kwa undani. Kuna taswira moja iliyo sawa katika *Sitaki Iwe Siri* na *Nimefufuka*. Ni taswira ya wazazi wa Haki na Ukwa na Musa kukondeana na kisha kufa. Taswira hii pia inapatikana katika *Nimefufuka* ambapo Lena anaoneshwa kitaswira akiwa amekonda kutokana na maradhi fulani yasiyojulikana na kisha kufa. Ni kama wahusika hawa wanaugua kutokana na ugonjwa sawa. Mtoto wa Lena, Taabu, pia amechorwa akiwa na hali hii ya kukonda kutokana na maradhi ya ajabu nusura afe. Kuna uwezekano kuwa taswira hizi zinadokeza kuhusu ugonjwa hatari wa Ukimwi. Pia imedhihirika wazi kuwa waandishi wote wametumia taswira za mguso, hisi, uoni, kusikia na mwonjo. Hata hivyo, taswira za uoni zimechukua sehemu kubwa mno. Katika *Nimefufuka* na *Sitaki Iwe Siri* waandishi wametumia taswira kadhaa kueleza kindani kuhusu michezo ya watoto wakiwa shuleni. Hili linafaa sana fasihi ya watoto kwani wao ndio hupenda mno michezo wakiwa katika umri huu.

Kwa kuhitimisha basi imebainika kuwa taswira zinazomjia msomaji haziwezi kuhesabiwa kwa sababu maelezo yote ya mwandishi katika kazi husika hutoa taswira fulani kwa msomaji. Taswira moja pia huweza kuzalisha taswira nyingine ndogondogo ili kuunda taswira moja kuu. Pia taswira inayomjia msomaji inategemea jambo linalomvutia msomaji

katika maelezo hayo na msomaji mmoja anaweza kuamua kutilia maanani sehemu tofauti na msomaji mwingine. Ni wazi pia kuwa vipengele vingine vyote vya fani husaidia kujenga taswira mbalimbali katika kazi ya fasihi. Hii inamaanisha kuwa taswira haziwezi kusimama pekee yazo bali hutegemea maelezo au usimulizi na vipengele vingine vya fani ili kupata maana kamili. Kwa hiyo, inafaa kutaja kuwa taswira ambazo zimejengwa katika vitabu tulivyotafiti zinasawiri picha sahili na inaweza kuwa rahisi kuzielewa na kuzikumbuka. Kwa mfano, katika ukurasa wa 7 wa riwaya ya *Wema wa Mwana,* mwandishi anaeleza kuwa Juma alikuwa anatetemeka kama matawi ya mnazi alipoitwa na babake akiwa na nyama mfukoni. Inaweza kuwa rahisi kwa mtoto kujua namna matawi ya mimea hutetemeshwa na upepo na hivyo picha ya namna Juma anavyotetemeka inamjia msomaji mtoto kwa urahisi, inaweza kumchekesha na kubaki akilini kwa muda mrefu na hivyo funzo analopata pia litadumu.

### 4.1.3 Nahau

Nahau ni msemo uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida. Aghalabu nahau huwa imesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno ya nahau yenyewe (Msokile, 1992). Nahau pia inaweza kufafanuliwa kuwa semi fupifupi ambazo hutumia lugha au maneno ya kawaida lakini hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno yenyewe. Japokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida, kauli yake ina undani kiasi kwamba kwa wageni wasiofahamu lugha hiyo hawawezi kuelewa maana (Saluhaya, 2013). Nahau pia inaweza kuelezwa kuwa ni semi zenye kitenzi tofauti na misemo ambayo ni semi zisizokuwa na vitenzi. Nahau ina sifa kama kuwa na maana zaidi ya moja, huundwa kwa lugha ya mkato, nahau mbili au zaidi huweza kuwa na maana moja na pia huundwa kwa maneno mawili au zaidi. Wamitila (2003) anaongeza kuwa kimuundo, nahau huwa na kitenzi na jina. Dhima ya nahau katika jamii ni kama kufunza maadili, kukuza lugha, kuhekimisha, kuendeleza utamaduni na matumaini (Namanya, 2016).

Kwa kuongozwa na maelezo ya wataalamu hawa wa fasihi, tulitambua nahau mbalimbali katika riwaya tulizokuwa tunachunguza. Katika sehemu hii tulichanganua nahau kwa misingi ya idadi, miundo yake, vitenzi vilivyotumiwa na hali ya maisha zinamojikita. Tulitoa mifano kuthibitisha kila hali kutokana na riwaya za waandishi mbalimbali tunaochunguza katika utafiti wetu. Hata hivyo, baadaye katika sehemu ya 4.3 tumeonesha namna nahau hizo zinavyochangia kufanikisha maudhui katika riwaya tulizochunguza.

**Jedwali 4.3:** ***Nahau katika Riwaya za Watoto***

| **Riwaya** | **Idadi ya Nahau** |
| --- | --- |
| *Kisasi Hapana* | 20 |
| *Sitaki Iwe Siri* | 16 |
| *Nimefufuka* | 6 |
| *Wema wa Mwana* | 3 |
| **Jumla** | **45** |

Kutokana na data hii imebainika kuwa mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia nahau kwa wingi sana akiwa na jumla ya nahau 20 ikifuatiwa na *Sitaki Iwe Siri* ambayo ina nahau 16. *Nimefufuka* na *Wema wa Mwana* ni riwaya zilizotumia nahau chache zikiwa na 6 na 3 mtawalia. Kwa ujumla basi, waandishi hawa wametumia nahau 45 katika kazi zao. Idadi hii kubwa ya nahau ni ithibati tosha kuwa nahau ni kipengele muhimu kilichotumiwa kuendeleza kazi hizi.

Kitenzi "piga" kimetumiwa kwa njia mbalimbali na waandishi wote. Riwaya ya *Kisasi Hapana* imetumia "piga" mara tatu. Kwa mfano: "Utawasikia nikiwapiga chenga watu" (Uk. 23), "Nikampiga chenga beki wao" (Uk. 28) na "Nikavuta kasi na kupiga shuti safi sana" (Uk. 28). Katika *Nimefufuka* kitenzi hiki "piga" kimetumiwa mara tatu. Kwa mfano, "Mama alipigwa na butwaa" (Uk. 4), "Wakapiga dau" (Uk. 8) na "Kumwendea mganga

ampigie ramli ndugu yangu" (Uk. 13). Riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* imetumia kitenzi "piga" mara nyingi zaidi kuliko riwaya hizo nyingine tatu ikiwa na nahau nne. Mifano ya matumizi yake ni: "Akipiga miayo" (Uk. 1), "Walianza kupiga miundi" (Uk. 6), "Hatimaye alipiga moyo konde" (Uk. 19) na "Baada ya kuhakikisha kwamba insha yake imepigwa msasa aliitumbukiza posta" (Uk. 49).

Katika *Wema wa Mwana,* nahau zinazotumia kitenzi "piga" zimetumiwa mara mbili pekee. Nahau hizo ni: "Mamake aliuliza huku amepigwa na butwaa" (Uk. 7) na "Baba Juma aliona gere na njiani walipiga gumzo hadi wakafika nyumbani" (Uk. 16). Katika nahau ya kwanza 'kupigwa na butwaa' inamaanisha kuwa mama ya Juma alikuwa na mshangao mkubwa kwa kugundua tabia ya Juma ya kuiba chakula kutoka jikoni. Katika Nahau ya pili "walipiga gumzo njiani hadi wakafika nyumbani" inarejelea mazungumzo kati ya Baba Juma na Baba Ngoyoni walipokuwa wametoka kumlaki Ngoyoni kutoka shuleni mwishoni mwa muhula.

Katika *Nimefufuka* pia kuna matumizi ya nahau ambazo zinahusu ugonjwa na kifo cha Lena. Nahau hizo ni kama: "Kumwendea mganga ampigie ramli ndugu yangu" (Uk. 13), "Kwamba kifo kinamkodolea macho" (Uk. 15), na "Aliaga dunia siku chache baada ya kujifungua mwana wa kiume" (Uk. 8). Nahau ya kwanza ikimaanisha Lena alipelekwa kwa mganga amsaidie kutambua chanzo cha ugonjwa huku ile ya pili inamaanisha kuwa maisha yake Lena yalikuwa hatarini na alielekea kufa. Nahau hii inatuchorea picha ya kifo kikiwa kinaonekana kuwa na macho na kutazama kama binadamu. Kwa njia hii nahau hii imetumiwa kutia chuku katika masimulizi haya. Hatimaye nahau kuaga dunia imetumiwa kumaanisha kufa. Katika *Sitaki Iwe Siri,* nahau zinazohusu ugonjwa na kifo ni kama: "Yusufu na mke wake waliugua kwa muda mrefu sana na hatimaye kusalimu amri" (Uk. 8).

Kigezo kingine muhimu cha uchanganuzi wa nahau ni matumizi ya nahau hizo katika mazingira yanayohusiana na ugonjwa na kifo. Ken Walibora katika *Kisasi Hapana*

ametumia nahau zinazohusu ugonjwa na kifo katika nahau kama: “Amekwenda jongomeo” (Uk. 3), “Ametuacha mkono” (Uk. 3), “Alivyotuacha mkono” (Uk. 11) na “Nilipata nafuu baada ya siku chache.” Nahau hizi zimetumiwa kumaanisha nyanya ya Kido alikuwa amekufa. Hata hivyo, katika nahau “amekwenda jongomeo” dhana inayodokezwa na mwandishi ni kuwa mfu ameenda safari fulani ikimaanisha mtu anapokufa anaenda mahali fulani.

Katika uhakiki wa nahau imekuwa wazi kuwa nahau zinazohusu michezo ni sehemu muhimu. Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia nahau zinazohusu uchezaji mpira hasa unaomhusisha Kido na zinafafanua jinsi ya kupitisha mpira kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine hadi wanapoingiza mabao. Nahau hizi ni: “Utasikia nikiwapiga chenga watu na kuwavisha kanzu uwanjani”, “Kukata tamaa ya kuwa mchezaji wa kimataifa”, “Nikawala chenga na kupasua safu ya wachezaji kama watatu hivi”, “Nikatoa pasi nzuri kwa Saulo”, “Na kutoa pasi nyingine nzuri”, “Nikampiga chenga beki wao”, “Nikakata mbuga”, “Nikavuta kasi na kupiga shuti safi sana”, “Na ningekuwa mzima kama wao ningewala chenga”, “Ningewavisha kanzu,” na “Nikawachezea chovoo na kuwafunga mabao” (Uk. 28).

Katika uchanganuzi huu ilibainika kuwa kipengele kingine cha kuhakiki nahau ni matumizi yake kuhusiana na kutia bidii katika hali mbalimbali maishani. Nahau hizo katika *Kisasi Hapana* ni: “Nilijikaza kisabuni” (Uk. 11), “Hawa watu wazima wa kijijini kwetu wanajua ulipo ila wamekula njama kunificha” (Uk. 17), “Ndoto zangu zinaelekea kugonga ukuta” (Uk. 30), ‘Fanya hima” (Uk. 33), “Uwafanye adabu waliotukosea” (Uk. 34) na “Endelea kuvuta subira na kuniombea” (Uk. 35). Katika nahau “nilijikaza kisabuni”, dhana inayojitokeza ni hali ya kutia bidii licha ya hali ngumu. “Kula njama” kunamaanisha kula kiapo ili kutosema habari fulani kwa mtu mwingine. Katika hadithi hii, majirani wanakataa

kumwambia Kido kuhusu alipo babake. “Ndoto kugonga ukuta” inahusu kutofaulu kwa Kido kuwa mchezaji hodari kwa kuvunjika mguu. Katika *Sitaki Iwe Siri*, nahau zinazohusu bidii ni kama, “Musa alisema kwa utani huku wote wakiangua kicheko”, “Alijitia moyo kwamba lisilo budi hutendwa”, “Baada ya kuketi kitako na kuishtaki njaa”, “Walianza kupiga miundi kwa hatua za chapuchapu” (Uk. 6), “Baada ya kuhakikisha kwamba insha yake imepigwa msasa aliitumbukiza posta” (Uk. 49), “Alijifunga kibwebwe kushiriki kwenye shindano hilo” na “Alikwenda kuwaandikia meza” (Uk. 5).

Aina nyingine za nahau ni zile zinazorejelea anasa. Katika kazi ya *Nimefufuka* kuna nahau ambayo inarejelea maisha ya anasa ya Lena akiwa kule mwambao. Mwandishi anasema “Lena alitorokea Mombasa eti kuponda maisha” (Uk. 4). Nahau hii imetumiwa kumaanisha kuwa Lena alienda Mombasa ili kufurahia maisha ya anasa.

Utafiti pia ulibaini nahau zinazohusiana na kutamauka. Katika *Nimefufuka* nahau hizo ni “Jitihada zaidi za kumwona Lena ziliambulia patupu” na “Musa alisalimu amri” (Uk. 4). Nahau ya kwanza inamaanisha kuwa Mama Lena hakufaulu katika kumpata mwana wake licha ya kutia bidii za mchwa katika kumsaka ili kumtoa katika lindi la ufuska. Maana tunayopata katika nahau ya pili ni kuwa Musa alikubali ingawa shingo upande kumsaidia mama Lena kumtafuta mwana wake.

Hatimaye, kuna nahau zinazohusiana na chakula. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia nahau mbili zinazohusu chakula. Nahau hizo ni: “Alikwenda kuwaandikia meza” (Uku. 5) na “Baada ya kuketi kitako na kuishtaki njaa” (Uk. 26). Nahau ya kwanza inamaanisha nyanya Mwalongo aliwaandalia wajukuu wake kiamshakinywa kabla ya kuondoka kwenda shuleni huku ya pili inamaanisha kuwa waliketi chini ili kula na kumaliza njaa yao.

Imebainika kuwa waandishi wote wanne wametumia nahau tofauti kabisa bila kuwa na mfanano wowote. Katika riwaya ya *Kisasi Hapana*, Ken Walibora ametumia nahau nyingi

sana kuhusu michezo hasa jinsi ya kupitisha mpira kutoka kwa mchezaji mmoja kwenda kwa mwingine hadi pale wanapofunga mabao. Pia katika *Kisasi Hapana* kuna nahau kadhaa zinazotoa picha ya ugonjwa na kifo na zimetumiwa kurejelea kifo cha nyanyake Kido. Kuhusu ugonjwa wa Kido pia kuna nahau "nilipata nafuu baada ya siku chache." Riwaya ya *Nimefufuka* kwa upande mwingine ina nahau nyingi zinahusu ugonjwa na kifo zikimlenga hasa mhusika Lena, maisha yake ya anasa, ugonjwa na kisha kifo chake. Hatimaye *Sitaki Iwe Siri* ina nahau kumi zikihusu kufanya bidii maishani na masomoni na zinaangazia hasa mhusika Musa. Katika sehemu ya 4.3 tulionyesha jinsi nahau hizi zilivyotumiwa na waandishi hawa ili kuendeleza maudhui mahususi katika kazi husika.

#### 4.1.4 Misemo

Wamitila (2003) anaeleza kuwa msemo ni dhana inayotumiwa kuelezea tungo ambazo hutumia picha, ishara na tamathali kueleza kitu au wazo kwa ufupi ili litolewe maadili au maonyo fulani. Misemo hutumia maneno ya kawaida kinjozi au kwa njia isiyo ya kawaida na huhitaji mtu kufikiria kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika. Lengo la kutumia misemo ni kusitiri maana, kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo, kulinganisha maisha na matukio au vitu na pia kueleza kauli ambazo hueleza ukweli fulani. Misemo pia hutumika kutambulisha mazingira maalum au kujulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa kwa sababu maneno hayo hutumika kama yalivyo katika mazingira maalum kuleta maana maalum (Njagi, 2002). Maelezo haya yalitusaidia kuelewa sifa za misemo na hivyo kuitambua misemo hiyo katika kazi ambazo tulitafiti. Katika sehemu hii tumeorodhesha idadi ya misemo tuliyotambua katika jedwali kisha tumechanganua misemo hii kwa misingi ya idadi, muundo au mtindo na masuala yanayoangaziwa na misemo hii kama vile masuala ya ugonjwa, kifo, elimu, bidii, kazi, na malezi ya watoto.

**Jedwali 4.4:** ***Misemo katika Fasihi ya Watoto***

| **Riwaya** | **Idadi ya Misemo** |
|---|---|
| *Kisasi Hapana* | 11 |
| *Wema wa Mwana* | 9 |
| *Sitaki Iwe Siri* | 7 |
| *Nimefufuka* | 3 |
| **Jumla** | **30** |

Kutokana na data hii imebainika kuwa kwa ujumla, waandishi wote wametumia misemo 30 katika kufanikisha kazi zao. Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ameongoza kwa idadi ya misemo na ametumia misemo 11, *Wema wa Mwana* ametumia misemo 9, *Sitaki Iwe Siri* ametumia misemo 7 hatimaye mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia misemo 3. Katika utafiti huu pia imebainika kuwa misemo mingi iliyotumiwa na waandishi hawa inahusu hali ya afya na ugonjwa ikifuatiwa na misemo inayohusu bidii kazini.

Kigezo cha kwanza katika uhakiki wetu wa misemo ni kile kinachohusiana na ugonjwa na kifo. Ken Walibora katika *Kisasi Hapana* ametumia misemo inayohusu ugonjwa na kifo kama: “Ametuondokea” (Uk. 3) na “Wewe ndiwe ungenishughulikia kwa hali na mali” (Uk. 28). Msemo wa kwanza umetumiwa kumaanisha kuwa nyanya ya Kido alikuwa amekufa huku msemo wa pili ni kauli ya Kido akimwambia babake kuwa ikiwa angekuwa karibu Kido alipokuwa mgonjwa angemtunza kwa vyovyote vile wakati wote wa ugonjwa wake. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia msemo unaohusu ugonjwa na kifo katika familia ya akina Sikitu kama vile “Jana nusura Jose atupe mkono wa buriani.” Kutupa mkono wa buriani imetumiwa kumaanisha kuwa Jose alikaribia kufa  ila alinusurika tu kwa nguvu za Mungu.

Aidha, kuna misemo inayohusu utu na ukarimu kati ya washiriki wa familia kama vile “Nimejitolea kukusaidia kwa hali na mali”, na “Kama ulivyonifaa” (Uk. 15). “Mjomba humpa mama moyo wa kujikakamua zaidi.” Msemo kukusaidia kwa hali na mali inamaanisha kusaidia kwa uwezo na namna zote.

Kipengele kingine kinachohusiana na misemo iliyotambuliwa ni ile inayohusu maisha ya shuleni na michezo. Katika *Kisasi Hapana*, misemo hiyo ni: “Uwanja umenyolewa nyasi na miguu yetu” na “Nikarejea shuleni tena, lakini shingo upande” (Uk. 11). Msemo wa kwanza unamaanisha nyasi zilikauka katika uwanja wa akina Kido kutokana na kukanyagwa kila mara wakati wa mchezo. Maana inayojitokeza katika msemo wa pili ni kuwa Kido alirudi shuleni baada ya kupona ugonjwa wake lakini kwa kulazimishwa tu. Katika *Sitaki Iwe Siri*, mwandishi ametumia misemo miwili kuhusu mazingira ya shuleni. Misemo hii ni: “Kufumba na kufumbua kengele ya mapumziko ikalia” (Uk. 22) na “Walimu wake walivyojitahidi kwa hali na mali kumwelimisha” (Uk. 47). Msemo huu wa kwanza unatumiwa ili kuonyesha jinsi muda huenda haraka kwa wanafunzi wakiwa shuleni. Ni kama tu kufumba na kufumbua macho ambacho ni kitendo kisichochukua hata sekunde. Katika msemo wa pili inamaanisha walimu hawa walijitolea sana ili kumsaidia Musa afaulu masomoni. Hata wanatumia pesa zao wenyewe mbali na muda wao kuhakikisha kuwa anafaulu katika uandishi wa insha kuhusu ugonjwa wa Ukimwi.

Aidha, misemo mingine iliyotambuliwa inahusu kazi. Katika *Sitaki Iwe Siri* misemo kama hii ni: “Magari yaliyojaa mizigo pomoni”, na “Ni dereva tu aliyekuwa akimenyana na usukani (Uk. 28). Katika msemo wa kwanza maana inayojitokeza ni kuwa gari hili lilijaa kiasi cha kutobakiza nafasi yoyote. Msemo wa pili unamaanisha kuwa watu wengine wote walikuwa wamenyamaza hata pengine kulala lakini dereva alibaki kazini akiendesha gari ili kufikisha wateja wake walikokuwa wakienda.

Hatimaye, kigezo kingine ni kile cha misemo inayohusu malezi katika familia ambapo riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* inatuchorea nyanya Mwalongo akiwatunza wajukuu wake alioachiwa na watoto wake baada ya kuuliwa na ugonjwa wa Ukimwi. Msemo huu ni: "Amewatunza wajukuu hawa miaka nenda miaka rudi" (Uk. 9). Msemo huu umetiwa chumvi kwa sababu hawa watoto bado wako shule ya msingi kumaanisha si miaka mingi sana imepita tangu wazazi wao walipokufa. Kwa hiyo msemo huu unasaidia tuelewe kuwa uwezo wa nyanya huyu ni mdogo na kwa hivyo miaka hii michache aliyotunza wajukuu wake ni kama ametumia uwezo wake wote na kwa hiyo kuonekana kuwa muda mrefu mno. Baadaye katika sehemu ya 4.3 tumeonyesha namna misemo hii tuliyotambua imefumwa na wasanii hawa kufanikisha maudhui yanayolenga watoto katika vitabu husika.

### 4.1.5 Methali

TUKI (2013), inaeleza methali kuwa ni usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yanayotumiwa. Methali hutumiwa kuelezea kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe maadili au maonyo fulani. Njagi (2002) anaendelea kusema kuwa methali humwingiza msikilizaji au msomaji katika hali ya kufikiri, kuchambua na kupatanisha ukweli na hali ili ajue maana ya ndani iliyokusudiwa, husaidia hadhira kukumbuka wazo kuu, hutumiwa kufafanulia maelezo ya msingi na kudhibiti kaida za kisarufi. Aidha, methali hutumiwa kujenga taharuki, ni chombo cha kuwasilisha hisia, kubainisha itikadi za mtunzi, kuelekeza na kuadilisha jamii. Maelezo haya yalituongoza kwa kutaja sifa za methali na tuliweza kutambua methali mbalimbali katika vitabu vya fasihi kwa kutemea vigezo hivi.

Baada ya kuonesha maana ya methali na umuhimu wake katika sehemu hii, tumedondoa na kuchambua methali kutoka riwaya zote nne. Tumehakiki methali hizo kwa kulinganisha na kulinganua matumizi yake kati ya hawa waandishi wanne. Pia tumetathmini miundo ya

methali hizi na kuonesha matumizi yake katika miktadha mbalimbali. Baadaye katika 4.3 tulionyesha jinsi baadhi ya methali hizi zimechangia kufanikisha kueleweka kwa maudhui katika riwaya hizo. Jedwali 4.5 inaorodhesha methali zilizojitokeza katika riwaya mbalimbali tulizochanganua.

**Jedwali 4.5:** ***Methali katika Fasihi ya Watoto***

| **Kitabu** | **Idadi ya Methali** |
|---|---|
| *Nimefufuka* | 20 |
| *Sitaki Iwe Siri* | 12 |
| *Kisasi Hapana* | 11 |
| *Wema wa Mwana* | 6 |
| **Jumla** | **49** |

Waandishi wote wanne wametumia methali 49. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia methali nyingi zaidi akiwa na methali 20 akifuatiwa na waandishi *wa Sitaki Iwe Siri* na *Kisasi Hapana* ambao wana methali 12 na 11 mtawalia. Mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia methali 6 tu.

Uchanganuzi huu umebainisha matumizi ya methali katika mazingira ya maisha ya familia, majukumu katika familia na mahusiano yake katika nyanja mbalimbali. Mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia methali kama: "Kumbe kuzaa si kazi, kazi ni kumlea mwana" (Uk. 11), "Mwana akililia wembe mpe" (Uk. 12), "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" (Uk. 15) na "Mwana mkaidi hafaidi" (Uk. 20). Katika methali "kumbe kuzaa si kazi, kazi ni kumlea mwana" tunapata wazo la kwamba mzazi anahitaji muda na bidii zaidi katika kumlea mtoto kuliko ilivyo katika kumzaa mtoto yuyo huyo. Methali "mwana akililia wembe mpe" imetumiwa kumaanisha kuwa ni vigumu kumzuia mtoto kufuatia kile anachoona kuwa ni kizuri kwake hata ikiwa ataumia. Methali hii inarejelea hali ya Juma

kutwalia nyama mekoni iliyomchoma na kumuumiza vibaya. Hatimaye methali "alisahau kwamba mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" imetumiwa kuwatahadharisha wazazi kuwa inawabidi waamue jinsi wanavyotaka watoto wao wawe na kujizatiti kuwakuza kuelekea lengo hilo. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia methali "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" (Uk. 20) ili kubainisha nafasi ya mzazi katika ulezi wa watoto. Pia ametumia methali kama "Damu kweli ni nzito" (Uk. 12), "Nimeamini mtu ni watu" (Uk. 28), "Mtegemea ndugu hufa maskini" (Uk. 29), "Angesema nini ilhali aliogopa, kumkunja samaki angali mbichi" (Uk. 4), "Wazazi walibaki kulaumiana badala ya kuganga yajayo" (Uk. 4), na "Mchuma janga hula na wa kwao" (Uk. 10).

Kigezo kingine kinachohusiana na uhakiki wa methali ni zile methali zinazohusiana na heshima. Katika riwaya ya *Wema wa Mwana* methali hizo ni kama: "Kwa kweli heshima si utumwa" na "Ni bora kuitikia mwito kuliko kujitia moto." (Uk. 20). Na katika *Sitaki Iwe Siri* kuna methali kama "Mtu hakatai wito hukataa aitiwalo" (Uk. 20).

Aidha, kuna zile methali zinazohusiana na kisasi. Kwa upande wake, mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia methali ambazo zinahusu chuki na tamaa ya kulipiza kisasi. Tulitambua methali kama: "Asomlifi, mlifi ni Mungu" (Uk. 12), "Dawa ya moto ni moto" na "Akutendaye mtende" (Uk. 30). Methali hizi zimetumiwa na Kido kuonyesha hasira yake kuelekea waliowatendea mabaya.

Kipengele kingine ni zile methali zinazohusu kukata tamaa na kutamauka. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia methali 6 zenye kukatisha tamaa na zinadokeza ukosefu wa matumaini. Methali hizi ni kama: "Mchuma janga hula na wa kwao", "Kwani ng'ombe akivunjika guu malishoni, hujikokota zizini kusaidiwa" (Uk. 10), "Wakamwacha afunzwe na dunia", "Hawakujua yaliyomwagika hayazoleki", "Alivuna alichopanda kwa kufukuzana na maisha" (Uk. 19), "Mtego uo huo huwanasa waliomo na wasiokuwamo"

(Uk. 20) na “Mtegemea ndugu hufa maskini” (Uk. 29). Katika methali “Mchuma janga hula na wa kwao”, dhana inayojitokeza ni kuwa Lena aliponda raha akiwa pekee yake lakini anapokuwa mgonjwa inabidi washiriki wa familia yake wamsaidie kupata matibabu. Anapokufa wanajamii wa karibu wanachanga pesa ili kumzika.

Aidha, kuna methali zinazohusu matatizo na majuto katika maisha. Kwa mfano, methali 6 zimetumiwa katika riwaya ya *Nimefufuka* na zinagusia maisha ya matatizo na majuto katika maisha ya wahusika kadhaa ambao wanakosa kutimiza majukumu yao mapema na hivyo kulia baadaye au kuumia. Methali hizo ni:

i. “Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo” (Uk 26)
ii. “Udongo upate uli maji” (Uk. 26).
iii. “Kuteleza si kuanguka” (Uk. 31).
iv. “Alivuna alichopanda kwa kufukuzana na maisha” (Uk. 19).
v. “Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake” (Uk. 17).
vi. “Wanasahau kuwa mtego uo huo unawashika waliomo na wasiokuwamo”. (Uk 4)

Katika *Sitaki Iwe Siri* zile methali zinazohusu kilio na majuto ni: “Lakini akalilia wembe” na “Nyembe za walimwengu zilikuwa zimemkata Yuri na kumjeruhi vibaya” (Uk. 48).

Kwa upande mwingine, kinyume na methali zinazokatisha tamaa, waandishi hawa pia wametumia methali ambazo zinatoa matumaini hasa baada ya matatizo na mahangaiko mengi. Katika *Nimefufuka,* methali hizo ni “Panapo nia pana njia” (Uk. 5), “Lakini kumbuka baada ya dhiki faraja”, “Kuteleza si kuanguka”, “Tugange yajayo” na “Ulimwengu ni kikoa, nifae nikufae, tufaane” (Uk. 23).

Katika *Sitaki Iwe Siri* pia kuna methali ambazo zinatoa matumaini hasa baada ya matatizo na mahangaiko mengi kama vile “Kusafiri kwingi ndiko kujua mengi”, “Ajidhaniye kusimama aangalie asianguke” (Uk. 45), “Hayawi hayawi hatimaye huwa” (Uk. 52), “Mambo ni kangaja huenda yakaja” (Uk. 52) na “Kilicho na mwanzo hakikosi kuwa na mwisho” (Uk. 66).

Waandishi wametumia methali kadhaa kwa njia sawa kati yao. Kwa mfano, mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia methali "Ni bora kuitikia mwito kuliko kujitia moto" na wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia methali "Mtu hakatai wito hukataa aitiwalo." Methali hizi zimetumiwa kwa njia sawa kuashiria mwitiko baada ya kuitwa na mwenzio. Methali nyingine iliyotumiwa kwa njia sawa katika *Wema wa Mwana* na *Sitaki Iwe Siri* ni "Mwana akililia wembe mpe" na "Lakini akalilia wembe, nyembe za walimwengu zilikukuwa zimemkata Yuri na kumjeruhi vibaya." Pia mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia methali "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" huku mwandishi wa *Nimefufuk*a akitumia "Aliogopa kumkunja samaki angali mbichi" na "Udongo upate uli maji." Methali hizi ni sawa ila tu mmoja anajuta kwa kuchelewa huku mwingine akiweka mikakati ya kutimiza jukumu lake.

Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia methali mbili tofauti lakini zenye kubeba dhana moja. Hizi ni "Wakione kilichomfanya kanga kukosa manyoya shingoni" na "Wakione kilichomfanya sangara kuchomwa moto." Methali zote mbili zinatumiwa katika kulipiza maovu au mabaya kwa yule aliyekutenda mabaya. Hali hii pia imetokea katika matumizi ya methali mbili "Hayawi hayawi hatimaye huwa" na "Mambo ni kangaja huenda yakaja" ambazo zimetumiwa kumaanisha mambo ambayo yamesubiriwa sana kutimia hatimaye hutimia.

### 4.1.6 Picha

Cass (1967) na Bakize (2014) wanasema kuwa kama kipengele cha fani, picha ni mbinu ya kupitisha ujumbe kupitia kwa mchoro, vielelezo au picha. Huweza kuwa sura ambayo imepigwa picha kwa kutumia kamera au kuchora kwa kutumia wino. Picha zinapotumiwa, hufanya kitabu kivutie kwa mtoto na kufanya iwe rahisi kwa mtoto kuelewa mambo makuu yaliyomo kitabuni kwa kuwa mtoto husoma maandishi akiyahusisha na michoro hiyo. Picha

pia humsaidia mtoto kushikilia makini yake. Picha zinazotumiwa katika riwaya za watoto zinapaswa kuwavutia ili kuwachochea kusoma. Picha hizi zinapaswa kuwa za rangi zinazong'aa kama vile rangi nyekundu, manjano, kijani kibichi na kadhalika.

Kutokana na maoni haya, ni wazi kuwa picha ni kipengele muhimu cha fani katika fasihi ya watoto. Hii ndiyo sababu waandishi wa riwaya za watoto tulizoteua wametumia picha katika kazi zao. Picha hizi hutumiwa ili kuendeleza maudhui.

Katika sehemu hii tumeonesha idadi ya picha katika kila kitabu na kujadili picha chache ili kuonesha kile ambacho kila picha inajaribu kueleza au kuendeleza. Baadaye katika sehemu ya 4.3 tumeonesha namna picha hizi zimeendeleza maudhui. Jedwali lifuatalo linaorodhesha idadi ya zilizojitokeza katika riwaya mbalimbali tulizochanganua.


**Jedwali 4.6:** ***Picha***

| **Kitabu** | **Idadi ya Picha** |
|---|---|
| *Sitaki Iwe* | 14 |
| *Nimefufuka* | 14 |
| *Wema wa Mwana* | 12 |
| *Kisasi Hapana* | 12 |
| **Jumla** | **52** |

Kutokana na data hii, ni wazi kuwa waandishi hawa wametumia picha kwa kiasi kikubwa kwani wote kwa pamoja wametumia picha 52. Riwaya za *Sitaki Iwe Siri* na *Nimefufuka* zimetumia picha 14 kila moja huku *Wema wa Mwana* na *Kisasi Hapana* zikiwa na 12 kila kimoja. Kiasi hiki kikubwa cha picha katika kila kitabu ni thibitisho tosha kuwa picha ni kipengele muhimu cha fani katika fasihi ya watoto tofauti na fasihi ya watu wazima ambayo huwa na picha chache au hata moja tu kwenye jalada. Wazo hili linaungwa mkono na Bakize (2014) anayesema kuwa matumizi ya picha au michoro huonesha uhalisia wa tukio


linalosimuliwa na maudhui yanayoendelezwa. Anaendelea kusema kuwa michoro na picha husaidia kueleza zaidi kile kinachozungumziwa katika kazi husika kwani huwa na mahusiano ya moja kwa moja na kile anachoeleza mwandishi au mtunzi.

Ilibainika katika utafiti huu kuwa picha zote kwenye riwaya hizi zina rangi zenye kuvutia ili kuchochea hamu ya watoto, pia zinaeleweka kwa urahisi na hivyo ni rahisi kupata maana na maudhui yanayoendelezwa nazo. Rangi na urahisi wa kueleweka pia hufanya watoto hawa kukumbuka mawazo makuu yanayoendelezwa katika kazi hizi.




**Kielelezo 4.1: Picha ya Watoto wa Shule Wakishauriwa na Mwalimu (*Nimefufuka* Uk. 18)**

Pia imebainika kuwa waandishi wote wametumia picha za watoto wenyewe katika hali mbalimbali ili watoto wasomaji wajinasibishe na wahusika hao. Hili litawafanya waone kuwa wao ndio wanaosawiriwa katika vitabu hivikama ilivyo katika Kielelzo 4.2 hapa chini ambapo tunamwona mtoto akicheza na mwanasesere.




**Kilelezo 4.2: Picha ya Mtoto Taabu Akicheza na Mwanasesere (*Nimefufuka* Uk. 13)**

Waandishi wa kazi hizi wamechora watoto wakicheza hasa shuleni au baada ya shule na hili linaungwa mkono na Ngugi (2011) anayesema kuwa watoto hupendelea sana michezo katika maisha yao na kwa hiyo, kazi nyingi zinazowahusu watu hawa lazima zihusishe michezo ili kuwafanya watoto wafurahi na kuendelea kusoma au kusikiliza kazi husika. Kama kazi hizi za watoto hazijali michezo yao, basi umakini wa watoto katika kusikiliza au kuzisoma hupungua. Maoni haya yanadhihirika wazi katika Kielelezo 4.3 ambapo tunaona watoto wakicheza katika uwanja wa shule yao.



**Kielelezo 4.3: Watoto Wakicheza katika Uwanja wa Shule (*Kisasi Hapana* Uk. 24)**

Kigezo kingine cha msingi kilichojitokeza katika uhakiki wetu ni kuwa picha zote ambazo zimetumiwa na waandishi wote wanne, zinaendana na maelezo ya kinathari yaliyomo vitabuni. Kila mara, baada ya kutoa maelezo kwa kina, waandishi hawa huweka picha kwenye ukurasa uleule ili kufanya hoja au wazo kuwa wazi zaidi. Kwa mfano katika *Nimefufuka* kwenye ukurasa wa 7, mwandishi anatueleza kuwa:

> "Waganga na waganguzi walijitahidi kumtibu (Lena). Kuna waliochoma magome, wengine mizizi na majani na wengine wakapiga dua imponye lakini miungu wakakinai" (Uk. 7).



**Kielelezo 4.4: Picha ya Mama ya Lena Akiwa kwa Mganga ( *Nimefufuka* Uk. 7)**

Mbali na maelezo haya, kuna picha kwenye ukurasa huohuo ikionesha waganga wawili na zana zao wakijaribu kutegua kitendawili cha ugonjwa wa Lena huku mama yake ameketi kwa majonzi makubwa akisubiri kitendawili kiteguliwe. Maelezo ya mwandishi yanajalizwa na picha ili habari hizi ziingie watoto akilini kwa urahisi.

Jambo jingine lililobainika katika utafiti huu ni kuwa picha hizi kama kipengele cha fani zimetumiwa sambamba na vipengele vingine vya fani. Hii inamaanisha kuwa picha hujalizana na mbinu nyingine kama tashbihi, misemo, nahau na hata methali. Baada ya mwandishi kutumia mbinu fulani kama methali au tashbihi, picha huwekwa ili kuonesha

wazi funzo la kipengele hicho cha fani. Kwa mfano katika *Nimefufuka* kwenye ukurasa wa 17 kuna msemo:

> " Maisha ni safari ndefu, safari ya kupanda na kushuka." (Uk 17).

Kisha chini yake kuna picha ifuatayo:




**Kielelezo 4.5: Picha ya Mkwea Mlima (*Nimefufuk*a Uk. 17)**

Katika uk. 5 katika *Sitaki Iwe Siri*, Haki anamwambia Musa: "Hujachana nywele aisee. Zinaonekana kama za mwendawazimu.". Ili kusisitiza ujumbe huu, mwandishi ameweka picha kando ya maelezo haya. Kwa njia hii, ujumbe unakuwa wazi zaidi kwa msomaji.




**Kielelezo 4.6: Picha ya Musa, Haki na Ukwa. Musa Anaonekana Akiwa na Nywele Ambazo Hazijachanwa *(Sitaki Iwe Siri* Uk. 5)**

Katika picha hii, ni wazi kuwa Musa hajachana nywele zake na kwa sababu hii, mmoja wa dada zake anaonekana akimfanyia mzaha kwani haonekani vizuri akiwa mwanafunzi. Kwa

njia hii, jambo hili linaweza kusisitizwa na kukumbukwa kwa urahisi na mtoto. Baadaye tumeonesha katika sehemu ya 4.4 jinsi picha hizi zimefanikisha maudhui mbalimbali katika vitabu tulivyochunguza.

**4.2 Maudhui katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto**

Kulingana na Msokile (1992), Wamitila (2002) na Ntarangwi (2004), maudhui ni kile kinachozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maudhui pia yaweza kufafanuliwa kuwa yaliyomo au jumla ya mambo yote yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi yoyote. Maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha dhamira, mtazamo, msimamo, ujumbe, maadili na falsafa. Maudhui hayo yanaibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya kazi husika ya fasihi (Wamitila, 2003).

Njogu na Chimera (1999) nao wanasema kuwa maudhui ni jumla ya mawazo mapana yanayoshirikishwa katika wakati maalum kadri kazi inavyoendelea. Mawazo haya huweza kuwa ya kila aina kutegemea lengo la mwandishi na hadhira anayotaka kuifikia. Kwa sababu hii, mwandishi wa fasihi ya watoto anaposhughulikia maudhui katika kazi yake anapaswa kushughulikia masuala yanayoleta burudani kwa watoto na yanayowaletea manufaa na yenye azma kwao (Cass, 1967). Syambo na Mazrui (1994) wanapendekeza maudhui katika kazi ya fasihi yawe na dhima ya kuonya, kutahadharisha, kukashifu, kuburudisha, kuelimisha, kuipa jamii mwelekeo miongoni mwa mambo mengine. Kwa kuongozwa na maelezo haya, tuliainisha maudhui katika riwaya za fasihi ya watoto tulizochunguza.

Kama tulivyoona katika 1.8.1, Nadharia ya Umuundo, mbali na kusisitiza jinsi vipengele vya kazi ya sanaa vinavyohusiana na kufungamana hadi kuikamilisha kazi hiyo, inazidi kushikilia kuwa sehemu hizo mbalimbali huweza kutenganishwa na kuchunguzwa. Mhimili huu ulituongoza kuchunguza madhumuni ya pili katika utafiti wetu kwa kutambua na

kutathmini maudhui. Tulichukulia kuwa kila maudhui ni kitu kizima kinachojisimamia kwa mujibu wa nadharia hii huku yale mawazo madogomadogo yanayochangia hayo maudhui makuu tuliyachukulia kama maudhui madogo. Maudhui haya tumeyaainisha na kuyaonesha kwenye Jedwali 4.7 kulingana utokeaji wake. Kisha tumeyajadili kwa kuyatolea maelezo kama yalivyotokezwa na waandishi mbalimbali. Baadaye katika 4.3, tulionesha jinsi vipengele mbalimbali vya fani vilivyotumiwa ili kutokeza maudhui hayo. Jedwali 4.7 linaainisha maudhui  yaliyojitokeza katika riwaya mbalimbali tulizochanganua.

**Jedwali 4.7:** ***Maudhui katika Fasihi ya Watoto***

| | *Wema wa Mwana* | *Nimefufuka* | *Kisasi Hapana* | *Sitaki Iwe Siri* |
|---|---|---|---|---|
| Familia | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Elimu | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Nidhamu | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Ushirikiano | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Bidii | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Nafasi ya jinsia ya kike | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| Ugonjwa na Kifo | | ✓ | ✓ | ✓ |
| Umuhimu wa Jina | | ✓ | | |
| Ushawishi | | | ✓ | ✓ |

Kama inavyoonekana katika Jedwali  4.7, tuliweza kuteua maudhui ya familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa, kifo, na ushawishi kwa sababu ndiyo tuliyoona kuwa yanaandamana na malengo ya utafiti na yanahusu watoto. Kutokana na data hii. imebainika kuwa waandishi wote wanne wameangazia maudhui ya familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii na nafasi ya jinsia ya kike. Hata hivyo, maudhui ya ugonjwa na kifo yameangaziwa na waandishi wa *Nimefufuka*,

*Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri*. Maudhui ya umuhimu wa jina yametokezwa na mwandishi wa *Nimefufuka* pekee. Hatimaye maudhui ya ushawishi yameelezwa na waandishi wa *Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri.*

### 4.2.1 Familia

Familia ni muungano kati ya watu wawili au zaidi unaokubaliwa na kuheshimiwa na jamii. Kulingana na Katiba ya Kenya (2010), familia ni muungano wa kiasili na wa kimsingi wa jamii na ambao ni kiungo msingi cha mpangilio wa kijamii na unaotambuliwa na kulindwa kisheria. Muungano huu huwa na lengo la uanzishaji wa kizazi. Mdee na wenzake (2019), wanashikilia maoni haya kwa kutaja familia kuwa jamaa ya watu wanaoishi pamoja yenye baba, mama na watoto na pia inaweza kuhusisha mume, mke, watoto, jamaa, ukoo hata nasaba.

Kulingana na Gatere (2020), kuna aina mbalimbali za familia. Aina ya kwanza ni familia kiini ambayo ni familia ya wazazi na watoto. Familia ya pili ni ile iliyo na wazazi, watoto, babu, nyanya, wajomba na shangazi. Hii anaitaja kuwa familia pana. Aidha, kuna familia ya mzazi mmoja kwa mtoto kuzaliwa nje ya ndoa, kufa kwa mzazi mmoja au kutokana na talaka. Familia ya mwisho ni ya ulezi ambayo ina watoto wanaoishi na wazazi walezi wala sio wazazi wa kibayolojia.

Katika riwaya tulizochunguza katika utafiti huu, kuna miungano mbalimbali ya familia. Familia ya kwanza ni ile ya muungano wa baba, mama na watoto. Muungano huu huitwa familia kiini. Kwa mfano, katika *Wema wa Mwana* kuna familia inayojumuisha Mama na Baba Juma ambao wamezaa Juma na watoto wengine ambao tunaambiwa wamefanikiwa kielimu kuliko Juma. Katika familia hii, Baba na Mama Juma wanajaribu kumrekebisha Juma ili awe na nidhamu na kufanya bidii shuleni ili naye afanikiwe kama hao wanao wengine. Familia kiini nyingine inahusisha Baba Ngoyoni, Mama Ngoyoni, Ngoyoni na

watoto wengine ambao hawakutajwa. Aina ya pili ni familia pana. Katika *Kisasi Hapana* kuna familia kama hii ambapo kuna Baba Kido, Mama Kido, nyanya ambaye ni mama ya Baba ya Kido, Kido na Salama. Washiriki wa familia hii hawaishi pamoja baada ya baba ya Kido kufungwa jela akiwa kazini mjini. Kwa sababu hii, Kido anatunzwa na mama yake na nyanyake. Katika riwaya ya *Nimefufuka* kuna familia ya Mama na Baba Lena ambao ni wazazi wa Chaurembo na Jose. Washiriki wengine ni kama vile shangazi ya Lena, Chaurembo, ambaye ana mume wake na Musa ambaye ni mpwa wa Lena.

Aina nyingine ya familia ni ile ya ulezi inayohusisha nyanya na wajukuu pekee. Hili linasababishwa na kifo cha wahusika wengine. Katika *Sitaki Iwe Siri* kuna familia kama hii ambapo wahusika wake ni Mwalongo na wajukuu wake Musa, Haki na Ukwa. Mwalongo alikuwa na mtoto wake Yusufu na mkaza mwanawe Honorota. Hawa wawili walikufa na kumwachia Mwalongo jukumu la malezi. Ametimiza jukumu hili kwa bidii na mapenzi licha ya umri wake mkubwa.

Kuna familia mbili ambazo baada ya muda zinasambaratishwa na majanga na kifo na hivyo kupunguza washiriki wake. Katika *Sitaki Iwe Siri*, Yusufu na Honorota wanakufa na jukumu hili la ulezi linamwangukia Nyanya Mwalongo anayelazimika kutunza wajukuu wake Musa, Haki na Ukwa. Katika *Kisasi Hapana* nyanya ya Kido ambaye ni mama ya Mkulu anauawa na watu wa familia ya dereva wa Mkuu wa Wilaya na hivyo kupunguza washiriki wa familia hii.

Kipengele kingine muhimu katika swala la familia ni pale ambapo mshiriki mmoja au zaidi haishi pamoja na familia yake. Hili linatokana na hali kuwa mshiriki huyu anaweza kuwa anafanya kazi mbali na nyumbani, ameolewa, ni mtoro au kufungwa jela. Kwa mfano, katika *Kisasi Hapana*, Bwana Mkulu alikuwa anafanya kazi mjini na baadaye tunampata kama amefungwa jela. Katika *Wema wa Mwana*, Lena anatoroka nyumbani ili kuponda raha

Mombasa lakini baadaye anakufa. Hali hizi zinafanya washiriki wengine kuwa na majonzi makuu kwa kukosa wenzao. Pia, inakuwa vigumu kutimiza mahitaji ya msingi kama chakula, nidhamu na mapenzi katika hali kama hii.

Katika utafiti huu, imebainika wazi kuwa lengo la muungano wa familia ni kuandaa mahitaji ya kimwili kama chakula, mavazi, ulinzi, nidhamu, mapenzi, elimu na kuliwazana kunapokuwa na mikasa. Katika *Wema wa Mwana*, jukumu hili linatekelezwa na baba na mama Juma. Mama Juma yuko jikoni akipikia familia huku baba Juma akionekana kushughulikia nidhamu na elimu ya Juma kwa kumshauri na kumuasa. Katika *Kisasi Hapana*, kazi zote zinazohusiana na ulezi zinafanywa na mama na nyanya ya Kido. Nyanya anamtambia Kido hadithi na kumpikia. Kido anapokuwa mgonjwa, mamake na nyanyake wanashirikiana kumtunza. Katika *Sitaki Iwe Siri*, majukumu haya yanaangukia Mwalongo ambaye anatunza wajukuu wake watatu, Musa, Haki na Ukwa kwa bidii baada ya wao kufiwa na wazazi wao Yusufu na Honorota.

### 4.2.2 Elimu

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni, maishani na kadhalika. Elimu inahusu kufundisha, kujifunza ujuzi na tajriba. Pia inahusu kusaidia watu wengine wajifunze namna ya kufanya mambo na kuwategemeza kufikiria kuhusu kile wanachojifunza. Ndalu na wenzake (2019), wanafafanua elimu kuwa mafunzo yatolewayo shuleni, vyuoni, maishani na kwingineko. Kwa hiyo, elimu ni mchakato wa kusaidia mtu kupata ujuzi, hekima, maadili, imani, mazoea, kusababu nakufanya maamuzi. Kwa njia hii, elimu hutayarisha mtu kwa maisha ya utu uzima. Wanaendelea kutaja kuwa njia za kupokea elimu hii ni kusimulia hadithi, majadiliano, kufundisha, kutazama, kufanya mambo au shughuli fulani, kujizoeza na kufanya utafiti. Matokeo ya elimu ni ya polepole na huleta mabadiliko chanya katika maisha na tabia ya mtu. Elimu pia husaidia mtu kutambua jema na baya maishani.

Kwa mujibu wa maelezo haya, inabainika kuwa elimu huhusisha kuenda shuleni kuanzia chekechea hadi chuo, michezo shuleni, kutazama jinsi wengine wanavyofanya mambo, majadiliano na wengine, kufanya utafiti, kujaribu mambo na hata mashauri. Elimu hii pia inahusisha tajriba apatazo mtu kutokana na anayotazama, kusikia au kupitia maishani.

Katika utafiti huu, tumebaini elimu kuwili. Kuna elimu rasmi inayohusisha kusoma vitabu shuleni. Nyingine ni elimu isiyo rasmi inayopatikana maishani kupitia kwa mashauri na tajriba apatazo mtu kutokana na anayopitia katika shughuli zake za kila siku. Elimu rasmi pia ina pembe mbili. Kwanza ni ya kusoma vitabu na kutangamana kwa wanafunzi na walimu darasani. Kisha kuna ile ambayo inahusisha shughuli za ziada kama vile michezo. Katika *Sitaki Iwe Siri*, elimu rasmi imeendelezwa kupitia kwa wahusika Musa, Haki na Ukwa ambao wameoneshwa wakienda shuleni kupata elimu. Huko shuleni kuna walimu wenye bidii kama Bwana Ochuka ambao wanafunza watoto hawa. Hata inadhihirika kuwa walimu wanatenga wakati kusaidia watoto na elimu yao kibinafsi. Kwa njia hii, wanasaidiwa kutambua kuwa bidii ni jambo la msingi maishani. Kwa mfano, Musa anasaidiwa kuandika insha katika mashindano ya kitaifa kuhusu ugonjwa wa Ukimwi na kushinda tuzo. Katika *Wema wa Mwana*, wazazi wa Ngoyoni wanampeleka shuleni Masomoni. Huko shuleni, mwalimu mkuu na walimu wengine wanafaulu kumrekebisha Ngoyoni kitabia. Matokeo mazuri anayopata Ngoyoni yanawavutia wazazi wa Juma ambao wanaazimia kumpeleka kuko huko katika shule ya Masomoni ili naye apate nidhamu kama ya Ngoyoni.

Sehemu ya pili ya elimu rasmi inahusu shughuli za ziada shuleni mbali na masomo ya darasa. Katika *Kisasi Hapana*, Ken Walibora anamchora Kido kuwa anaenda shuleni ingawa anapenda kucheza kandanda kuliko masomo kwani anataka kuwa mchezaji wa mpira maarufu ikiwezekana achezee timu za kimataifa. Dadake Kido kwa upande wake

alikuwa mwerevu sana shuleni mbali na kuwa bingwa katika riadha na soka ya wanawake. Kule shuleni, wanafunzi pia wanajihusisha na michezo kama kandanda na kukimbia na wengine hata wanacheza hadi kiwango cha kitaifa.

Kipengele kingine muhimu cha elimu ni kile kinachohusu elimu ya maisha kupitia kushauriwa ili kuadilishwa au kusaidiwa kupata sifa fulani maishani. Katika *Wema wa Mwana*, wazazi wa Juma wanamuasa na kumshauri pamoja wakiwa nyumbani, wanamkanya kuhusu tabia yake mbaya ya kuiba chakula jikoni. Wazazi wa Ngoyoni kwa upande mwingine wameshindwa kumrekebisha mwanao na anapelekwa katika shule ya Msingi ya Masomoni ili wasaidiwe katika kumrekebisha mwana huyu kitabia. Katika *Nimefufuka*, Chaurembo anapata elimu ya maisha kupitia kwa mashauri ya shangazi yake. Shangazi anamshauri avae vizuri, ajipende na akubali kufungua moyo wake kupendwa na mwanamume. Matokeo ni kuwa anavaa vizuri, anatunza wengine vizuri, anapata kazi na hata mchumba anayempenda kwa dhati na wanapanga kufunga ndoa.

Aina nyingine ya elimu isiyo rasmi ni ile aipatayo mtu kupitia tajriba apatazo maishani. Inahusisha mtu kupata shida kwa sababu ya maamuzi yake mabaya na kisha anapata funzo. Elimu kama hii ya maisha inapatikana katika *Nimefufuka* ambapo Lena anaacha shule na kukimbilia Mombasa na kuishi maisha ya anasa. Anapata elimu ya dunia kupitia matatizo anayokabiliana nayo anapojiingiza katika mapenzi na wanaume mbalimbali na anakufa kabla ya kurekebisha mwelekeo wake maishani. Katika *Sitaki Iwe Siri*, dereva wa matatu na utingo wake wamejifunza nidhamu kupitia elimu ya maisha kwa kufanya kazi yao kwa muda na hivyo wanatekeleza kazi hiyo kwa weledi mkubwa.

### 4.2.3 Nidhamu

Kulingana na Ndalu na wenzake (2019), nidhamu ni hali ya kufanya jambo kwa mpangilio maalum. Maana nyingine ni mwenendo wa tabia nzuri au hulka njema. Kisawe chake ni

adabu ambayo ni kufanya matendo ya heshima, sifa njema au staha. Mdee na wenzake (2019), wanaongeza kuwa nidhamu ni tabia nzuri inayolingana na maadili. Pia inaweza kumaanisha adabu, staha au heshima. Inaweza pia kumaanisha uendelezaji mzuri wa jambo. Katika sehemu hii tumeangazia pande mbili za nidhamu. Utafiti huu umeangazia tabia nzuri za wahusika na mpangilio mwema wa utendakazi wao. Pia, umeangazia wale wanaoonesha ukosefu wa nidhamu kitabia na katika utendakazi wao.

Kuna wahusika ambao wamedhihirisha nidhamu njema na hili linawafanya kufanikiwa maishani na kuheshimiwa katika jamii. Kwa mfano, katika *Sitaki Iwe Siri*, Musa anachorwa na mwandishi kama mtoto mwenye nidhamu ya hali ya juu kwa jinsi anavyotenda kwa heshima akiwa nyumbani. Anawaheshimu nyanyake na dada zake kwa kuwasaidia kwa bidii katika shughuli zao pale nyumbani. Musa akiwa shuleni anaonesha wanafunzi wenzake heshima wanapocheza pamoja. Anaomba walimu wake msaada kwa heshima nao pia wanaishia kumpenda na kumsaidia kwa njia mbalimbali. Hii ni ishara ya nidhamu. Haki na Ukwa wana nidhamu kwa jinsi wanavyoonesha heshima kwa watu wote pamoja na ndugu yao mkubwa, Musa. Wauguzi na daktari wanaonesha nidhamu kubwa kazini hasa kutokana na jinsi wanavyoshughulikia Musa na ndugu zake kwa kuchukua muda wao kuwasikiliza na kuwahudumia. Dereva na utingo wa matatu inayowabeba akina Musa pia wanadhihirisha nidhamu wakiwa kazini kwa kuendesha gari kwa utaratibu huku utingo akiwarai abiria kuingia katika gari kwa heshima na kuwawekea mizigo yao.

Riwaya ya *Kisasi Hapana* pia inamsawiri Kido kuwa ni mwenye nidhamu na anawaheshimu wazazi wake na hili linadhihirika kwa jinsi anavyowatendea kwa kutii maagizo yao na kushirikiana nao. Anamheshimu na kumpenda nyanya yake na wanakaa pamoja kwa vipindi virefu wakila na kuhadithiana ngano. Mhusika Chaurembo katika *Nimefufuka* pia anaonesha nidhamu ya hali ya juu anapowajibika kutunza mpwa wake, mama yake, baba yake na hata

ndugu yake Jose. Nidhamu ya Chaurembo inamfanya kupendwa na shangazi yake ambaye anamsaidia kwa njia nyingi. Kupitia kwa mashauri ya shangazi yake Chaurembo, anajitunza vizuri na kujiheshimu. Hatimaye anapata kazi na mchumba.

Kwa upande mwingine, kuna wahusika ambao wanakosa kuonesha nidhamu kupitia kwa matendo yao. Kwa mfano, katika *Wema wa Mwana* Juma anasawiriwa kuwa mtovu wa nidhamu kwa kuwa anaiba vyakula jikoni. Wakati mmoja Juma anaiba na kutia nyama moto mfukoni. Matokeo ni kuwa anachomeka vibaya. Pia, Juma hatii bidii shuleni na hili linadhihirika kupitia matokeo yake mabaya katika masomo ya Hisabati na Sayansi Kimu. Babake anagundua kuwa sababu yake ya kufeli ni kutumia muda wake mwingi jikoni badala ya kusoma. Ngoyoni pia ana utovu wa nidhamu kama anavyoripoti baba yake kuwa wameshindwa kumrekebisha. Wazazi wake wanaamua kumpeleka katika shule ya kurekebishia tabia. Ngoyoni hatimaye anakuwa na tabia njema ambayo hata watoto wengine kama Juma wanatamani kuiga.

Katika *Nimefufuka*, Lena anajipata matatani kwa kukosa nidhamu kwani anajiingiza katika mapenzi kiholela na wanaume. Hili ni kinyume cha maadili ya jamii na ndiyo sababu mama yake anajaribu kumtafuta ili kumkomboa kutokana na tabia hii lakini anashindwa. Matokeo ni kuwa anapata ugonjwa wa ajabu na kuishia katika kifo cha mapema. Katika *Kisasi Hapana*, dereva wa Mkuu wa Wilaya anakosa nidhamu kwa kumchapa nyanya ya Kido. Baadaye dereva huyu anapopata ajali ya barabarani, anaamini imesababishwa na nyanya ya Kido.

### 4.2.4 Ushirikiano

Ushirikiano ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli. Neno hili ushirikiano linalotokana na kitenzi shiriki. Kulingana na Ndalu na wenzake (2019), "shiriki" ni kufanya mambo pamoja na wengine. Kitenzi hiki hutumiwa kuunda nomino shirika linalomaanisha kumiliki pamoja. Mdee na wenzake (2019), wanaongezea kuwa shirika ni kitu kinachomilikiwa na watu wawili au zaidi huku shirikiana likimaanisha

jumuika kufanya jambo na mtu au watu wengine. Pia linaweza kumaanisha tangamana au fungamana. Kwa kuongozwa na kauli hizi tumegawa ushirikiano katika nafasi tatu; ushirikiano nyumbani, ushirikiano shuleni na ushirikiano kazini.

*Wema wa Mwana* inasawiri ushirikiano nyumbani pale ambapo Wazazi wa Juma wanashirikiana kumrekebisha Juma kitabia kwa kumshauri. Baba ya Juma ndiye wa kwanza kutoa nasaha yake kisha mamake anapogundua kuwa amesononeka baada ya kushauriwa na babake naye pia anatoa nasaha zake na kumsihi atie bidii ili asiwatie aibu. Wazazi wa Ngoyoni wanaamua kwa pamoja kumpeleka Ngoyoni katika shule ya kurekebisha tabia na hii ni ishara ya ushirikiano. Katika *Nimefufuka*, Musa na Mama Lena wanashirikiana kumtafuta Lena baada ya kukimbia kutoka nyumbani. Wanafanya hivi ili kumtoa kutoka lindi la anasa na kumrejesha nyumbani. Hata hivyo, juhudi zao hazikufua dafu kwani Lena anakataa katakata kurudi nyumbani. Wanakijiji pia wanashirikiana kuchangisha pesa na kufanya mipango ya kumleta Lena nyumbani anapokufa badala ya kuzikwa mbali na watu wake wa ukoo. Mama ya Lena anapowehuka wanajamii wanashirikiana kumuasa ili asiwe na mawazo kupita kiasi na matokeo ni kuwa anaanza kuboresha maisha yake.

Kwenye riwaya ya *Kisasi Hapana*, ushirikiano nyumbani unasawiriwa pale ambapo mama na nyanya ya Kido wanashirikiana katika kutunza wanao na wajukuu. Wanafanya bidii kumpeleka Kido hospitalini anapokuwa mgonjwa na hili wanalitimiza licha ya changamoto nyingi wanazopitia. Jirani yao pia anashirikiana nao kwa kuwasaidia kumtunza Kido anapokuwa mgonjwa kwa kumbeba kwa baiskeli hadi nyumbani na kukusanya majirani wamchangie pesa ili kumnunulia dawa. Mke wa jirani kwa upande wake anasaidia kwa kumwosha Kido hata anapojitapikia. Katika *Sitaki Iwe Siri*, ushirikiano nyumbani unaoneshwa kwa Mwalongo kushirikiana na wajukuu wake ili kuandaa mahitaji ya msingi.

Pia, wajukuu watatu wa Mwalongo wanashirikiana katika mambo yote wanayofanya nyumbani kama kuchunga mifugo, kupika na hata kuenda matembezi pamoja.

Ushirikiano shuleni unaonekana kupitia kwa wanafunzi wanaosoma na kucheza pamoja na pia kati ya walimu na wanafunzi. Katika *Wema wa Mwana*, Walimu wa Ngoyoni katika shule ya Masomoni wanashirikiana ili kumsaidia Ngoyoni pamoja na wanafunzi wengine waboreshe tabia zao na kufuzu katika masomo na maisha. Katika *Kisasi Hapana*, kuna roho ya ushirikiano shuleni kati ya wanafunzi wenzi wa Kido wanapocheza pamoja bila kuzozana. Ile timu ya wasichana wanaocheza mpira wa miguu wanashirikiana kucheza hadi kiwango cha kitaifa.

Katika kuendeleza kipengele cha ushirikiano kazini, riwaya *Sitaki Iwe Siri* inatuchorea uhusiano wa kikazi kati ya utingo na dereva wa matwana inayobeba Musa na dada zake kuelekea hospitali ya Nyagacho kufanya utafiti. Utingo anatimiza wajibu wake wa kuwarai abiria kuingia kwenye gari, kupakia mizigo na kisha kukusanya nauli. Dereva kwa upande wake tunaambiwa anatimiza sehemu yake kwa kuendesha gari huku watu wote wametulia garini. Baadaye Daktari Ataya na manesi wanashirikiana kutunza wagonjwa na kuwashughulikia Musa na dada zake wanapoenda kufanya utafiti kuhusu Ukimwi.

### 4.2.5 Bidii

Bidii ni jitihada katika kutekeleza jambo fulani. Kulingana na Ndalu na wenzake (2019), bidii ni kuwa na wajibu wa kufanya jambo fulani. Pia humaanisha moyo ama ari ya utendaji wa kazi, juhudi au hima. Katika kutathmini maudhui ya bidii, utafiti huu umeangazia bidii ya wazazi katika familia, bidii inayooneshwa na watoto na walimu shuleni na hatimaye bidii inayodhihirika kazini.

Bidii nyumbani inadhihirishwa kuwili kupitia kwa wazazi kutia bidii ili kutekeleza majukumu yao na pia watoto wanapotimiza sehemu yao pale nyumbani. Katika kuonesha jinsi wazazi wanavyotia bidii nyumbani, *Wema wa Mwana* inasawiri hali ambapo Juma anakosa kutia bidii shuleni. Anashindwa katika masomo ya Sayansi Kimu na Hisabati. Babake anagundua kuwa sababu yake ya kufeli ni kutumia muda wake mwingi jikoni badala ya kusoma. Kwa sababu hii, anashirikiana na mke wake kwa bidii kumsaidia Juma. Wanataka Juma aone umuhimu wa kufanya bidii shuleni na nyumbani kwa kuzamia vitabu vyake ili aboreshe gredi zake shuleni. Wazazi wa Ngoyoni wanatia bidii kumsaidia mwanao awe na tabia nzuri. Wanaposhindwa wanampeleka katika shule ya kurekebisha tabia.

Bidii ya wazazi nyumbani inadhihirishwa katika *Nimefufuka* pale ambapo Mama ya Lena, kwa msaada wa Musa, anafanya bidii ili kumtafuta bintiye ambaye amepotelea Mwambao katika anasa. Hata hivyo, licha ya bidii yake ya mchwa hakuweza hata siku moja kufaulu kuongea na mwanawe. Wakati mmoja alipompata alidinda kuzungumza naye na kumwona kama takataka. Chaurembo anafanya bidii kumtunza Shujaa, mtoto wa Lena pamoja na wazazi wake hasa baada ya kutoka kwa mumewe na kurudi kwao. Ni yeye pia anayemtunza ndugu yake Jose baada ya kuwa mlevi kiasi cha kushindwa kujitunza mwenyewe. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* anaeleza kuwa Nyanya Mwalongo anafanya bidii kuwatunza wajukuu wake baada ya wazazi wao kufa kutokana na ugonjwa wa ajabu.

Sehemu nyingine ambapo wahusika wameonesha bidii ni shuleni. Ken Walibora katika *Kisasi Hapan*a anaangazia bidii shuleni kwa kumsawiri Kido akiwa anafanya bidii katika michezo kuliko masomo. Dada ya Kido kwa upande wake anafanya bidii masomoni na michezoni na hili linamfanya afuzu kucheza hadi kiwango cha kitaifa mbali na kuwa namba moja darasani. Tabia hii ya kupenda michezo pia inamfanya kufaulu kutoroka kutoka kwa mikono ya wale waliomteka nyara. Katika *Sitaki Iwe Siri,* bidii shuleni inaangaziwa kupitia

kwa Musa ambaye anafanya bidii kuandika insha kwa ajili ya mashindano ya kitaifa kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Musa, Haki na Ukwa wanatia bidii kwenda shuleni kila siku licha ya umbali wa shule hii kuwa kilomita nane kutoka nyumbani kwao. Walimu wanafanya bidii shuleni kwa kusomesha wanafunzi, kuwatia nidhamu na kuhakikisha kuwa wanadumisha unadhifu. Hili linaoneshwa kupitia kwa Ochuka ambaye ni mwalimu katika shule anakosomea Musa. Anatimiza hili wakiwa gwarideni na darasani. Ni yeye pia anayefanya bidii kumsaidia na kumwelekeza Musa kuandika insha ambayo hatimaye inapata ushindi kitaifa. Katika *Wema wa Mwana*, walimu wa Ngoyoni wanatia bidii kusaidia Ngoyoni na wanafunzi wengine. Wanapata matokeo mazuri kwani Ngoyoni anarekebisha tabia yake. Hata wanasema wakiwa na hakika kuwa watafanya yote wawezayo ili kuwasaidia watoto wote katika shule hii ya Masomoni.

### 4.2.6 Nafasi ya Jinsia ya Kike

Katika utafiti huu imedhihirika kuwa jinsia ya kike imesawiriwa kuwa inapenda elimu kwa dhati. Katika *Wema wa Mwana*, mama ya Juma anaunga mkono mume wake kumshauri Juma kupenda masomo na kuwa na tabia njema. Mama ya Ngoyoni naye anampokea mwanawe kwa shangwe anapotoka shuleni kumaanisha aliunga mkono uamuzi wa kumpeleka huko. Mwalimu wa darasa la Ngoyoni kule shuleni Masomoni ni mwanamke. Pia, kuna wanafunzi wa kike kule shuleni kwa akina Ngoyoni. Jambo hili ni la maana kwa mtoto wa jinsia ya kike kwani ni kitia moyo kwao kuwa hata wao wanaweza kufaulu kama hao wanawake wengine. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* anatuonesha kuwa kuna wanawake ambao ni wauguzi na wengine kuwa walimu kuonesha kuwa wamepata elimu kwa kiwango fulani. Mbali na Haki na Ukwa, kuna wasichana wengine katika shule hii ambao wanatia bidii kupata elimu. Mkutubi katika Shule ya Msingi ya Hekima ambaye ni mwanamke

amesoma ili kustahili kazi hii. Hii ni ithibati kuwa wanawake wamezinduka na kuikumbatia elimu.

Mwanamke pia amechorwa kuwa mwenye bidii na mapenzi. Katika *Nimefufuka*, Chaurembo amechorwa akiwa anawatunza wazazi wake na Shujaa mtoto wa Lena kwa bidii na mapenzi. Mama Lena anaonesha mapenzi kwa kumtafuta binti yake aliyepotelea mjini katika anasa. Anaposhindwa kumpata anakuwa mwendawazimu kuashiria kutamauka kwake. Hii ni ishara ya mapenzi ya dhati aliyonayo mama huyu kwa mwanawe. Katika *Kisasi Hapana*, nafasi hii inaendelezwa kupitia Mama ya Kido na nyanyake kumtunza Kido wakati babake alikuwa amefungwa na wanafanya hili kwa hali na mali hata Kido anapokuwa mgonjwa. Pia, dada yake Kido anafuzu katika michezo na masomoni. Wasichana wanaosoma katika shule ya akina Kido wanafuzu katika michezo hadi viwango vya kitaifa. Hatimaye katika *Sitaki Iwe Siri*, Mwalongo anadhihirisha kuwa ni mwanamke mwenye mapenzi na mlezi bora wa wana wake na baadaye analea wajukuu wake vizuri. Hii ni ishara tosha kuwa yeye ni mwenye bidii na mwingi wa mapenzi.

Aidha, mwanamke amesawiriwa kama mshauri mwema. Kwa mfano, riwaya ya *Nimefufuka* inamsawiri Shangazi ya Lena kama mshauri mwema kwani baada ya kumshauri Chaurembo, anabadili mwelekeo wake maishani na afya yake kuimarika.

Kwa upande mwingine, mwanamke amechorwa kama chombo cha kuzaa. Hili linadhihirika katika *Nimefufuka* ambapo Chaurembo anachukiwa na mavyaa wake kwa kukosa kuzaa. Hatimaye, anatalikiwa na mumewe. Hii ni ishara kuwa jamii hii inamthamini tu mwanamke ikiwa atazaa. Hatimaye, mwanamke amesawiriwa kwa njia hasi anapoangaliwa kama mpenda anasa na kuwa chombo cha kutumbuiza wanaume. Katika kuendeleza wazo hili, riwaya ya *Nimefufuka* inamchora Lena akiwatumbuiza wanaume kule Mwambao alipokimbilia baada ya kuacha shule. Huu bila shaka ni mfano mbaya kwa mtoto msichana.

Hili ni thibitisho kwamba kuna wanawake ambao ni mifano mizuri ya kuigwa na wasichana na vilevile wapo ambao ni mifano mibaya wanaopaswa kuepukwa.

### 4.2.7 Umuhimu wa Jina

TUKI (2013) inafafanua jina kuwa neno la kumtaja mtu au kitu. Mtu hupewa jina anapozaliwa na mhusika hujinasibisha na jina lake. Imedhihirika kuwa jina linaathiri maisha ya baadaye ya mtu. Katika kuonesha maudhui ya umuhimu wa jina, mwandishi wa *Nimefufuka* ametuchorea mhusika aliyepewa jina Sikitu alipozaliwa. Mhusika huyu anapoolewa anashindwa kupata mtoto na kuamua kurudi kwao. Hili linamfanya kuvunjika moyo na kuhisi kuwa hafai. Shangazi yake anapendekeza abadilishiwe jina na kuwa Chaurembo na matokeo ya mabadiliko haya ni kuwa mhusika huyu anajiheshimu zaidi, kuvaa nguo zinazomsetiri na kujipenda. Hili linachangia kuimarika kwa afya yake na baadaye hata anapata kazi na kuolewa.

Mtoto wa Lena aliitwa Taabu. Taabu anakuwa na afya mbaya na kujikojolea ovyo kutokana na ugonjwa unaomkabili. Shangazi ya Sikitu anapendekeza naye pia abadilishiwe jina na kuwa Shujaa badala ya Taabu na baada ya badiliko hili afya yake inaboreka na kuacha kuwa kikojozi. Hata mji wa akina Chaurembo unaitwa Mjibalaa na hivyo hauna maendeleo na Chaurembo anatamani ubadilishiwe jina uitwe Mjiadilifu pengine hili pia litabadilisha mwelekeo wa watu na kuwaletea maendeleo.

### 4.2.8 Ugonjwa na Kifo

Kulingana na TUKI (2013), ugonjwa ni kitu kinachosababisha mtu au mnyama kuwa katika afya mbaya. Kifo ni tukio au tendo la kufikia mwisho wa uhai. Maudhui ya ugonjwa na kifo yanajitokeza katika kazi zote nne tulizotafiti. Katika *Nimefufuka*, tunashuhudia kifo cha Lena ambaye aliugua ugonjwa wa ajabu, muda mfupi baada ya kujifungua mtoto Taabu. Hata hivyo, Musa, Taabu, Mama Sikitu na Baba Sikitu wanaugua na kunusurika kifo. Musa

anaugua ugonjwa unaotokana na utumiaji wa dawa za kulevya. Hili linamfanya Musa kuwa mchafu na kukosa kujitunza kiafya. Mtoto wa Lena kwa jina Taabu kwa upande wake anaugua ugonjwa usiojulikana na ni kama alirithi ugonjwa huu kutoka kwa mamake ambaye pia alikonda hadi akafa. Mama mzazi wa Chaurembo ana mahoka kutokana na kutamauka maishani kwa mambo kutomwendea vizuri hasa kwa kifo cha Lena, kuharibikiwa kwa ndoa ya Sikitu na tabia mbaya ya mtoto wake Jose. Katika *Kisasi Hapana,* Nyanya yake Kido anakufa bila kuugua. Mhusika huyu anakufa baada ya kushambuliwa na watu wa ukoo wa dereva wa Mkuu wa Wilaya. Kido naye anakuwa mgonjwa sana na kupelekwa hospitalini kwa msaada wa mamake na nyanyake na hatimaye anapona. Baadaye Kido anavunjika mguu wakiwa katika mchezo wa kandanda na hili linamzuia kuenda shule na kucheza mpira.

Katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri*, maudhui ya ugonjwa na kifo yanaoneshwa kupitia kwa vifo vya wahusika wawili, Yusufu na mke wake Honorota ambao wanakufa kwa Ukimwi baada ya kuugua kwa muda na kukondeana. Jambo hili linamsononesha mama yao Mwalongo sana. Baada ya kifo chao wanaacha Musa, Haki na Ukwa wakiwa mayatima na wanatunzwa na nyanya yao Mwalongo ambaye naye anaonekana kuwa mnyonge kutokana na uzito wa moyo. Kwa kuwa nyanya Mwalongo ni mjane na ana watoto, kuna uwezekano kuwa mume wake alikufa. Aidha, mhusika Yuri katika hadithi aliyotunga Musa anakufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi.

### 4.2.9 Ushawishi

Neno ushawishi limetokana na kitenzi shawishi. Kulingana na Ndalu (2019), neno shawishi lina maana ya kuambia mtu jambo ili akubali kufuata maelezo ama avutike kutenda jambo fulani. Katika riwaya tulizotafiti, kuna ushawishi shuleni na katika maisha kwa ujumla. Kwa mfano, katika *Kisasi Hapana*, Baba ya Kido anamshawishi Kido kutia bidii masomoni kwa

sababu mwana huyu alipenda sana kucheza kuliko kusoma. Anamshauri kuwa si vibaya kutia fora katika michezo. Anamwonesha umuhimu wa kushiriki katika nyanja zote mbili. Kuhusu maisha, babake anamshawishi kuwa asilipize kisasi kwa wale waliowatendea vibaya kwani si jukumu lake.

Katika *Sitaki Iwe Siri*, tunamwona mwalimu mkuu anamshawishi Musa kushiriki katika shindano la kuandika insha juu ya Ukimwi. Musa anakubali nasaha hii na hatimaye anaibuka kuwa mshindi. Mkutubi pia anamshawishi Musa kutafuta habari zaidi kutoka maktaba mjini. Habari hii inamfaidi Musa katika uandishi wake na hatimaye kuibuka mshindi katika taifa zima. Ushawishi wa maisha unapatikana katika *Nimefufuka* wakati shangazi anamshawishi Sikitu kujiamini. Anamwambia abadilishe jina na kuvaa vizuri. Anafanya hivyo na hatimaye anapata mchumba na kazi.

Kwa kuhitimisha basi imekuwa wazi kuwa waandishi wote tuliotafiti kazi zao wameangazia maudhui yanayoweza kuwagusa watoto na maisha yao ya kila siku. Tumeangazia maudhui kama elimu, familia, nidhamu, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ushawishi, ugonjwa na kifo. Katika sehemu ya 4.3 tunaonyesha jinsi vipengele mbalimbali vya fani vimefumwa kwa ustadi ili kufanikisha ujitokezaji wa maudhui haya ambayo tumejadili.

### 4.3 Jinsi Fani Inavyoendeleza Maudhui katika Fasihi ya Watoto

Katika utafiti huu, ilibainika wazi katika sehemu ya 4.2 kuwa vitabu tulivyotafiti vimeangazia maudhui mbalimbali yanayolenga watoto. Maudhui hayo ni familia, nidhamu, elimu, nafasi ya jinsia ya kike, bidii, ushirikiano, umuhimu wa jina, ushawishi, ugonjwa na kifo. Maudhui haya yamesukwa kwa njia mbalimbali. Pia, katika 4.1, imebainika kuwa vitabu tulivyotafiti vina vipengele vya fani kama tashbihi, misemo, nahau, picha, methali na taswira. Vipengele hivi haviwezi kujisimamia katika hali halisi. Lazima maudhui yachanganuliwe katika muktadha wa fani na fani pia lazima zihakikiwe katika muktadha

wa maudhui. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu tulitenganisha vipengele hivi viwili ili kuvichunguza kwa undani.

Mhimili wa pili wa nadharia ya Umuundo unashikilia kuwa katika kupata maana, lazima kuwe na uhusiano wa kipembe tatu, yaani dhana, alama na kitajwa. Uhusiano huu pia unadhihirika katika kazi ya fasihi ambapo kuna kitengo cha sanaa chenye vipengele kama vile maudhui, ploti, wahusika, muktadha na fani za lugha. Hakuna kipengele kati ya hivi kitakachoelezwa katika upekee wake bali lazima kielezwe kwa kuzingatia kuwepo kwa jukumu la vipengele vingine. Hii ni kwa sababu vipengele vinavyounda kazi hushirikiana, kujengana na kukamilishana ili kuwa kitu kizima. Katika utafiti huu, tumetumia mhimili huu kuonesha kuwa maudhui na fani ni dhana zinazotegemeana na kukamilishana. Pia ushirikiano uliopo baina ya vipengele hivi na unaovikamilisha unaweza kuchunguzwa. Tuliongozwa na mihimili huu kutathmini madhumuni ya tatu kwa kuchanganua na kuchunguza ni vipi msanii husuka vipengele vya fani yake ili kueleza na kuweka wazi maudhui yake katika fasihi ya watoto.

### 4.3.1 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Familia katika Fasihi ya Watoto

Katika utafiti wetu tulibaini kuwa maudhui ya familia yameendelezwa na vipengele vya fani kama tashbihi, picha, methali, taswira, nahau na misemo. Tumeonyesha namna uendelezaji huu umetokea katika kila kitabu.

#### 4.3.1.1 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Familia

Tashbihi zimetumiwa na waandishi wote wanne katika kuendeleza maudhui ya familia. Riwaya ya *Kisasi Hapana* imetumia tashbihi tano kuendeleza maudhui ya familia. Kwa mfano:

> "Humwona (mama) kama, sijui niseme, mtoto mdogo au aliyefiwa. Kawaida kila nikimwangalia mama, machozi humtoka njia mbilimbili. Machozi humdondoka

> machoni kama chemchemi ya maji. Ilimradi tangu ulipoondoka nyumba yetu imefunikwa wingu la huzuni. Majonzi. Simanzi tele" (Uk. 1).

Katika tashbihi "humwona mama kama aliyefiwa", Ken Walibora ameangazia maudhui ya familia kwa kutuchorea familia ya Andrea Mukulu ambaye alikuwa anafanya kazi ya ubawabu mjini. Mukulu aliishia kufungwa jela akiwaacha washiriki wa familia wengine kama mama yake, mke wake na watoto wakiteswa na majonzi ya kumkosa mpenzi wao. Mtoto wake Kido Mukulu, katika barua yake kwa babake anatumia tashbihi hii kuonesha majonzi anayopitia mamake ambaye ni mke wa Mukulu. Mama huyu anashinda akilia kwa kumkosa mumewe. Kwa kutumia tashbihi "machozi humdondoka machoni kama chemchemi ya maji" mwandishi anatuonesha hisia za Kido pamoja na mamake kuwa wana majonzi kiasi cha kutokwa na machozi kama chemchemi ya maji. Kiasi cha machozi kimetiwa chumvi ili kuonesha kulia kupita kiasi kwa sababu ya hisia nzito za mama huyu kuelekea mwenzi wake ambaye ametiwa mbaroni. Kido pia hulia kila mara mamake anapolia. Hii ni ishara tosha kuwa katika familia hii, washiriki wanajali hisia za wenzao.

Tashbihi pia inatumiwa kudhihirisha kina cha uhusiano kati ya Kido na nyanyake. Mwandishi

kupitia kwa Kido anasema:

> "Baba mimi nilimpenda nyanya sana. Naye alinipenda kama mboni ya jicho.
> Eeh! Nyanya alinipenda kwelikweli." (Uk. 2).

Mboni ya jicho ni sehemu iliyo katikati mwa jicho na hutunzwa ili isiguswe na chochote kwa sababu ndiyo hutumiwa kuona. Jicho pia ni taa ya mwili mzima. Kusema kuwa nyanya alimpenda na kumtunza mjukuu wake Kido kama mboni ya jicho lake ni ishara tosha kuwa mapenzi kati yao yalikuwa ya dhati na nyanya alimwona Kido kama taa au tegemeo katika jamii hii kwa sababu alikuwa ni mwanamume pekee aliyebaki baada ya babake kufungwa.

Sababu za Kido kumpenda nyanyake pia zinadhihirishwa kwa kutumia tashbihi. Kido anasema:

> "Nyanya alikuwa mpishi bora. Mpishi bora kama mama. La, mpishi bora kuliko mama." (Uk. 2).

Kwa kawaida, watoto wadogo hupenda mama zao kuliko mtu mwingine yeyote kwa sababu mama ndiye huwa nao pindi nyingi na ndiye huwatimizia mahitaji yote ya kimsingi kama vile kuwaandalia chakula. Kwa hiyo, kulinganisha mapenzi ya nyanyake na ya mama inamaanisha alimpenda kwa moyo wake wote. Jambo la pili lililomfanya Kido kumpenda nyanya yake ni hadithi zake ambazo Kido anakiri kuwa zilimfunza na kumburudisha. Anatumia tashbihi nyingine kuonesha jinsi alivyothamini sana hadithi hizi. Anasema:

> "Alitamba (nyanya) huku anaimba beti za mashairi na kuimba nyimbo kwa sauti nzuri kama ya ninga" (Uk. 3).

Hapa, Kido analinganisha sauti ya nyanyake na ya ninga kumaanisha aliithamini sana sauti hii. Watoto wa kiume hupenda kuwinda sana ndege lakini si ajabu kupata watoto wakimsikiliza ninga akiimba badala ya kumuua. Sababu ni kuwa wanapendezwa na sauti zao tamu. Kupitia kwa tashbihi hii, tunagundua kwamba jukukmu muhimu ya familia ni kupitisha turathi muhimu kwa watoto. Katika familia nyingi za Kiafrika, hili linapitishwa kwa njia ya hadithi. Hadithi hizi zilitumiwa kuwafunza watoto maadili mema. Mwandishi anaonesha kuwa Kido anatambua hili kupitia kwa maneno yake anayoyasema kwa kutumia tashbihi:

> "Lakini kilichonifanya nimpende zaidi ni ngano alizonitambia. Ngano zake ziliniburudisha, zikanifunza na kuniliwaza. Zilinipa sababu ya kuishi. Zilikuwa tamu kama chakula chake" (Uk. 3).

Hadithi hizi anazotaja alitambiwa wakila na hili linaonyesha uhusiano mzuri wa familia hii.

Tashbihi tatu zimetumiwa katika kuendeleza maudhui ya familia katika *Sitaki Iwe Siri*. Kwa mfano, mwandishi anasema kuhusu Mwalongo kuwa:

> "Aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho" (Uk. 10).

Hili linamaanisha kuwa Mwalongo aliwakimu wajukuu wake kwa hali na mali. Tunaambiwa kuwa aliwaandalia kiamsha kinywa asubuhi na mapema kabla hawajaenda shuleni na kula chajio pamoja. Ili kutimiza mahitaji haya, nyanya Mwalongo alifanya kazi za kilimo na ufugaji. Tunapendezwa na bidii hii kwa sababu alitimiza haya licha ya uzee na ugonjwa. Hili linaelezwa kwa kutumia tashbihi ambapo tunaambiwa:

> "Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji na mgongo wake ulikuwa umepinda kama uta" (Uk. 7).

Hii ni taswira inayochorwa kwa mbinu ya tashbihi ya jinsi Mwalongo anavyoonekana. Hili limesababishwa na ugonjwa na hatimaye kifo cha wanawe ambacho kimeuatua moyo wake na kumpatia mawazo mengi yaliyoathiri afya yake. Mgongo unaweza kuwa umepinda kutokana na uzee au hata kazi nyingi za shamba akijaribu kupata mahitaji ya lazima ili kuwakimu wajukuu wake. Hili anafanya bila shaka kwa sababu ya mapenzi yake kwa wajukuu wake.

Katika kuwatunza wajukuu wake kihisia moyo, Mwalongo alihakikisha wanakuwa na mazungumzo kila jioni wakila. Katika nafasi kama hizi aliwafunza mengi. Wajukuu hawa nao walikuwa wadadisi sana. Tunaambiwa:

> "Je mbona wajukuu hawa wana maswali mengi kama chiriku" (Uk. 5).

Nyanya Mwalongo alihofu kuwa kupitia kwa maswali haya, siku moja wangemuuliza kilichoua wazazi wao kwa sababu hili lingemtonesha kidonda cha kuwapoteza wapendwa wake. Pia ni kama anahisi kuwa ni mapema mno kwa wana hawa kujua kilichosababisha kifo cha wazazi wao.

Katika *Nimefufuka*, mwandishi anatumia tashbihi kuendeleza maudhui ya familia kwa kusema:

> "Ilikuwa mwiko mwana wao kuzikwa Mwambao kama mnyama asiye na wa kwao" (Uk. 8).

Tashbihi hii inadokeza hali ambapo familia ya akina Lena ilikuwa tayari kufanya yote yaliyokuwa katika uwezo wake ili kuleta mwili wa mwanao kutoka Mwambao kuzikwa nyumbani kwao. Mnyama huwa hazikwi na wa kwao. Akifia karibu na makazi ya binadamu huwa anashughulikiwa na watu hao. Akifia msituni mnyama huyu huliwa na wanyama wengine au hujiozea tu. Watu wa familia ya Lena wangepata aibu ikiwa mwanao angezikwa mbali na nyumbani na hivyo ikawabidi kuchangisha pesa ili kumleta na kumzika nyumbani. Hii ni ishara ya undugu unaopatikana katika mahusiano mema ya familia.

#### 4.3.1.2 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Familia

Picha 11 zimetumiwa na mwandishi wa *Wema wa Mwana* kuendeleza maudhui ya familia. Picha kwenye ukurasa wa 3 inadhihirika wazi kuwa Baba Juma ni mzazi ambaye anajali masomo ya familia yake. Anaonekana katika picha kuwa amechukua nafasi kumjulia mwanawe hali na kudadisi kuhusu hali yake shuleni. Juma anatumia nafasi hiyo kumweleza masomo yanavyomtatiza shuleni. Hata hivyo, Juma anaonekana mwoga kwa sababu anajua moyoni kuwa anafanya mzaha shuleni na kuwa ana tabia mbaya ya kuiba chakula pale nyumbani. Kwenye ukurasa wa 4, mamake Juma pia anashiriki majukumu haya ya uzazi. Mama Juma anapika jikoni huku Juma akiegemea ukuta. Mama anamshauri Juma kwa kumwambia kuwa sharti afanye bidii kwani nduguze Juma wanatia bidii masomoni.

Katika picha kwenye kurasa za 5 na 6, Baba Juma anachungulia jikoni ili aone anachofanya Juma. Kwa kufanya hivi anatekeleza wajibu wake kama mzazi. Baadaye katika ukurasa wa 7, baba Juma anampata akiwa na nyama moto mfukoni. Babake anatumia fursa hii kumkemea na kumkosoa dhidi ya tabia hii. Baadaye Juma anapoanza kulia kwa kuchomwa na nyama, washiriki wote wanamkimbilia na kumhurumia. Kwenye ukurasa wa 10, Baba Juma anamhurumia na kumsaidia kutoa vipande vya nyama moto mfukoni na kumpaka

dawa. Hii ni ishara ya mzazi mwenye kujali. Hili linadhihirika zaidi pale ambapo baba Juma anampaka Juma mafuta ili kumtulizia uchungu katika ukurasa wa 11.

Katika ukurasa wa 12, Baba Ngoyoni ambaye ni jirani ya babake Juma amemtembelea ili washauriane kuhusu ukosefu wa nidhamu ambao umekithiri miongoni mwa watoto wa siku hizi. Baba Ngoyoni ameamua kumpeleka Ngoyoni shule ya bweni ili afunzwe adabu. Babake Juma kwa upande wake anahisi kuwa ni jukumu lao kama wazazi kuwafunza watoto na hawapaswi kuwaachia walimu jukumu hilo. Baba Juma anashindwa kumshawishi babake Ngoyoni asimpeleke mwanawe katika shule ya bweni kwa sababu tunamwona katika picha kwenye ukurasa wa 13 akipokewa na mwalimu mkuu katika Shule ya Msingi ya Masomoni. Amempeleka Ngoyoni ili asome kule. Hii ni ishara ya uwajibikaji katika familia.

Katika picha kwenye ukurasa wa 15, tunamwona Baba Ngoyoni akichukua jukumu lake kwa uzito kwa kumchukua Ngoyoni kutoka shuleni. Kwenye ukurasa wa 16, mama yake pia anafyatuka mithili ya mshale ili kumlaki mwanawe anapoletwa nyumbani kutoka shuleni. Hili ni tofauti kabisa na inavyoonekana katika picha hii ambapo binti mmoja analazimika kubeba sanduku lake mwenyewe bila kulakiwa na wazazi wake. Basi ni wazi kuwa familia ya akina Ngoyoni inajali wanao na elimu yao. Inatimiza wajibu wake katika familia. Matokeo ya Ngoyoni shuleni na mfano mzuri katika familia hii yanamfanya Babake Juma kushawishika na kuamua kuwa naye angempeleka Juma katika shule hiyo ya Masomoni.

Katika riwaya ya *Nimefufuka,* picha kwenye ukurasa wa 2 inaonesha Sikitu akiwa ameketi mezani akiandikia shangazi yake barua. Anamweleza matatizo wanayopitia hapo nyumbani ili apewe mashauri ya jinsi ya kuyashughulikia. Picha hii inaendeleza maudhui ya familia kwa sababu kunapokuwa na shida, watu wa kwanza wa kuombwa msaada ni washiriki wa

familia. Pia katika ukurasa wa 4, kuna picha inayoonesha mama ya Lena wakiwa pamoja na Musa katika hoteli ya Bora Bora walikoenda kumtafuta Lena. Mama ya Lena anafanya bidii kwa sababu ya mapenzi ya mama kwa mwana wake. Baadaye, katika picha kwenye ukurasa wa 7, anachukua hatua ya kuenda kwa mganga ili kumtibu mwanawe kutokana na ugonjwa usiojulikana. Hata hivyo, hakupona.

Picha kwenye ukurasa wa 11 inaonesha Sikitu akiwa amechukua jukumu fulani pale nyumbani baada ya kutoka kwa mume wake aliyemuoa. Anaonekana akifua huku akimtunza mtoto wa Lena anayejililia kwa maradhi yanayomsumbua. Pia kwenye ukurasa wa 13, kitoto Taabu ambacho sasa kinaitwa Shujaa kinacheza na mwanasesere. Hata ingawa mamake alikufa, Sikitu amekifaa kama mamake mzazi na kinaonekana kuwa na furaha tele. Katika ukurasa wa 15, Jose anaonekana akimsihi Sikitu amsaidie. Jose anaonekana kuwa mchafu na dhaifu. Anaomba Sikitu amsaidie na pesa ili apate kunywa pombe au dawa za kulevya. Jose anataka Sikitu amfae kwa sababu ni mtu wa jamaa yake. Picha kwenye ukurasa wa 25 ni baada ya Upendo, shangazi ya Sikitu kumshauri na sasa Sikitu amekuwa na maoni mapya kuhusu maisha na anavaa nadhifu na kuonekana kuwa mwenye furaha zaidi. Kwa njia hii, washiriki hawa wa familia wanafaana na kujengana.

Picha katika ukurasa wa 1 katika *Kisasi Hapana* inaonesha Kido akiwa na majonzi huku anaandika barua kwa babake Mukulu. Picha ya mzee Mukulu pia inaoneshwa ukutani katika ukurasa huu. Hii ni ishara kuwa kuna mapenzi ya dhati katika familia ya mzee Mukulu. Picha katika ukurasa wa 3 inaonesha Kido akiwa na nyanyake jikoni wakila chakula ambapo anadai kuwa mamake ni bingwa katika kupika. Hii ni roho nzuri ya shukrani inayoonesha kuwa wanathaminiana. Pia, picha kwenye ukurasa wa 5 inaonesha jinsi mapenzi ya nyanya ya Kido yanamsukuma kujilazimisha kuingia ndani ya chumba cha daktari kwa lazima kabla

ya zamu yake kufika kwa kuhofia kuwa hali ya mjukuu wake iko taabani na hivyo anahitaji huduma ya dharura.

Katika familia, washiriki wanatunzana kukiwa na shida. Kwa mfano, kwenye ukurasa wa 9 katika *Kisasi Hapana*, picha inaonyesha jinsi mama na nyanya ya Kido wanambeba mgongoni na kupokezana mzigo huu kwa mapenzi wakati Kido anakuwa mgonjwa sana. Kwa upande wake, Kido mwenyewe anaonekana kwenye picha akiwa amezubaa na kupigwa na butwaa baada ya kumpoteza nyanyake mpendwa katika kifo.

#### 4.3.1.3 Methali Inavyoendeleza Maudhui ya Familia

Katika *Nimefufuka*, mwandishi ametumia methali kuonyesha jinsi Sikitu anavyokashifu wazazi wake baada ya kushindwa kumlea Lena:

> "Angesema nini ilhali aliogopa kumkunja samaki angali mbichi" (Uk. 4).

Methali "kukunja samaki" imetumiwa kuonesha mafunzo yanayotolewa na mzazi kwa mwanawe. Inamaanisha kuwa wazazi wanakosa kumfunza Lena kimaadili. Hawakutimiza jumkumu lao la ulezi vizuri. Kuna uwezekano hawakufanya lolote na wakashtukia maji kuzidi unga wakati binti huyu alipotoroka nyumbani na kujiingiza katika anasa. Kuhusu uzembe wao, mwandishi anasema:

> "Wazazi walibaki kulaumiana badala ya kuganga yajayo. Hawakujua yaliyomwagika hayazoleki" (Uk. 4).

Huu ni mdokezo wa methali "Maji yakimwagika hayazoleki." Imetumiwa kuonesha jinsi wazazi wa Lena wenyewe wanalaumiana kwa kushindwa kulea binti yao kimaadili mapema. Hakuna kile wangesema kwa kuwa hakukuwa na muda wa kurekebisha mambo kwani tayari alikuwa ameambukizwa ugonjwa mbaya. Sasa maisha ya Lena yanamhangaisha mama yake sana hadi Sikitu anasema methali inayoakisi ukweli wa hisia hizi akisema:

"Kweli uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi." (Uk. 20).

Uchungu anaohisi mama huyu unamsukuma kutia bidii kumtafuta binti yake na anajiliwaza kwa methali:

"Wakati huu alikuwa mwingi wa matumaini. Panapo nia pana njia" (Uk. 5).

Kwa sababu mama ya Lena alikuwa na azma ya kutafuta binti yake, ilimbidi kufanya juu chini kumpata Lena. Kwa hiyo, methali hii inampatia nguvu ya kurudi tena Mwambao kujaribu kumtafuta binti yake lakini bado anaambulia patupu.

Mwandishi wa *Nimefufuka* anatumia methali kuonesha kuwa Sikitu anapoingia katika mpango wa familia na kushindwa kupata mtoto anahuzunika sana. Anasema:

"Niliposhindwa kustahimili matusi, nilifunganya virago na kurudi kwetu, kwenu, kwani ng'ombe akivunjika guu malishoni, hujikokota zizini kusaidiwa" (Uk. 10).

Hii ina maana kuwa katika jamii, kupata mtoto katika familia ni jambo la msingi. Ikiwa wenzi wa ndoa hawawezi kupata mtoto, ni mwanamke anayelaumiwa. Wanaume hata hukataa kutafuta tiba. Hili linafanyika katika familia ya Sikitu. Sikitu anaripoti kuwa katika jamii hii, ukosefu wa uwezo wa kupata mtoto ni shida ya mwanamke. Wanaume ni safi safina na ikiwa itatokea kasoro, hiyo ni kasoro ya mwanamke. Mambo yanapoharibika, ilibidi mwanamke huyu kurudi kwao na hili ndilo linafafanishwa na ng'ombe aliyevunjika mguu kurudi zizini mwake. Sikitu anarudi kwao kwa kukosa mtoto. Sikitu anamaanisha ilimbidi kurudi zizini kwao akimaanisha nyumbani ili washiriki wa familia yake wamfariji na kumtia moyo kwa yale yaliyompata.

Katika riwaya ya *Kisasi Hapana*, mwandishi anatumia methali pale ambapo Kido anasema kwamba ikiwa babake angekuwako pale nyumbani, hangehitaji kuambiwa tu yaliyotokea. Kido anasema:

"(Baba) kusikia si kuona, tuone ndipo tuambe" (Uk. 16).

Kwa kutumia methali hii, ni kama yale ambayo baba huyu ameambiwa kupitia kwa barua kuhusu hali ilivyo nyumbani hayatoshi. Alipaswa ajionee ndipo ajue uzito wa anayoambiwa. Kupitia haya, tunagundua kuwa Kido anakosa mapenzi ya baba katika familia. Pia katika kuonesha hasira zake, Kido kuelekea kwa yule aliyeua nyanyake anaonesha kuwa kama ingewezekana naye pia alipaswa kuuawa. Hata hivyo, kwa kukosa uwezo, anamalizia kuwa inabidi wamwachie Mungu na anatumia methali kudhihirisha hilo. Mwandishi anasema:

> "Lakini watu wa ukoo wa dereva pia ni wa kuachiwa Mungu? Asomlifi, mlifi ni Mungu" (Uk. 16).

Babake Kido pia anatumia methali kudhihirisha hisia zake wakati Salama anapopatikana baada ya kutekwa nyara na hili linaandamana na majonzi ya kumpoteza mamake. Anasema:

> "Heri nusu ya shari kuliko shari kamili" (Uk. 38).

Katika methali hii, Mzee Mkulu anaona ni afadhali kuwa binti yake aliyetoroshwa na majambazi amepatikana kwa kuwa ingekuwa hasara mara mbili ikiwa angepoteza mamake katika kifo na pia binti yake apotee kabisa bila kupatikana. Kwa njia hii, mapenzi kati ya washiriki wa familia yanaendelezwa.

### 4.3.1.4 Taswira Inavyoendeleza Maudhui ya Familia

Katika *Wema wa Mwana*, Kido anaeleza kwa huzuni jinsi mama yake hulia kila mara na kila mama yake anapolia yeye naye hulia. Hili linatoa taswira ya watu walio na majonzi na wanalizana bila ya kuwa na mtu wa kusaidia mwingine. Hii inadhihirisha maudhui ya familia kwa kuwa mapenzi ndiyo yanafanya washiriki wa familia hii kulia kwa kumkosa baba na mume. Katika *Wema wa Mwana*, kuna taswira ya furaha kuu katika nyumba ya akina Ngoyoni. Wanafurahi kuwa mwanao Ngoyoni amerudi kutoka shuleni. Kila mmoja anataka kuzungumza na Ngoyoni ili aelezwe hali ilivyo katika shule yao. Hii ni ishara tosha kuwa washiriki wa familia hii wanapendana na kujaliana. Kwenye ukurasa wa 1 wa *Kisasi*

*Hapana*, kuna taswira ya kilio cha kila siku cha mama ya Kido baada ya babake kuondoka na kuwekwa korokoroni. Mama huyu analia kama mtoto mdogo kwa sababu ya upweke unaomkabili.

Hatimaye katika *Sitaki Iwe Siri*, kuna taswira ya jinsi Mwalongo anavyomwamsha Musa asubuhi na mapema na kisha Musa kuzinduka kutoka usingizini na kupapasa juu ya meza ili kupata taa yake ya kibatari na kuiwasha. Pia, kuna taswira ya Musa akiwaamsha dada zake Haki na Ukwa ambao walikuwa katika usingizi mzito wa pono ili wajiandae kwenda shuleni. Kazi wanayofanya kuamsha wenzao inamaanisha kuwa walikuwa na mapenzi kati yao kama washiriki wa familia moja.

#### 4.3.1.5 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Familia

Katika *Nimefufuka*, nahau imetumiwa kudhihirisha uhitaji wa msamaha katika familia. Mwandishi anasema:

> "Bila hata kupumzika mama aliomba kupelekwa hoteli ya Whispering Trees, maskani mapya ya Lena. Musa alisalimu amri" (Uk. 4).

Musa, mpwa wa Lena aliposikia yaliyompata Lena, alizika aliyofanyiwa katika kaburi la sahau ili kumuauni mwenzake anapopatwa na janga. Alimshughulikia Lena aliyekuwa ametorokwa na marafiki zake. Nahau **"**kusalimu amri" imetumiwa kumaanisha kwamba Musa alikubali kutimiza aliloombwa kufanya hata ingawa anafanya hivyo shingo upande. Licha ya jitihada za mama kumtafuta mwanawe, mwana huyu anakataa kuonana naye. Mwandishi anatumia nahau kudhihirisha hili anaposema:

> "Mama alipigwa na butwaa asijue la kusema. Hakuamini mwanawe aliyembeba tumboni miezi tisa na kumzaa angemtenda hivyo". (uk 4).

"Kupigwa na butwaa" ni mshangao mkubwa. Hakuna mtoto anayeweza kukataa kuonana na mamake hata hali iwe mbaya kiasi gani. Kwa hivyo, tendo hili la Lena kukataa kuonana na mamake ni tendo la ajabu sana. Hii ndiyo sababu Mama Lena anahisi amesalitiwa pakubwa kutokana na binti yake mwenyewe kumkana mbele ya watu.

Nahau imetumiwa pia kuonyesha hali ya ujauzito na kuzaa. Mwandishi anatuambia kuwa Lena anapopata ujauzito, mimba ile ilimpatia matatizo na hili linadhihirishwa wazi kupitia nahau:

> "Wakati huo, Lena alikuwa mjamzito. Inadaiwa mimba hiyo ilimkataa. Iliasi kukaa chupani mwake. Ikaomba itoke lakini akaiomba kughairi tarehe ya kutoka". (Uk 7)

Kupitia maelezo haya tunagundua kuwa Lena alikuwa na matatizo akiwa na mimba kiasi cha kumfanya kutamani mimba isitoke hadi wakati wake unaofaa.

Kama ilivyo desturi katika familia, mtoto ni wa kila mtu. Wakati Lena anakufa inabidi Sikitu kumtunza mtoto wake kwa sababu nyanya yake pia ni mgonjwa na hawezi kumtunza mjukuu wake. Sikitu anasema hili kutumia nahau:

> "Baada ya mazishi ya Lena, jukumu la malezi ya kitoto chake liliniangukia" (Uk. 10 ).

Kutokana na nahau hii, inadhihirika kuwa Sikitu hana hiari ila inambidi amshughulikie mtoto huyu kwa sababu jamii inatarajia hivyo. Baada ya muda, Jose pia anakuwa mgonjwa vibaya. Dadake anasema hivi kuhusu hali hii:

> "Haihitaji daktari kutangaza kwamba kifo kinamkodolea macho. Jana, nusura Jose atupe mkono wa buriani" (Uk. 15).

Maneno haya kifo "kinamkodolea macho" ni hisia za huzuni za Sikitu akimhurumia ndugu yake kwa hali anayopitia ya ugonjwa. Ugonjwa huu ulikuwa mbaya kiasi cha kumuua Jose. Alinusurika tu. Kwa hiyo, kupitia nahau hii maudhui ya familia yanaendelezwa. Katika *Kisasi Hapana*, maudhui ya familia yameendelezwa na mwandishi kwa kutumia nahau ambapo tunafahamishwa kuwa Kido anampenda sana baba yake na angependa kujua aliko. Anahisi kuwa wengine wanajua alipo na wanakataa tu kumwambia. Anatumia nahau kueleza hisia zake:

> "Hawa watu wazima wa kijijini kwetu wanajua ulipo ila wamekula njama kunificha" (Uk. 17).

Hapa "kula njama" imetumiwa kumaanisha kuwa watu hawa wameshauriana ili mtu yeyote asiende kinyume na maagano kwa kumwambia Kido siri ya aliko babake na kwa njia hii, anahisi kuwa amesalitiwa nao. Kido pia ana hisia nzito kuelekea washiriki wengine wa familia kiasi cha kutaka baba yake awalipizie kisasi watu wote waliowakosea au kuwatendea mabaya kama yule dereva wa mkuu wa wilaya aliyesababisha kifo cha nyanyake na wale walioteka dada yao nyara. Anasema hivi:

> "Uwafanye adabu waliotukosea" (Uk. 34).

Kido pia anatoa hisia zake kwa dadake ambaye wana uhusiano wa damu. Anasema kuwa; "Salama amekuwa fahari yetu." Kido anasema hili kwa sababu dadake Salama ni bingwa katika masomo na hata michezo shuleni. Anafanya vizuri katika riadha na mpira wa miguu. Pia kuhusu kifo cha nyanyake, Kido ametumia nahau kadhaa kuelezea hisia zake. Analalamika kwa kusema:

> "Ametuondokea…. amekwenda jongomeo… ametuacha mkono" (Uk. 3).

Mzee Mkulu, baba ya Kido pia anatamani kurudi nyumbani na kujiunga na familia yake ili wafurahie na kuteseka pamoja. Hili linadhihirika katika ombi lake analotumia nahau kulitoa:

> "Endelea kuvuta subira na kuniombea" (Uk. 35).

Anamsihi Kido amwombee ili aachiliwe haraka kutoka jela ndipo wawe pamoja kama familia.

Katika *Sitaki Iwe Siri* tunaambiwa kuhusu vifo vya wanawe Mwalongo. Mwandisi anasema:

> "Vifo hivyo vimeutia kovu moyo wake. Yusufu na mke wake waliugua kwa muda mrefu sana na hatimaye kusalimu amri" (Uk. 8).

Katika nahau "kusalimu amri" tunagundua kuwa Yusufu na mke wake waliugua kwa muda mrefu na katika kipindi hiki mama yao aliishi kwa simanzi kwa kuwaonea imani. Hatimaye wana hawa wanakufa. Vifo vyao vinamwacha mama yao na kovu linalokataa kupona. Hii

ni ishara ya mapenzi yake kwao. Mwalongo anahuzunika sana kwa kutazama makaburi ya mwanawe Yusufu Matano na mke wake Honorota Matano. Katika kuonesha hisia hizi mwandishi anasema:

> "Nyanya Mwalongo alipiga miundi kwa hatua haba huku akionekana mwenye mawazo mengi" (Uk. 6).

Kupiga miundi ni kutembea polepole huku umeshika mikono nyuma na kuinamisha kichwa chini. Hii ni ishara ya kuwa katika mawazo mazito ya majonzi. Basi kwa maelezo haya, ni wazi kuwa Mwalongo anahuzunika kwa kiwango kikubwa anapowakumbuka wanawe.

**4.3.1.6 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Familia**

Katika kuendeleza maudhui ya familia, msemo umetumiwa katika *Kisasi Hapana* unaosema:

> "Baba wewe ndiwe ungenishughulikia kwa hali na mali" (Uk. 28).

Katika msemo "kwa hali na mali", tunapata maana kuwa mtu angetumia chochote kilicho katika uwezo wake kumsaidia mwenzake. Kupitia maneno haya, Kido anahisi kuwa ikiwa babake angekuwapo angetunzwa vema zaidi kwa sababu ya uzito wa damu. Katika *Sitaki Iwe Siri*, mwandishi ametumia misemo ili kufanikisha maudhui ya familia. Mwandishi anatuambia:

> "Nyanya Mwalongo amewatunza mayatima hawa miaka nenda miaka rudi hadi nguvu zimemwisha kwa sababu ya umri wake mkubwa" (Uk. 9).

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa Mwalongo alijitahidi kadri ya uwezo wake ili kuwapa wajukuu wake malezi mema. Alifanya yote aliyoyaweza ili kuwaandalia mahitaji yao.

Katika *Kisasi Hapana*, tunapata kuwa mtoto anapochokozwa na watu au wanafunzi wenzake shuleni huhisi kuwa babake anaweza kumwokoa. Hili linadhihirika wakati Kido anaposema hivi kwa wachokozi wake:

> "Wakione kilichomfanya kanga kukosa manyoya shingoni. Wakione kilichomfanya sangara kuchomwa moto. Wakione cha mtema kuni" (Uk. 22).

Kido anahisi kuwa anateseka shuleni kwa sababu baba yake hayuko karibu. Ikiwa angekuwa nyumbani, basi wanafunzi wenzake hawangemchokoza kwa kuwa babake angewaadhibu. Kwa njia hii, mwandishi anadokeza kuwa Kido anakosa mapenzi ya babake katika familia yao.

### 4.3.2 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu katika Fasihi ya Watoto

Katika kuendeleza maudhui ya elimu, waandishi wametumia misemo, tashbihi, taswira, picha, methali, misemo na nahau. Vipengele hivi vimeendeleza maudhui haya kwa njia mbalimbali kama tunavyoonesha hapa chini.

#### 4.3.2.1 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Kwa kutumia tashbihi, Ken Walibora ameangazia elimu kuwili katika riwaya yake ya *Kisasi Hapana*. Kwanza, kuna elimu ya wazazi kwa watoto wao ambayo iliendelezwa kupitia kwa hadithi walizohadithiwa jioni huku wakila. Pili, kuna elimu ya shuleni iliyo na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni ile ya kuendeleza vipawa vya wanafunzi na ya pili ni elimu ya vitabuni. Mwandishi ametumia tashbihi kudhihirisha hisia za wanafunzi kuelekea sehemu hizi mbili za elimu. Kwa mfano, dada ya Kido anayeitwa Salama alikuwa msichana hodari sana darasani. Ndugu yake Kido anatumia tashbihi kwa kudhihirisha hili anaposema:

> "Salama alikuwa mwanafunzi mzuri shuleni. Alifaulu kwenye masomo na michezo. Kama unakumbuka, Salama ni aina ya mwanafunzi ambaye kwake yeye kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala." (Uk. 17)

Kwa kutumia tashbihi "kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala" Kido anakiri kuwa kuna wanafunzi wengine ambao ilikuwa rahisi sana kwao kupasi mitihani kama tu ilivyo rahisi kufumba macho kwani mtu hahitaji kutumia nguvu kufumba macho yake pindi anapohitaji kulala. Hata hivyo, ni kawaida kwa wanafunzi

kutofautiana katika viwango vyao vya elimu wanapokuwa shuleni kwa sababu hawawezi kuwa na uwezo sawa. Hili linaonekana katika maneno haya:

> "Shule imeumbiwa watu kama Salama, sio watu kama mimi wasioweza kuunga moja na moja wakapata mbili" (Uk. 17).

Mwanafunzi mwingine aliyekuwa na uwezo mkubwa darasani ni Samueli ambaye Kido anasema kumhusu kuwa, "Kwa hivyo niliwaachia mabingwa wa hesabu, kama akina Samueli, kuhesabu magoli." Ni wazi kuwa wanafunzi wengine wangefurahi sana ikiwa shuleni wangefunzwa tu michezo bila masomo ya darasa. Haya ndiyo matamanio ya Kido na yanaelezwa kwa kutumia tashbihi. Kido anasema:

> "Kama shule ingekuwa mpira tu unachezwa, mbona ningependa shule kama mboni ya jicho langu? Ningependa shule kama ninavyopenda peremende na nyama ya kuku" (Uk. 28).

Tashbihi "ningependa shule kama mboni ya jicho langu" ikiwa ni mpira ungekuwa unachezwa inafaa kwa sababu watoto wanapenda kucheza sana. Watoto hupenda mpira hata kuliko chakula. Kwa hiyo, wazazi na walimu lazima kwa kiasi fulani kukaza kamba ili kuwafanya watoto kuenda shuleni kwa sababu wao ndio wanaoelewa umuhimu wa elimu. Na hili hata watoto wenyewe wanajua kwa kuwa wanasema:

> "Vinginevyo kwangu mimi shule ni kama dawa chungu ambayo mtu analazimishwa kumeza. Unameza tu maana wanaokupa wanadhani utafaidika, ingawa unaumia" (Uk. 28).

Hapa, Kido anaelewa kuwa dawa ni muhimu kwa tiba lakini bado inabidi alazimishwe ndipo aweze kuimeza. Kwa jinsi hii pia, watoto wengine hubidi walazimishwe ndipo waende shuleni kwa sababu walimu na wazazi ndio wanaojua umuhimu wa elimu kwa watoto hawa. Pia, inawezekana kwa mtu kufuzu katika sehemu zote mbili za masomo, yaani michezo na kazi za darasa au masomo ya vitabuni. Salama anafanya vizuri katika sehemu zote mbili. Ndugu yake anasema kuwa:

> "Hili la werevu wake Salama pengine bado unalikumbuka. Lakini sidhani una babari kuhusu ubingwa wake michezoni. Nafikiri wewe uliondoka huku kijijini kabla Salama hajaingia kwenye kikosi cha shule yetu cha mpira wa pete. Tena yeye

amejaliwa uwezo wa kukimbia mbio za masafa mafupi. Alikimbia mpaka kiwango cha taifa" (Uk. 28).

Kuhusu michezo, uwanja wao wa michezo na ubingwa wa Kido katika kandanda, mwandishi anasema:

> "Nikizifunga goli kwa urahisi kama kuteremsha maji kooni."
> "Wakati wa kiangazi (uwanja) una mavumbi kama jangwa na wakati wa masika au vuli una matope kama kinamasi" (Uk. 22).

Shuleni wanafunzi hufundishwa na kuzoeshwa kufanya kazi chini ya usimamizi wa watu wengine. Hili linaoneshwa kwa kutumia tashbihi Kido anaposema:

> "Yaani pote (shuleni) hapo ni mahali ambapo maisha ya watu yanaendeshwa kama gari na watu wengine" (Uk. 13).
> "… kaendesha gari kama vile walimu wanavyotuendesha sisi wanafunzi shuleni" (Uk. 13).

Kwa mtoto, gari huendeshwa kwa kasi na pia gari huwa halina hiari ya litakakoelekea. Ni juu ya dereva kuamua kasi na sehemu ya kwenda. Ndivyo ilivyo na wanafunzi shuleni. Hawana hiari ya jambo la kufanya. Walimu ndio wanaoamua; na hili ndilo Kido hapendi.

Katika *Sitaki Iwe Siri*, mwandishi ametumia tashbihi kuonesha namna watoto wanavyobeba vitabu wanapoelekea shuleni. Tunaambiwa:

> "Walikuwa wamebeba mikoba ya vitabu vyao kama watalii" (Uk. 12).

Wakati wa gwaride hasa wakati walimu walikuwa wanaongea, mwandishi anasema hivi kuhusu kimya:

> "Wanafunzi walifyatuka kama mishale ungedhani ni wanajeshi kwenye vita vya kwanza vya dunia" (Uk. 14).
> "(Wakati wa gwaride) mlio wa sindano sakafuni ungalitoa kishindo kikubwa kama cha bomu la atomiki" (Uk. 15).

Maana inayojitokeza katika tashbihi "kishindo kikubwa kama cha bomu la atomiki" ni kwamba kimya kinaashiria kuwa elimu inahitaji utulivu na nidhamu na hilo ndilo linaonekana katika wanafunzi hawa.

Wanafunzi wenye bidii wakiwa shuleni muda wao huonekana kuenda haraka sana. Hii ni kwa sababu ya shughuli nyingi walizo nazo. Hili limeelezwa kwa kutumia tashbihi ambapo mwandishi anasema:

> "Muda una mbawa kama ndege. Wakati wa Jumatatu hiyo ulionekana kukimbia sana"
> (Uk. 22).

Baada ya masomo ya siku, wanafunzi walishangilia kwelikweli waliporuhusiwa kuenda nyumbani. Furaha yao inaoneshwa kupitia kwa tashbihi:

> "Alifululiza hadi eneo la paredi ambapo wanafunzi walikuwa wameanza kukusanyika huku wakipiga kelele kama bumba la nzi". (Uk 58).

Shangilio hili linaashiria pumziko wanalopata baada ya siku yenye shughuli nyingi kwani elimu ni shughuli inayochosha akili.

Wakiwa shuleni, wanafunzi bora hupewa kazi za ziada za kufanyia utafiti. Kwa mfano, Musa anakubali kazi ya kufanya utafiti kuhusu Ukimwi ili hatimaye aandike insha itakayoshiriki katika shindano la kitaifa. Hii si kazi rahisi na mwandishi anaelezea jukumu hili kwa tashbihi na kusema:

> "Tangazo hilo la mwalimu mkuu lilimfanya ajihisi kwamba alikuwa amejitwika mzigo mzito kama nanga" (Uku. 26).

Wanafunzi wanaopenda masomo yao hufurahia fursa wanazopata za kuendeleza kazi zao. Kwa mfano, nyanya ya Musa anapompatia Musa ruhusa ya kwenda mjini ili kufanya utafiti, Musa anafurahi sana. Hisia zake  zinadhihirishwa kupitia kwa tashbihi:

> "Alifurahi kama kibogoyo aliyetunukiwa jino ombi lake lilipokubaliwa" (Uk. 27).

#### 4.3.2.2 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Mwandishi Ken Walibora ametumia misemo katika riwaya yake ya *Kisasi Hapana* katika kuendeleza maudhui ya elimu. Kuhusu tabia ya Kido anasema:

> "Ninapenda kufunga magoli, sio kufungwa" (Uk. 11).

Msemo huu unatuonesha kuwa Kido alipenda michezo sana na alikuwa bingwa kwani kila mara, yeye ndiye angefunga magoli. Hata hivyo, alipenda mpira kuliko kusoma. Kwake yeye, kama shule ingekuwa inafunza michezo peke yake, angeipenda kwelikweli. Yeye anaona masomo ya darasani kama jela. Pindi fulani baada ya kukaa nyumbani kwa muda kwa sababu ya ugonjwa, hakutaka kurudi shuleni kwa sababu hakupenda kusoma. Kido anasema:

> "Nikarejea shuleni tena, lakini shingo upande" (Uk. 11).

Kuhusu uwanja wa mpira wa akina Kido, Kido anasema hivi:

> "Umenyolewa nyasi na miguu yetu" (Uku. 23).

Hii ni ishara kuwa uwanja huu unafanyiwa kazi na wanafunzi hawa wanapocheza mpira kila siku kule shuleni. Hisia hizi za Kido zinaashiria kuwa labda pana haja ya mfumo wa elimu kutilia uzito ukuzaji wa vipawa vya wanafunzi.

### 4.3.2.3 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Katika kuendeleza maudhui ya elimu hasa michezo ambayo ni sehemu ya mafunzo wanayopokea wanafunzi shuleni, mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia nahau. Nahau hizi ni:

> "Ninavyowala chenga… nikatoa pasi nzuri kwa Saulo… na kutoa pasi nyingine nzuri… nikampiga chenga beki wao… nikakata mbuga… nikavuta kasi na kupiga shuti safi sana" (Uk. 28).

Nahau hizi zimetumiwa kuelezea jinsi Kido alivyokuwa bingwa katika kucheza kandanda huko shuleni. Ubingwa wake katika michezo unamfanya Kido kuwa na tamaa ya kuwa mchezaji hodari wa kandanda kimataifa. Hata hivyo, baada ya kuvunjika mguu anahisi kuwa ndoto yake ya kuwa mchezaji hodari ni kama haitafaulu. Anasema:

> "Ninaelekea kukata tamaa… ndoto zangu zinaelekea kugonga ukuta" (Uk. 30).

#### 4.3.2.4 Taswira Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia taswira kuendeleza maudhui ya elimu kwa kukejeli hali ya masomo katika Shule ya Mitini ikiilinganishwa na Shule ya Masomoni. Picha inayomjia msomaji akilini ni kuwa masomo katika shule ya Mitini ni duni hata kutokana na jina lake tu. Shule ya Masomoni inaonekana kuwa bora na kuwa walimu wanatia bidii hata kwa kuwashauri wanafunzi na kuwarekebisha tabia. Mwanafunzi akionesha maendeleo wanafuatilia na kumzawadi ili iwe mvuto kwa wanafunzi wengine. Kwa upande mwingine, katika shule ya Mitini, wanafunzi wanacheza tu na walimu hawahusishi wazazi kujadili matatizo ya wanao kwani hakuna hata mwalimu ambaye amewahi kuripoti kuwa Juma ana shida katika baadhi ya masomo shuleni.

Katika ukurasa wa 20 kutokana na maelezo ya mwandishi, taswira inayomjia msomaji ni furaha kubwa iliyo katika nyumba ya akina Ngoyoni wakati anaporudi kutoka shuleni. Familia hii ina furaha kuu kwa sababu mwanao ametoka shuleni akiwa mtu tofauti. Amekuwa na nidhamu zaidi na mwenye mapenzi zaidi kwa wazazi na ndugu zake. Hii ni kwa sababu ya matokeo mazuri katika elimu ya Ngoyoni. Taswira hii ya furaha kuu ndiyo inayowashawishi wazazi wa Juma kumpeleka Juma katika shule hiyo pia.

Maudhui ya elimu yameangaziwa katika *Sitaki Iwe Siri* kwa kutumia kipengele cha taswira ambapo tunawaona Musa, Haki na Ukwa wakiamka ili kujiandaa kwenda shuleni. Watoto hawa watatu wana mazoea ya kufanya masomo ya ziada nyumbani. Tunatambua hili kupitia maelezo ya kitaswira ya mwandishi ambapo Musa alipapasa kwenye meza aliyokuwa anasomea kule chumbani kutafuta kiberiti. Meza ile ilikuwa na vitabu vyake na vya dada zake. Hii ni ishara kuwa kabla achukuliwe na usingizi alikuwa akisoma na hivyo basi kuendeleza maudhui ya elimu.

Musa, Haki na Ukwa walikuwa wakisoma katika shule ya Msingi ya Hekima. Kupitia kwa maelezo ya kitaswira tunaambiwa kuwa, katika Shule ya Hekima wanafunzi wasichana walivalia sare ya samawati mshono wa debe pamoja na blausi nyeupe. Walivalia viatu vyeusi na soksi nyeupe. Wavulana nao walivalia shati jeupe na suruali ya khaki ya rangi ya samawati, viatu vyeusi na soksi za rangi ya kijivu. Kupitia kwa maelezo haya ya kitaswira ni kama tunaona hao wanafunzi wakiwa katika sare zao. Tunaambiwa kuwa ilibidi hawa watoto watatu watoke nyumbani saa kumi na mbili asubuhi ili waweze kuwahi shuleni. Nyanya yao Mwalongo aliwatakia mema shuleni kwa kusema kuwa wajitahidi na wahakikishe kwamba wamevisoma vitabu vyote ulimwenguni. Kitaswira, tunaona kiasi cha kazi ambayo wajukuu hawa walipaswa kufanya. Na kwa kuwatakia mema hivi, vijana hawa walitia bidii sana shuleni ili kumfurahisha nyanya yao.

Sehemu muhimu ya elimu ya shule ni kucheza. Michezo hii huwawezesha wanafunzi kupumzisha akili na kukuza urafiki. Katika kudhihirisha hili, mwandishi anatumia taswira inayoonesha kuwa wengine walisimama katika vikundi vya wanafunzi wawili watatu wakipiga gumzo huku wengine walikuwa wakicheza mchezo wa mwajificho. Kwa upande wake, Musa akiwa shuleni alikuwa tofauti sana kwani tunaambiwa kuwa punde alipofika shuleni aliingia katika darasa lake la 6A na kuanza kufanya kazi zake za ziada. Mwandishi anatumia taswira ya uporo ili kuonesha kuwa Musa alikuwa akifanya kazi alizokuwa amepewa siku iliyotangulia lakini hakuweza kuimaliza.

Kupitia taswira ni wazi kuwa wanafunzi wanapokuwa shuleni huhitajika kutii na kufuata mwelekezo wa kengele kwa kukimbia wanapohitajiwa na kutenda walilozoeshwa kufanya. Tunaambiwa kuwa dakika tano baadaye, wanafunzi wote katika shule ya msingi ya Hekima walikuwa wamepanga mistari kulingana na madarasa yao na kufyata ndimi zao. Kulikuwa na kimya hivi kwamba, mlio wa sindano sakafuni ungalitoa kishindo kikubwa kama cha

bomu ya atomiki. Kupitia taswira hii, tunaoneshwa jinsi watoto hawa walikuwa wametulia gwarideni. Baadaye kuna taswira ya Mwalimu Ochuka akitembea kati ya wanafunzi kwenye gwaride akikagua usafi wa wanafunzi wake kabla ya bendera kupandishwa. Kupitia kwa maelezo haya ya kitaswira, tunagundua pia kuwa wanafunzi katika shule hii ya Hekima pia hufunzwa uzalendo kupitia kwa kuimba wimbo wa taifa kila wanapopandisha bendera. Hili hufanywa kila Jumatatu na Ijumaa wanapokuwa kwenye gwaride.

Katika kuendeleza maudhui ya elimu, Musa anatembelea kituo cha afya cha Nyagacho ili akutane na daktari atakayemsaidia katika utafiti wake kuhusu Ukimwi. Kwa kutumia taswira, mengi yanasemwa kuhusu mkutano huu. Kwa mfano, wanapokutana kwa mara ya kwanza na Daktari Ataya, tunaambiwa macho yao yalikutana na mtu mrefu mwenye macho makali yaliyopenya kama miale ya jua na alikuwa amevalia koti jeupe kama maziwa. Daktari huyu aliwasalimu huku amevaa tabasamu usoni. Kabla ya kuendelea na mazungumzo, mwandishi anazidi kusema kuwa kulikuwa na kimya cha kaburi kama kwamba Shetani alikuwa anapita. Haya ni maelezo ya kitaswira kuhusu yanayotokea wakati Musa na wenzake wanapopata nafasi kuzungumza na Daktari Ataya kuhusu Ukimwi ili kupata habari za ziada ili kunogesha uandishi wao wa insha. Tukio hili linadhihrisha maudhui ya elimu ambayo yameendelezwa nje ya maeneo ya darasani hadi kituo cha afya.

#### 4.3.2.5 Methali Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia methali katika kufanikisha maudhui yake ya elimu kwa kutuchorea jinsi Musa anajibwaga katika mashindano ya kuandika insha baada ya kushawishiwa na mwalimu mkuu. Musa anatumia mdokezo wa methali kuelezea azimio lake la kukubali kuandika insha kuhusu Ukimwi anaposema:

> "Alimradi nimeyavulia nguo, sina budi kuyaoga…" (Uk. 21).

Maneno ya methali hii yanamaanisha kuwa angejitahidi kufanya kazi hii kwa bidii kwa sababu alikwisha kumuahidi mwalimu wake mkuu. Katika insha yake, Musa anamchora mhusika kwa jina Yuri ambaye anajuta kwa kujiingiza katika anasa na kupata Ukimwi. Methali inatumiwa kuonesha kuwa hili lilimpata Yuri kwa sababu alikataa elimu kutoka kwa wazazi:

> "Alikumbuka jinsi wazazi wake na walimu wake walivyojitahidi kwa hali na mali kumwelimisha ili ajitayarishe kwa maisha ya siku za usoni lakini akalilia wembe. Nyembe za walimwengu wa ulimwengu zilikuwa zimemkata Yuri na kumjeruhi vibaya" (Uk. 48).

Kulilia wembe ni mdokezo wa methali inayosema "Mtoto akililia wembe mpe". Hapa imetumiwa kuonesha kuwa Yuri alijiingiza katika anasa mwenyewe na akapata ugonjwa wa Ukimwi. Ugonjwa huu unamuua hatimaye.

Katika riwaya ya *Kisasi Hapana*, Ken Walibora ametumia methali kutueleza kuwa wakati wa michezo wanafunzi huhisi kuwa wanapaswa kulipiza kisasi wanapoumizwa na wenzao. Hili linaonekana wakati Kido anakanyagwa na Fwenjo walipokuwa wanacheza. Kido anatumia methali anaposema:


> "Nilikuuliza kama napaswa kumtendea kama alivyonitenda. Nilipe jino kwa jino, kwa mujibu wa methali ya wahenga isemayo, dawa ya moto ni moto?" (Uk. 33).

Kupitia methali hii, Kido anadokeza kuwa kama ingekuwa ni uwezo wake, angekanyaga hasimu wake Fwenjo ili naye avunjike mguu na ahisi uchungu jinsi naye alivyohisi. Anasahau kuwa hii ilikuwa tu ajali na kuwa hakufanya hivi kimakusudi. Wanafunzi wanapaswa kujifunza kuishi na wenzao kwa kuwasamahe kila uhitaji huo unapotokea.

#### 4.3.2.6 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Elimu

Katika riwaya ya *Kisasi Hapana*, picha imetumiwa kuendeleza maudhui ya elimu pale ambapo Baba Juma anachukua nafasi ya kujua maendeleo ya Juma shuleni. Anagundua kuchelewa kuwa Juma ana matatizo katika masomo kadhaa kama Sayansi Kimu na

Hisabati. Hili limedhihirishwa wazi katika picha kwenye ukurasa wa 3 ambapo Juma anaonekana akisailiwa na babake.



**Kielelezo 4.7: Picha ya Juma Akishauriwa na Baba Yake (*Wema wa Mwana* Uk. 3)**


Katika ukurasa wa 4, Mamake Juma pia anaonesha kupendezwa na elimu kwa kushikilia msimamo kama wa Baba Juma wa kumtaka Juma atie bidii masomoni. Hili linaonekana anapomwangalia Juma kwa macho makali huku Juma akionekana mwenye kuvunjika moyo kwa mashauri makali anayopewa.



**Kielelezo 4.8: Picha ya Juma Akishauriwa na Mama Yake (*Wema wa Mwana* Uk. 4)**


Kwenye picha katika ukurasa wa 13, Baba ya Ngoyoni anaamua kumpeleka Ngoyoni katika shule ya bweni ili asaidiwe kurekebisha tabia. Baada ya kufika shuleni, mwalimu mkuu wa shule ya Masomoni anawakaribisha Ngoyoni na wazazi wake na kuwahakikishia kuwa shule yao ni mahali pa masomo, adabu njema, kuwajibika na kumcha Mungu. Mwalimu

mkuu pia anaahidi kuongea na Ngoyoni ili abadilishe tabia yake. Hii ni sehemu muhimu ya elimu.




**Kielelezo 4.9: Picha ya Mwalimu Mkuu Akiwalaki Ngoyoni na Baba Yake (*Wema wa Mwana* Uk. 13)**

Mwalimu mkuu anatimiza jukumu lake katika kuendeleza elimu kama inavyoonekana katika picha kwenye ukurasa wa 18 ambapo anaonekana akimshauri Ngoyoni wakiwa ofisini kwake. Anapitia pamoja na Ngoyoni sehemu mbalimbali za matokeo ya masomo yake na kumshauri namna ya kuyaboresha. Kwa njia hii, mwalimu huyu katika Shule ya Msingi ya Masomoni anatunza wanafunzi katika shule hii kama mzazi kwa sababu ameachiwa jukumu hilo na wazazi wao. Matokeo ya kazi yake yanadhihirika wazi mwishoni mwa muhula ambapo Ngoyoni anakiri wazi kuwa tabia yake imebadilika kutokana na mafunzo aliyopata katika shule hii. Pia, ameboresha matokeo yake darasani.



**Kielelezo 4.10: Picha ya Ngoyoni Akishauriwa na Mwalimu Mkuu (*Wema wa Mwana* Uk. 18)**

Baada ya kutia bidii masomoni, Ngoyoni anaibuka mwanafunzi bora muhula ule katika darasa lake. Hili linamfanya ajiamini na kutia bidii hata zaidi. Matokeo ni kuwa aliacha hata ukorofi wake na akawekwa kama kiranja katika darasa lake kama inavyoonekana katika picha kwenye ukurasa wa 19. Anavishwa nembo iliyoandikwa Kiranja na mwalimu wake huku mwalimu mkuu na wanafunzi wengine wakitazama na kushangilia. Hili linamfanya Ngoyoni kusema: "Nimejua maana ya nidhamu. Nimejua namna ya kuishi na ndugu, wazazi na walimu wangu bila ukorofi wowote…" (Uk. 19) Kwa sababu hii, Ngoyoni anaheshimiwa na wanafunzi wenzake na anachochewa kutia bidii zaidi katika masomo yake ili kudumisha heshima hiyo.



**Kielelezo 4.11: Picha ya Ngoyoni Akivalishwa Nembo ya Mwanafunzi Bora *(Wema wa Mwana* Uk. 19)**

Kupitia kwa picha, pia tunaoneshwa jinsi wazazi wanavyopitisha elimu kwa wanao. Hii inapitishwa kwa hadithi wanazotambiwa watoto na wazazi, nyanya au babu zao. Hili linaonekana kupitia kwa picha kwenye ukurasa wa 2 na 3 (tazama kielelezo 4.11) ambapo Kido na nyanyake wanakula huku wakitambiana hadithi.



**Kielelezo 4.12: Picha ya Kido na Nyanyake Wakila na Kutambiana Hadithi (*Kisasi Hapana* Uk. 3)**

Elimu ya ziada kupitia kucheza pia inaoneshwa katika ukurasa wa 24 katika riwaya ya *Nimefufuka* (tazama kielelezo 4.3) ambapo tuna wanafunzi wasichana wakiwa katika uwanja wa michezo wakicheza kandanda. Wasichana hawa tunaambiwa wamechezea shule yao hadi viwango vya wilaya na mkoa. Hii ni elimu inayoendeleza vipawa vya wanafunzi na inaweza kuwafaa katika kupata ajira siku za usoni. Pia, picha katika ukurasa wa 26-27 inaonesha jinsi watoto wanavyopenda mpira na kuushabikia kweli. Kido anasema akiambia baba yake "…acha nikupe taarifa kemukemu kwamba siku hizi wasichana nao wanacheza kandanda shuleni mwetu. Timu yetu ya shule ina wanasoka wasichana hodari sana."

### 4.3.3 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu katika Fasihi ya Watoto

Katika kuendeleza maudhui ya nidhamu, waandishi hawa wametumia tashbihi, methali, misemo, nahau, taswira na picha. Vipengele hivi vimetumiwa kwa njia tofauti na kila mwandishi katika kuendeleza maudhui ya nidhamu.

#### 4.3.3.1 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu

Mwandishi wa *Wema wa Mwana* ameliweka swala la nidhamu wazi kupitia kwa Mama Juma anapomkashifu Juma anapogundua kuwa ana tabia ya kuiba chakula kutoka jikoni badala ya kukaa na kusoma. Hili limeathiri matokeo yake katika mtihani. Anapogunduliwa, mwandishi anatumia tashbihi kadha kuonesha mwitiko wa Juma. Anasema:

> "Alishindwa kusema lolote. Uso ulimtuma. Macho yalilegea kama ya ndulele. Mwili ulilainika kama aliyezaliwa jana. Machozi yalimlengalenga asiwe na la kusema. …Woga ulimvaa Juma mwili mzima. Wasiwasi ukampanda kwamba huenda baba atamchapa. Alianza kutetemeka kama kuti la mnazi" (Uk. 11).

Maana inayojitokeza katika tashbihi "kulegea kama ndulele" na "kulainika kama aliyezaliwa jana" ni kutazama chini kwa aibu, kutetemeka na kutokwa na machozi. Hili linaonesha kuwa Juma alijua msimamo wa wazazi wake kuhusu uzembe shuleni na tabia yake mbaya ya kuiba chakula kutoka jikoni. Kuna uwezekano kuwa aliwahi kushauriwa kuhusu tabia hii na ndio sababu anaaibika. Tendo lake linaonesha anatubu kwa kosa ambalo

bila shaka alikuwa amekwishakanywa alipokuwa anatiwa nidhamu. Lakini inasikitisha kuwa bado anaendelea na tabia hii mbaya. Hii ni ishara ya ukosefu wa nidhamu.

Ngoyoni ambaye ni mtoto wa jirani ya akina Juma pia ana tatizo la utovu wa nidhamu. Baba ya Ngoyoni anaonelea kuwa shule ya bweni ya kurekebisha tabia ndiyo suluhisho kwa tatizo hili kwa sababu yeye binafsi amejaribu kumuasa akashindwa. Anasema hivi:

> "…Nimechoka kabisa. Kesho napanga kumpeleka katika Shule ya Masomoni ya kurekebisha tabia. Huko atafunzwa adabu. Atanyooka kama mlingoti. Akirudi hapa nyumbani atakuwa na heshima zaidi" (Uk. 13).

Kwa kutumia tashbihi "atanyooka kama mlingoti" tunaoneshwa matokeo mema ambayo baba ya Ngoyoni anatarajia kuwa mwanawe atakuwa nayo baada ya kuadilishwa. Mlingoti ni mti unaotokana na mkonge na huwa haujikunji hata kidogo. Inamaanisha kuwa Ngoyoni atakuwa amefunzwa nidhamu vizuri. Katika *Nimefufuka,* ukosefu wa nidhamu unatokea pale ambapo Lena anamkosea mamake heshima alipoenda kumtafuta Mwambao. Alipompata alikuwa akifukuzana na wanaume. Mwandishi anadokeza sababu ya msichana huyu kujiona kuwa wa maana sana kiasi cha kukosa nidhamu kwa kutumia tashbihi mbili. Anasema:

> "Lena alikuwa mrembo kama malaika na hili likamfanya kuwa mwingi wa maringo kama tausi" (Uku. 2).

Katika tashbihi hii, tunapata kuwa Lena alikuwa mrembo wa kufananishwa na malaika ambao ni viumbe wa kimbingu wanaoaminiwa kuwa bila dosari yoyote. Urembo wake ulimfanya kupendwa na wanaume wa kila nui na hili likamfanya kuwa na kiburi na kukosa heshima kiasi cha kumpuuza mamake mzazi. Huu ni utovu mkubwa wa nidhamu. Kisha maringo yake yanafananishwa na ya tausi. Tausi ni ndege mwenye rangi za kupendeza na hutembea kwa madaha na kuonesha rangi zake kwa kupanua mkia wake. Hili huonwa kama maringo na matembezi ya Lena yanafananishwa na tendo hili.

#### 4.3.3.2 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu

Nuhu Bakari, katika *Wema wa Mwana* ametumia misemo katika kufanikisha maudhui ya nidhamu kwa kutuonesha jinsi watoto wa siku hizi kwa jumla wanavyokosa nidhamu. Baba Juma anasema:

> "Usijali baba Ngoyoni, hawa watoto wa siku hizi adabu imewapungukia kabisa" (Uk. 12).

Kwa kutumia msemo huu "adabu imewapungukia" inakuwa wazi kuwa suala la utovu wa nidhamu limekithiri na si tatizo la Juma peke yake. Msemo huu unadokeza kuwa watoto wengi wa siku hizi hawana nidhamu. Kwa hiyo, ni kama wazazi hawa wanaliwazana na hivyo wanafaa kuchukua hatua za kurekebisha tatizo hili katika familia zao. Hata hivyo, wazazi hawa wanatofautiana katika maoni ya jinsi ya kutia watoto hawa nidhamu. Baba Juma anashabikia kuwa wazazi wenyewe waweze kuongea na wanao ili kuwatia nidhamu kwani wao wenyewe ndio wenye jukumu la kuwafunza wanao tabia njema. Mke wake anakiri kuwa wamefanikiwa kusaidia wana wao wengine kwa njia hii. Baba Ngoyoni kwa upande wake anahisi kuwa njia nzuri ya kumrekebisha mwanawe ni kumpeleka katika shule ya kurekebisha tabia. Anaonesha tamaa yake kwa kusema:

> "Huko atafunzwa adabu" (Uk. 13).

Baada ya kupelekwa katika shule hii, Ngoyoni anapata matokeo mema na mwandishi anasema hili kupitia kwa msemo:

> "Lakini sasa nina imani kwamba siwezi kufanya hivyo tena" (Uk. 19).

Kupitia kwa msemo huu,"nina imani" Ngoyoni anatoa hakikisho kuwa amebadilika na kuwa hawezi kuwa mwenye utovu wa nidhamu tena. Kwa hiyo, njia zote mbili za kutoa nidhamu zina matokeo mema na ni juu ya kila mzazi kuchagua njia anayohisi itamfaa mtoto anayesaidiwa.

#### 4.3.3.3 Methali Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu

Methali zimetumiwa kuendeleza maudhui ya nidhamu katika *Wema wa Mwana*. Kwanza, Babake Juma anakashifu tabia ya Juma ya kuiba chakula kutoka jikoni kwa kutumia methali. Mwandishi anasema:

> "Mwana akililia wembe mpe. Kama wewe ulitaka maumivu kilio cha nini?" (Uk. 12).

Methali hii inaonesha kuwa tabia hii ilikashifiwa katika familia yao. Baba Juma anazidi kumshauri kwa uchungu na kumuasa ili aachane na tabia hii mbovu kwani anawaaibisha. Mama Juma kwa upande wake, anavunjika moyo kwelikweli na mwandishi anatumia methali kuelezea majuto haya kwa kusema:

> "Alishangaa ikiwa yeye kama mama alikuwa ameshindwa na malezi. Kumbe kuzaa si kazi, kazi ni kumlea mwana!" (Uk. 11).

Maelezo haya yanaonyesha kuwa Mama Juma alikuwa amemkanya mwanawe mara kadhaa dhidi ya tabia mbaya ya kuiba vyakula jikoni. Mama huyu anaelekea kuvunjika moyo kwa kushindwa kumrekebisha mwanawe Juma.

Katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri*, methali zimetumiwa kuonesha ukosefu wa nidhamu ya mhusika Jose. Aidha, Jose ambaye ni ndugu ya Lena na Sikitu anajiingiza katika ulevi na wizi. Wazazi wake wanashindwa kumdhibiti na wanasalimu amri. Hili linadhihirishwa kwa kutumia methali:

> "Maisha ya kufukuzana na kulazimisha yakawashinda wazazi. Wakamwacha afunzwe na dunia. Nayo dunia imetimiza jukumu hilo" (Uk. 14).

Ingawa wazazi hawa wanasalimu amri kwa kuacha kujaribu kumsaidia, kuna uwezekano kuwa wazazi hawa walianza kufukuzana na Jose ili kumkosoa kuhusu ulevi kwa kuchelewa na hivyo wanakata tamaa na kumwacha aendelee na maisha yake. Anazidi kuwa mlevi zaidi na hata kushindwa kudhibiti maisha yake mwenyewe. Lena kwa upande wake anakosa nidhamu kwa kumpuuza mamake aliyemzaa. Anafanya hivi kwa sababu hakufunzwa vema

na wazazi wake. Matokeo ya ukosefu wake wa nidhamu yanadhihirishwa kupitia kwa methali anayoitumia shangazi yake anaposema:

> ‘Kurejelea mbwembwe za Lena ni kumaliza wakati. Alivuna alichopanda kwa kufukuzana na maisha” (Uk. 19).

Methali “alivuna alichopanda” inamaanisha kuwa mbali na kufunzwa na wazazi, mtu pia huwa na jukumu la kujitia nidhamu na kujiamulia jinsi maisha yake yatakavyokuwa. Kwa sababu hii basi, mtu hujutia sababu zake za kujiingiza katika utovu wa nidhamu. Matokeo ya utovu wa nidhamu wa Lena ni kuwa alipata ugonjwa wa Ukimwi ambao hatimaye ulisababisha kifo chake. Kutokana na visa hivi viwili vya ukosefu wa nidhamu, ni kama mwandishi anatuambia kuwa malezi yanayopitishwa na wazazi yana sehemu kubwa katika kuamua nidhamu ya hatimaye ya mtoto. Anatumia methali kusema hivi:

> “Malezi ni hoja tata. Haina jibu kamili. Ingawa methali inasema mtoto umleavyo ndivyo akuavyo….”’ (Uk. 20).

Wazazi wa watoto hawa wawili, Lena na Jose wanalaumiwa kwa kuwadekeza na kukosa kuwapatia mwelekeo ufaao maishani. Wanaishia kuwa makahaba na walevi wa kupindukia.

#### 4.3.3.4 Taswira Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu

Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia taswira ili kufanikisha maudhui katika kazi yake. Kupitia kwa taswira ya uoni na hisi, tunaelezwa jinsi jioni moja baada ya kutoka hospitalini, mama na nyanya ya Kido walikuwa wamechoka kumbeba na wakaketi chini ya mti ili wapumzike hadi giza likaingia. Baada ya muda waliona taa za gari likielekea walikokuwa. Mama ya Kido aliamua kulisimamisha na kuomba msaada. Baada ya dereva huyu kusimama alitoa mshipi kiunoni mwake na kuanza kumcharaza mama ya Kido vibaya hadi akazirai. Huu ni utovu wa maadili kwa sababu mtu mwenye nidhamu hawezi kumpiga mja kwa kuomba msaada. Badala ya kumpiga kwa kuhisi kuwa hataki kusaidia, angempuuza tu na kupita. Hili limechagizwa kutumia kipengele cha picha kwenye ukurasa wa 8.

Kwenye ukurasa wa 5 wa *Nimefufuka*, tunapewa taswira katika hospitali inayodhihirisha utovu wa nidhamu kwa wagonjwa kukosa kuzingatia utaratibu. Utovu huu wa nidhamu unamwambukiza nyanya ya Kido ambaye naye anaamua kuvunja sheria na kuingia ndani ya chumba cha daktari bila kufuata utaratibu wa foleni. Tunachorewa taswira ya uoni ya hospitali iliyo na foleni ndefu sana na foleni hii haisongi kisa na maana watu wengine waliojuana na mlinzi walikuwa wakiruka foleni huku walio kwenye foleni wakibaki bila kuhudumiwa. Nyanya ya Kido alipoona hivyo, akaamua kumchukua Kido na kuingia naye ndani ya chumba cha daktari kwa nguvu almuradi mjukuu wake atibiwe. Mlinzi alipojaribu kumzuia, daktari anaingilia kati na kutaka kuona mgonjwa. Hii ni ishara kubwa ya ukosefu wa nidhamu.

#### 4.3.3.5 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Nidhamu

Kwenye ukurasa wa 24 wa *Kisasi Hapana,* (tazama kielelezo 4.3) tunawaona wasichana wakiwa katika sare zao wakicheza mpira wa miguu uwanjani kwa madaha. Tunaambiwa kuwa wasichana hawa wamecheza hadi kiwango cha kitaifa. Mchezo wowote ule unahitaji nidhamu ndipo mchezaji aweze kufuzu kwa sababu nidhamu inamsaidia mtu kuwa makini katika kufanikisha jambo analonuia kutimiza. Kwa hiyo, nidhamu ya wasichana hawa inawawezesha kufaulu kwa kiwango kikubwa. Hili pia linaonekana katika ukurasa wa 26-27 ambapo akina Kido nao wanacheza uwanjani kwa umoja wakifurahia na hii ni dalili nzuri ya nidhamu.



**Kielelezo 4.13: Picha ya Kido na Wenzake Wakicheza (*Kisasi Hapana* Uk. 26)**

#### 4.3.4 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano katika Fasihi ya Watoto

Maudhui ya ushirikiano yameendelezwa katika riwaya hizi nne kupitia kwa nahau, misemo, methali na picha. Kila mwandishi ametumia vipengele hivi vya fani kwa njia yake ili kuendeleza maudhui ya ushirikiano.

##### 4.3.4.1 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano

Katika kuendeleza maudhui ya ushirikiano, mwandishi wa *Wema wa Mwana* anatumia nahau kutuonesha hali kuwa Baba Juma na Baba Ngoyoni wanashirikiana wanapompeleka Ngoyoni katika shule ya Masomoni. Katika shule hii, Ngoyoni anajifunza tabia njema na kubadili mwelekeo wake kuhusu maisha. Baba Juma anatiwa moyo na matokeo haya mazuri na kufikiria kumpeleka mwanawe katika shule hii pia. Mwandishi anatumia nahau kuonesha hili. Anasema:

> "Baba Juma aliona gere" (Uk. 15).

Huu ni wivu mzuri kwa sababu unamsukuma Baba Juma naye pia kumpeleka mwanawe katika shule hii anakosomea Ngoyoni akiwa na matumaini kuwa Juma naye angepata matokeo mema. Kwa hiyo, wivu huu unaofaa unamsukuma mzazi huyu kuiga mwenzake na kwa njia hii kuendeleza moyo wa ushirikiano. Katika *Nimefufuka*, nahau imetumiwa kuendeleza maudhui ya ushirikiano ambapo Mama ya Lena wanashirikiana na Musa kumtafuta Lena mara kadhaa na kumpata ingawa Lena anakataa kuongea nao. Haya yanadhihirishwa kupitia nahau. Kwa mfano:

> "Shemejiyo alifunga safari ya pili hadi Mombasa. Wakati huu alikuwa mwingi wa matumaini" (Uk. 4).

Nahau hizi mbili "kufunga safari" na "mwingi wa matumaini" zimetumiwa kudhihirisha hali hii ya Mama Lena kumtafuta mwanaye kwa udi na uvumba na alipompata. Lena alipokataa kuongea naye, mwandishi anatumia nahau na anasema hivi:

> "Mama alipigwa na butwaa asijue la kusema" (Uk. 4).

Mama huyu anashangaa sana akiwazia juhudi alizofanya ili kumfikia Lena lakini alivunjika moyo sana binti yake anakataa kuongea naye. Kwa njia, hii Lena anakosa kushirikiana na mama yake ili amwokoe kutoka katika lindi la ufuska aliloingia.

Nahau nyingine inatumiwa kudhihirisha umoja na hivyo kuendeleza maudhui ya ushirikiano. Mwandishi anasema:

> "Wazee wa ukoo wakaketi chini na kusema ilikuwa mwiko mwana wao kuzikwa Mwambao kama mnyama asiye na wa kwao" (Uk. 8).

Baada ya kusema maneno, "ilikuwa mwiko mwana wao kuzikwa Mwambao" wanachangisha pesa za kutosha kulipia gharama ya kumtoa Sikitu alikofia hadi akazikwa kwao nyumbani. Wanajamii pia wanashirikiana kuzungumza na baba ya Lena na mama yake ili waboreshe maisha yao.

#### 4.3.4.2 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano

Katika *Kisasi Hapana*, msemo umetumiwa kuendeleza maudhui ya ushirikiano pale ambapo baada ya kutoka hospitalini, Kido anabebwa kwa baiskeli na jirani yao Bwana Lukoko. Bwana Lukoko anampeleka kwake ambapo mke wake alimpokea kwa ukarimu. Msemo umetumiwa kudhihirisha hili. Kido anasema:

> "Alinipokea kwa moyo mkunjufu" (Uk. 10).

Hili lilimpendeza sana Kido kwa sababu alikuwa akitapika na mke huyu wa jirani hakuonesha kuchukizwa naye. Pia, ulikuwa ni muda mfupi tangu Kido alipokuwa ameshuhudia mamake akipigwa vibaya na dereva wa mkuu wa wilaya kwa kuomba msaada. Kwa hiyo, tendo hili la mke wa jirani linamkumbusha kuwa bado kuna watu wenye utu na wako tayari kushirikiana kumsaidia Kido apate afueni kutokana na ugonjwa wake.

#### 4.3.4.3 Methali Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano

Katika *Nimefufuka*, majirani wa Sikitu wanatumia methali mbili na kusema:

> "Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Msipojirekebisha maisha yatakwenda kombo na hamna mtakayelaumu. Udongo upate uli maji. Bwana Simba, punguza ulevi na ujenge tena mji wako". (Uk 26).

Kupitia kwa mashauri haya, "Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo" na "Udongo upate uli maji" wazazi wa Sikitu wanaambiwa waanze haraka kufikiria namna ya kujikwamua kutokana na mawazo mabaya juu ya matatizo waliyo nayo. Hatimaye wanafaulu kwa kiasi fulani kushinda majuto ya kutotimiza madaraka yao kama wazazi na upweke.

#### 4.3.4.4 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Ushirikiano

Umuhimu wa ushirikiano unaonekana waziwazi katika riwaya ya *Wema wa Mwana* kupitia kwa matumizi ya picha kwenye ukurasa wa 3 na 4 (tazama kielezo 4.7 na 4.8) ambapo wazazi wa Juma wanashirikiana kumshauri Juma atie bidii masomoni. Babake ndiye wa kwanza kumfokea kwa kutotia bidii. Juma anapoenda kwa mamake ili amtetee, anashangaa kuwa hata mamake anasema maneno yaleyale aliyomwambia babake. Hii ni ishara ya ushirikiano wa wazazi wa Juma ambao wanaongea kwa sauti moja katika kumkosoa mwanao. Juma na mama yake wako jikoni na mamake anamshauri kwa ukali na hili linaonekana kumkera Juma ambaye anaonekana kukasirishwa.

Katika ukurasa wa 9, watu wote wa familia ya akina Juma wanashirikiana kumkosoa Juma kutokana na tabia yake ya kuiba chakula jikoni. Hata wadogo zake wanasema waziwazi kuhusu tabia ile ili apate msaada. Wanaonekana kumzunguka na kumsikitikia kwa yaliyompata na kumsaidia. Kwenye picha katika ukurasa wa 12, wakati baba ya Ngoyoni anapohisi kuwa ameshindwa na tabia ya Ngoyoni, anamtembelea baba Juma kutafuta maoni yake kuhusu hatua anayopanga kuchukua ya kumpeleka Ngoyoni katika shule ya kurekebisha tabia. Baba Ngoyoni anaonekana mwenye huzuni na kuvunjika moyo huku baba Juma akionekana kumsikitikia na kumshauri. Hii ni ishara kuwa jamii hii inashirikiana kwa kushauriana kunapokuwa na uhitaji.

Baba Juma na Baba Ngoyoni wanaandamana pamoja kumpeleka Ngoyoni shuleni na hii ni ishara ya ushirikiano katika jamii. Hata muhula unapoisha tunaona kwenye ukurasa wa 15 wazazi wa Ngoyoni na baba Juma wakionesha ushirikiano kwa kumpokea Ngoyoni kutoka shuleni. Walimu pia wanashirikiana kusaidia watoto. Hili linaonekana wazi wakati wa kumtawaza Ngoyoni kuwa kiranja katika darasa lake. Ngoyoni anaripoti hivi: "Mwalimu mkuu alikuwa darasani siku hiyo kuja kushuhudia kupandishwa ngazi kwangu." Hili pia linaonekana katika picha kwenye ukurasa wa 19 mwalimu mkuu akiwa amesimama na mmojawapo wa walimu anamvisha Ngoyoni nembo ya kuwa kiranja katika darasa lao. Ushirikiano huu unazidi kuonekana wakati wazazi wa Juma wanapomwalika Ngoyoni kueleza vile hali ilivyo kule shuleni Masomoni. Kwa njia hii, wanamshawishi Juma naye pia kujiunga na Ngoyoni kule shuleni kwao ili kuzidisha ushirikiano wa familia hizi mbili.

Katika *Kisasi Hapana*, picha inatumiwa kudhihirisha ushirikiano pale ambapo Kido anakuwa mgonjwa na nyanya yake na mama yake wanashirikiana kumpeleka hospitalini. Wanafanya hivyo kwa kupokezana kumbeba mgonjwa wao kwa umbali wa kilomita kumi na saba. Kama inavyooneshwa katika picha kwenye ukurasa wa 9 (tazama kielelezo 4.14).



**Kielelezo 4.14: Picha ya Kido akiwa amebebwa na nyanya, mama na Lukoko (*Kisasi Hapana* Uk. 10)**

Picha katika ukurasa wa 8 inaonesha jinsi Nyanya ya Kido akidhani kuwa kila mtu atashirikiana kusaidia mgonjwa, anamsimamisha dereva wa gari fulani awaokoe. Huyu dereva anaishia kumpiga nyanya ya Kido vibaya na hatimaye kufanya mipango ya kumshambulia na hata kumuua. Hili ni funzo kuwa si kila mtu ni ndugu. Kinyume kabisa na dereva huyu, mke wa Lukoko kwa upande wake anampokea Kido kwa moyo mkunjufu na kumwosha alipofikishwa katika nyumba yake usiku ule akiwa mgonjwa. Hata Kido alipotapika alimpangusa na kumhudumia hadi wazazi wake walipofika. Picha kwenye ukurasa wa 10 nayo inaonesha jirani yao, mzee Lukoko akiwasaidia kwa kumbeba Kido kwenye baiskeli yake. Baadaye, Lukoko anawaongoza majirani ili kuchangisha pesa ili wamnunulie Kido dawa alizohitaji. Wanamtunza hadi anapata afueni na huu ni ushirikiano wa kupendeza sana.

Picha kwenye ukurasa wa 17 inaonyesha ushirikiano pale ambapo majirani wanamiminika nyumbani kwa akina Kido nyanyake anapokufa ili kuwafariji. Inaonekana kuwa nyanya yake Kido aliishi pamoja na familia ya akina Kido na hivyo kushirikiana katika kila jambo pale nyumbani. Nyanya huyu aliwasaidia katika kutunza wagonjwa, kupika na kufundisha watoto. Hili linadhihirishwa wazi wakati nyanya ya Kido pamoja na Kido wakiwa mezani na kula pamoja katika ukurasa wa 3. Picha katika kurasa za 24, 26 na 27 (tazama kielelezo 4.13) zinazoonesha kuwa katika kucheza mpira na michezo mingine, watoto walishirikiana ili kupata magoli na kufurahia mchezo wao. Hata hivyo, kuna ushirikiano mbaya katika riwaya hii pale ambapo watu wa ukoo na marafiki wa yule dereva wa mkuu wa wilaya wanashirikiana kumkatakata kwa panga nyanya ya Kido na kumuua wakiamini kuwa yeye ndiye aliyemfanya dereva kupata ajali na kuumia vibaya. Wezi pia katika ukurasa wa 20 na 21 wanashirikiana kushambulia akina Kido na kuwanyang’anya ng’ombe wote kisha wanamteka nyara Salama, dada ya Kido na hili linaongezea familia hii majonzi makubwa.

### 4.3.5 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii katika Fasihi ya Watoto

Katika kuendeleza maudhui ya bidii, waandishi hawa wanne wametumia nahau, misemo, tashbihi na picha.

#### 4.3.5.1 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii

Katika *Sitaki Iwe Siri*, tunagundua kuwa Musa hakutaka kumwaibisha mwalimu wake kwa sababu alikuwa anahisi kuwa mwalimu huyu alikuwa na imani katika uwezo wake. Baada ya kuanza kazi hii, ni wazi kuwa Musa anatia bidii ili insha yake iweze kufuzu katika shindano hili. Bidii yake inaoneshwa kutumia nahau inayosema kuwa:

> " (Musa) Alijifunga kibwebwe kushiriki kwenye shindano hilo" (Uk. 21).

Hapa "kujifunga kibwebwe" inamaanisha kuwa alitia bidii sana ili kutimiza mradi wa kuandika insha. Baada ya kuandika insha hii, bado Musa hachoki katika kuhakikisha kuwa kila kitu kiko sawa na kabla ya kuitumbukiza insha yake katika posta ili iwafikie watahini, tunaambiwa kwa kutumia nahau kuwa:

> "Baada ya kuhakikisha kwamba insha yake imepigwa msasa aliomba nyanya yake pesa za stampu" (Uk. 49).

Nahau "kupiga msasa" imetumiwa kumaanisha kuwa Musa alipitia tena kazi yake ili kuondoa makosa yoyote yaliyokuwamo. Tendo hili linahitaji bidii.

Katika maeneo ya kazi pia kuna wale wanaonesha bidii. Mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* anasema:

> "Kondakta alimwambia dereva ang'oe nanga" (Uk. 29).

"Kung'oa nanga" ni kuanza safari kwa hivyo kondakta anamwambia dereva aanze safari. Baada ya muda, wakati gari limeanza safari na abiria kutulia garini, ni dereva pekee anayeonekana akitimiza jukumu lake kwa bidii. Wengine wote katika gari wamenyamaza na mwandishi anadokeza hili kwa kusema:

> "Ni dereva tu aliyekuwa anamenyana na usukani" (Uk. 29).

Kumenyana na usukani na kuendesha gari. Kwa jinsi hii bidii ya dereva huyu inadhihirishwa kwani wengine wote garini walikuwa wamenyamaza wakisubiri kufikishwa wanakoenda.

Kwa kuendeleza maudhui ya bidii katika *Kisasi Hapana*, baba yake Kido, Andrea Mukulu anamsihi mtoto wake atie bidii katika kumwombea ili Mungu asikie maombi yake amtoe jela. Anasema:

> "Nitarudi hivi karibuni. Endelea kuvuta subira na kuniombea." (Uk. 39).

Anaposema "Endelea kuvuta subira na kuniombea" Babake Kido anamtaka Kido adumu katika maombi kwa bidii na subira ili Mungu amfungue kutoka jela alikofungiwa bila yeye kuwa na kosa lolote.

#### 4.3.5.2 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii

Tashbihi zimetumiwa katika kuendeleza maudhui ya bidii katika *Sitaki Iwe Siri*. Kwanza, tunampata Musa akiwa tayari kushiriki katika kuandika insha kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Mwandishi anamwonyesha Musa akijisemea na inaripotiwa kuwa:

> "Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa. Alihisi msukumo wa aina fulani ukimchochea kushiriki kwenye shindano hilo… alijitia moyo kwamba lisilo budi hutendwa" (Uk. 26).

Tashbihi "Moyo wake ulidunda kama kengele ya kanisa" inamaanisha kuwa Musa alikuwa na wasiwasi kwa kiasi fulani kuingia katika kinyang'anyiro hiki. Hata hivyo, alijifunga kibwebwe na kuamua kujaribu kwa sababu alishakubali mbele ya mwalimu wake mkuu na hivyo akajitahidi ili ampendeze. Katika riwaya hii ya *Sitaki Iwe Siri*, bidii inaonekana katika maeneo mengine mbali na nyumbani na shuleni. Hili linadhihirishwa kwa matumizi ya tashbihi kuhusu shughuli za wafanyabiashara. Mwandishi anasema:

> "Kituo cha biashara cha Mwembe Tayari kilikuwa na shughuli nyingi kama za nyuki mzingani" (Uk. 28).

Kuwa na "shughuli nyingi kama za nyuki mzingani" ni ishara kuwa kila mtu alikuwa ameshika kazi yake kwa bidii. Katika matatu inayowabeba Musa na dada zake, kuna kondakta anayefanya kazi yake kwa bidii na tashbihi inatumiwa kudhihirisha hili:

> "Utingo naye alikazana kama siafu kukusanya nauli kutoka kwa abiria" (Uk. 29).

Mwandishi anaendelea kusema hivi kuhusu mkono wa kondakta:

> "Mkono wake ulioonekana kukauka kama kibanzi cha ukuni" (Uk. 30).

Hili ni dhihirisho kuwa utingo amefanya kazi hii kwa muda na kufanya mwili wake kukauka. Ni ishara ya bidii katika kazi hii. Kuhusu magari ya kubeba wagonjwa, tunaambiwa hivi:

> "Magari hayo yaliingia kwa kasi kama umeme kupitia lango kuu" (Uk. 31).

Katika *Kisasi Hapana*, Kido anahisi kuwa ile bidii aliyo nayo ni ishara ya nguvu na kuwa anaweza hata kuvunja miti ya simu ipitayo kwao kwa njia rahisi tu. Anasema:

> "Nafikiri hata nikila nikashiba naweza kuzivunja kama kijiti kidogo au sio" (Uk. 31).

Babake Kido naye anamtia Kido moyo ili atie bidii katika masomo jinsi anavyofanya katika mchezo wa kandanda. Anasema:

> "Usichukie kusoma. Penda kusoma kama vile unavyopenda michezo. Kila kimojawapo ya vitu viwili hivi, kina umuhimu wake. Michezo inaweza kukupa sifa, labda pesa, kama zile wapatazo baadhi ya wanariadha na wanasoka wa kulipwa kutoka nchi kadha Barani Afrika" (Uk. 37).

Hapa, Mkulu analinganisha michezo na masomo na hivyo kumsihi mwana wake apende masomo pia na kwa kufanya hivi atafaidi kutokana na yote mawili.

**4.3.5.3 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii**

Katika *Sitaki Iwe Siri*, misemo inatumiwa kuendeleza maudhui ya bidii kwa kutuchorea jinsi Musa alivyotia bidii katika kuandika insha ambayo ingeshiriki katika mashindano. Mwandishi anasema:

> "Alijitia moyo kwamba lisilo budi hutendwa. Ima fa ima angejizatiti kuandika mtungo ambao ungezungumziwa kwa muda mrefu" (Uk. 26).

Kupitia kwa msemo huu "Ima fa ima" tunagundua kuwa Musa alikuwa tayari kufanya yote yaliyokuwa katika uwezo wake kuhakikisha kuwa mradi wake wa kuandika insha unafaulu. Ilikuwa ni azma yake kufaulu liwe liwalo. Katika kufanikisha mradi huu, walimu wa Musa

pia wanatia bidii kumsaidia ili afuzu katika masomo na uandishi wa insha na msemo umetumiwa kuonyesha hili:

> "Walimu wake walivyojitahidi kwa hali na mali kumwelimisha ili…." (Uk. 47).

Kwa kusema walimu "walivyojitahidi kwa hali na mali", maana inayodhihirika ni kuwa walimu hawa wanamtakia Musa mema na wanajitahidi kumuelimisha. Pia walikuwa tayari kutumia pesa na uwezo wao kuhakikisha kuwa anafaulu. Bidii pia inadhihirishwa pale ambapo tunaoneshwa sehemu kadhaa za soko la Nyagacho na jinsi wahusika kadhaa wanatia bidii katika shughuli zao za kujitafutia riziki. Tunaambiwa:

> "Kulikuwa na magari yaliyojaa mizigo pomoni". "Jasho hilo lilifanya nguo zao zilowe
> chepechepe" (Uk. 28).

Msemo huu "kujaa pomoni" unadokeza kuwa bidii imefanywa ili kujaza mizigo katika magari haya na wale wanaofanya kazi hii inawabidi nguo zao zilowe kwa kutoa jasho. Kwa hiyo, wahusika hawa wanafanya bidii kutimiza sehemu zao katika ujenzi wa taifa.

#### 4.3.5.4 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Bidii

Katika *Wema wa Mwana*, kwenye kurasa za 3 na 4 (tazama kielelezo 4.8) swala la bidii limeangaziwa kupitia kwa Babake Juma kumsaili Juma ili kujua ikiwa anafanya bidii shuleni. Inadhihirika kuwa kuna ulegevu na utepetevu katika masomo kwa upande wa Juma ambapo anakiri mwenyewe kuwa alikuwa na tatizo katika masomo ya Sayansi Kimu na Hisabati. Ni wazi kuwa Juma hatii bidii kurekebisha hali yake masomoni na badala yake anatazama tu televisheni na kukaa jikoni. Wazazi wake Juma wanatia bidii kuwasaidia watoto wao kwa kuwashauri, kuwaasa na kuwatia nidhamu. Hili linaonekana wakati wazazi wa Juma wanapotumia muda kuwasaidia wanao.

Kama inavyodhihirishwa na mwalimu mkuu kwenye ukurasa wa 18 (tazama kielelezo 4.10), walimu nao wanafanya bidii kuwasaidia watoto walio mikononi mwao kutia fora masomoni na maishani. Huyu mwalimu mkuu wa shule ya akina Ngoyoni anachukua nafasi

yake na kuongea na Ngoyoni binafsi ili kumsaidia kuboresha masomo yake na nidhamu. Katika picha kwenye ukurasa wa 19 (tazama kielelezo 4.11), tunaona matokeo ya bidii ya Ngoyoni akiwa shuleni kuwa anatambuliwa na kuwekwa kama kiranja katika shule yao. Matokeo mazuri ya bidii ya Ngoyoni pia yanamchochea Juma ambaye pia anatamani kuenda katika shule anakosomea Ngoyoni ili naye awe na matokeo mema.

Katika ukurasa wa 2 wa *Nimefufuka*, Sikitu ameketi na anafanya bidii kumwandikia shangazi yake barua. Aliandika barua kadhaa ambazo shangazi yake naye alifanya bidii kuzijibu. Kupitia barua hizi Sikitu anapata mashauri mazuri yanayombadilisha maisha kabisa na kuwa bora zaidi. Mama ya Lena na Musa kwa upande wao wanafanya bidii kumtafuta Lena. Hili linaonekana katika picha kwenye ukurasa wa 4 ambapo ameandamana na Musa katika hoteli ya Bora Bora wakiwa katika harakati za kumtafuta Lena. Hatimaye picha kwenye ukurasa wa 11 inaonyesha wazi kuwa Sikitu anafanya bidii kumtunza Shujaa mtoto wa Lena. Anamwangalia na wakati ule ule anafanya kazi ya kufua nguo.

Katika picha kwenye kurasa za 26 na 27 (tazama kielelezo 4.13) za *Kisasi Hapana*, ni wazi kuwa Kido alikuwa na bidii katika michezo na ni kawaida kwake kutia bidii na kufunga mabao mengi. Siku moja walifunga mabao arobaini na saba kwa kumi na nane ya wapinzani wao. Kido anatia bidii hivi kwa sababu kucheza kandanda ni jambo ambalo anapenda kufanya na anaicheza kwa madaha akiwa na tumaini kuwa siku moja ataweza kuchezea timu za kimataifa kama Inter Milan, AC Millan, Barcelona na kadhalika. Kwa njia hii, ataweza kupata riziki huku akifanya kazi aipendayo sana. Wanafunzi wengine kama Salama dada ya Kido na Samueli wanatia bidii ya mchwa na kufuzu vema katika masomo na hata michezo. Salama anacheza hadi kufikia kiwango cha wilaya na bado alifanya vizuri sana katika darasa. Hili ni wazi kupitia kwa picha kwenye ukurasa wa 24 ambayo inaonesha wale wasichana katika shule ya akina Kido wakicheza mpira wa kandanda kwa bidii (tazama

kielelezo 4.3). Hata baada ya kuvunjika mguu, bado Kido anahakikisha kuwa anafika uwanjani ili kujionea mchezo anaoupenda sana. Hii ni ishara ya bidii yake katika michezo.

### 4.3.6 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike katika Fasihi ya Watoto

Katika kumulika maudhui ya nafasi ya jinsia ya kike, waandishi hawa wametumia vipengele vya fani kama misemo, tashbihi, taswira, nahau na picha.

#### 4.3.6.1 Misemo Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike

Rebecca Nandwa ametumia misemo katika *Nimefufuka* kwa kumsawiri mwanamke kama chombo cha mzinduko na mabadiliko. Sikitu anamshauri shangazi kuwa akishinda kiti cha udiwani, apiganie maslahi ya wanawake. Anazidi kumwomba kuwa ashirikiane na wananchi hasa kina mama kubuni mikakati ya kuwakomboa kutokana na minyororo ya utamaduni. Shangazi yake anaonesha nia ya kusaidia kwa kutumia msemo na kusema kuwa:

> "Nimejitolea kukusaidia kwa hali na mali" (Uk. 15).

Katika msemo huu "kwa hali na mali", ni wazi kuwa mwanamke ana azma ya kufanya mengi sana ili kujikomboa mwenyewe na kuhakikisha kuwa wanawake wenzake wanaheshimiwa. Mwanamke pia amejidhihirisha kama mshauri mwema. Tunamwona Sikitu akimwambia shangazi yake kuwa:

> "Kama ulivyonifaa, mjomba humpa mama moyo wa kujikakamua zaidi" (Uk. 15).

Kutokana na maelezo haya, tunapata kuwa mashauri ya shangazi ya Sikitu yamezaa matunda kwa sababu baadaye mama huyu anakuwa na furaha na kuanza kujitunza na kutunza familia yake.

#### 4.3.6.2 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike

Katika *Kisasi Hapana*, mama ya Kido na nyanya yake wamechorwa kama wanawake wenye mapenzi na bidii katika kazi zao. Wanatia bidii kumpeleka Kido hospitalini huku

wamembeba mgongoni kwa umbali wa kilomita nane. Kido pia anasifu mapishi yao ya hali ya juu kwa kutumia tashbihi anaposema:

> "Nyanya alikuwa mpishi bora. Mpishi bora kama mama" (Uk. 2).

Hii ni ishara tosha kuwa jinsia ya kike inadhihirisha mapenzi na bidii katika shughuli zao za kila siku. Aidha, msichana anaoneshwa kuwa mtu hodari katika masomo. Salama anaheshimiwa na ndugu yake kwa uwezo wake mkubwa darasani. Kido anatumia tashbihi kuonesha huu uhodari wake kwa kudai:

> "Salama ni aina ya mwanafunzi ambaye kwake yeye kuwa nambari moja darasani ni kawaida kama watu kufumba macho wanapolala" (Uk. 17 ).

Kwa sababu hakuna nguvu inayohitajika ili kufumba macho, basi ni wazi kuwa Salama alikuwa mwerevu hivi kwamba hakuhitaji kuzama vitabuni ndipo apite mtihani.

#### 4.3.6.3 Taswira Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike

Katika *Sitaki Iwe Siri*, taswira zimetumiwa kuendeleza nafasi ya jinsia ya kike na mwanamke amechorwa kama mwenye bidii akiwakilishwa na Mwalongo anayefanya juu chini kuwatunza wajukuu wake. Kuhusu umri na hali yake, mwandishi anatuchorea taswira kuwa Nyanya Mwalongo alikuwa na umri wa miaka sitini hivi. Nywele zake kichwani zilikuwa zimebadilika na kuwa nyeupe kama theluji. Mwili wake ulikuwa umevamiwa na makunyanzi kwa sababu ya uzee. Mgongo wake ulikuwa umepinda kama uta na alilazimika kutembea kwa mkongojo. Licha ya hali hii, mwandishi anaeleza kuwa aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho. Hili linamaanisha kuwa alijitahidi kadri ya uwezo wake kuwatunza wajukuu wake na kuwapa malezi mema.

Kupitia kwa taswira, mwanamke amechorwa kuwa msomi. Tunamwona Bi Maria Kavoi akiwa ofisini mwake akisoma gazeti. Musa anamwomba msaada katika kuandika insha yake kuhusu Ukimwi na anamweleza namna ya kupata habari zaidi. Mashauri yake yanadhihirisha ni mwelewa wa mambo na hii ni ishara ya usomi. Anaambia Musa kuwa bila shaka insha yake itatoa mchango mkubwa iwapo atafanya utafiti wa kutosha na wa kina, sio

maktabani tu bali pia kwa kufanya mahojiano na matabibu na hata wagonjwa wanaougua Ukimwi hospitalini.

Mbali na kuwa msomi, Bi Kavoi pia ni dhihirisho la mwanamke ambaye ni mshauri mwema kwa jinsi anavyomwelekeza Musa katika utafiti wake. Anamshauri kuwa huenda maktaba ya shule isimfae kwani haina vitabu wala majarida yatakayomsaidia katika utafiti wake. Anamshauri kutembelea maktaba ya umma. Huenda ikamfaa zaidi. Kwa upande wao, manesi kule hospitalini licha ya kuwa wasomi, ni wawajibikaji na wahisani. Hili linadhihirika wazi wakati wa tukio fulani la dharura kule hospitalini. Tunaambiwa nesi waliokuwa wamevaa sare nyeupe pe pe pe na karatasi, umbo la sambusa mbili zilizotulia dede kichwani walifika karibu na magari yale haraka huku wanasukuma machela yenye magurudumu. Walikuwa tayari kabisa kuhudumia wagonjwa bila kushurutishwa. Waliwaondoa wanawake wajawazito haraka na kuwapeleka katika chumba cha kujifungulia. Kwa njia hii, wanadhihirishwa kuwa wasomi, wenye bidii na wenye kujali. Huu ni mfano mzuri unaompatia motisha mtoto wa jinsia ya kike.

Mwanamke pia anasawiriwa kuwa mwenye utu na mtambuzi. Kupitia taswira tunatambua jinsi nesi mmoja katika hospitali ya Nyagacho alivyo mwenye utu na utambuzi. Mwandishi anaeleza kuwa muuguzi huyu alivaa tabasamu iliyochanganyika na mshangao kwenye uso wake mpana wenye mashavu yaliyounda vidu kwa sababu ya ufasaha wa Musa katika kusema. Alivutiwa na adabu ya Musa na dada zake. Akaamua moyoni mwake kwamba liwe liwalo angewasaidia kadri ya uwezo wake.

#### 4.3.6.4 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike

Katika *Nimefufuka*, mwanamke amechorwa kuwa ni mpenda anasa. Hili linadhihirika pale ambapo Lena anaacha shule na kujiingiza katika anasa. Tunaambiwa:

> "Dada yangu mdogo hakumaliza masomo ya shule ya upili. Alitorokea Mombasa eti kuponda maisha." (Uk 2).

“Kuponda maisha” ni kula raha kwa kujiingiza katika anasa. Raha hii anaiponda kwa kujiingiza katika mapenzi na wanaume. Hata anasafiri kuenda nchi za nje ili kuendeleza starehe zake. Kuhusu hili, Sikitu anaongezea nahau moja inayohusu maisha ya Lena:

> “Raha ya Lena ikawa kuabudiwa na walimwengu. Uvumi ulisema dada alifanya yanayosemeka na yasiyosemeka” (Uk. 2).

Katika mfano huu, nahau “kuabudiwa na walimwengu” imetumiwa kuonesha jinsi alivyopendwa kiasi cha kuabudiwa na wanaume waliomtaka kimapenzi. Matokeo ya maisha ya raha na anasa ya Lena yanaelezwa kwa kutumia nahau isemayo:

> “Maradhi ya Lena yaliasi dawa na kafara ingawa mimba iliendelea kukua. Aliaga dunia siku chache baada ya kujifungua mwana wa kiume” (Uk. 8).

Maisha ya raha na anasa aliyoingilia Lena yalimfanya kupata ugonjwa mbaya ambao mwandishi anatumia nahau kuueleza anaposema “Maradhi ya Lena yaliasi dawa na kafara.” Ugonjwa huu ulimsumbua hadi alipokufa na nahau inatumiwa kudhihirisha hili kwa kusema “Aliaga dunia.” Hili ni onyo kwa wasichana kuwa wanapaswa kujitunza na kujiheshimu.

Katika jamii hii ya *Nimefufuka*, kazi ya mwanamke ni kuzaa na kama hawezi analaumiwa hata ikiwa kasoro ni ya mume na hatimaye anafukuzwa. Sikitu mwenyewe anatuambia masaibu anayopitia kwa kusema:

> “Shangazi wajua nimeitwa tasa. Sikuweza kupata watoto nilipoolewa kutokana na sababu ambazo bado ni fumbo kwangu. …. wataalamu wa kunga na tiba walionikagua walisema sehemu zangu za uzazi hazina kasoro. Mume alikataa katakata himizo la kwenda hospitalini. Alisema ukosefu wa uwezo wa kupata mtoto ni shida ya mwanamke. Wanaume ni safi safina na ikiwa itatokea kasoro, hiyo ni kasoro ya mwanamke” (Uk. 8).

Hata mwanamke mwenzake alimlaumu na Sikitu mwenyewe anatumia nahau kwa kusema:

> “Mama mkwe aliniambia kinagaubaga kwamba alihitaji kuona wajukuu wake kabla mauti kumchukua …. nilijaribu kuvumilia ndimi hizo zilizonolewa kila kulipokucha na jua kutua. Niliposhindwa kustahimili matusi, nilifunganya virago na kurudi kwetu, kwenu.” (Uk. 9).

Pia, ni wazi kuwa katika jamii hii mwanamke ni mlezi wa watoto wake na mayatima katika jamii yake. Hakuna mwanamume anayeonekana kujali malezi. Jukumu hili limeachiwa

mwanamke. Mwandishi anasema hivi kuhusu Sikitu:“Baada ya mazishi ya Lena, jukumu la malezi ya kitoto chake liliniangukia” (Uk. 10). Jukumu la kulea mwana wa Lena linamwangukia Sikitu licha ya kuwa kuna watu wengine ambao wangeachiwa jukumu hili. Hata hivyo, jinsia yake ya kike inamfanya aangaliwe kama anayestahili kutimiza jukumu hili la ulezi.

#### 4.3.6.5 Picha Inavyoendeleza Maudhui ya Nafasi ya Jinsia ya Kike

Katika kuonesha nafasi ya jinsia ya kike katika *Wema wa Mwana,* Baba Juma anadai kuwa mamake Juma ni kizingiti kwa bidii ya Juma masomoni kwa kudai kuwa Juma anapoteza muda mwingi jikoni na mamake. Hata anaposhauriwa na babake, anakimbilia jikoni aliko mamake akidhani kuwa atatetewa na mamake. Hili linadhihirishwa kupitia kwa picha iliyoko kwenye ukurasa wa 3 (tazama 4.8) ambapo Juma anaonekana akizungumza na babaye. Punde tu baada ya kuongea na babake, anakimbilia kwa mamake akionekana amesononeka kwa kushauriwa na baba yake kuhusu kazi yake ya shuleni. Hata hivyo, mamake Juma anatimiza wajibu wake kwa kutilia mkazo mashauri ya baba Juma kwa Juma na kumtaka atie bidii masomoni kama ndugu zake wengine. Kwa hiyo, mama Juma anaikomboa jinsia ya kike kutokana na mwelekeo hasi wa uendekevu kwa kushirikiana na mume wake kumshauri mwanao na sio kumdekeza kama alivyodhania mume wake.

Picha kwenye ukurasa wa 16 inamwonesha mamake Ngoyoni kuwa anaunga mkono mume wake katika kumsaidia Ngoyoni. Hili linaonekana anapofurahia kwa kumlaki mwanawe anaporudi kutoka shuleni. Na kwa njia hii, jinsia ya kike inaonekana kupenda elimu na kuiunga mkono. Pia, katika picha kwenye uk 15, inaonekana wazi kuwa mtoto msichana pia amepewa nafasi kusoma katika shule ya Masomoni. Hii ni ishara kuwa wazazi na watoto wamezinduka na kulionea fahari swala la elimu kwa mtoto msichana. Aidha, kutokana na picha kwenye ukurasa wa 19, nafasi ya jinsia ya kike imeangaziwa ambapo kuna mwalimu

wa kike darasani pamoja na wanafunzi wa kike. Ni wazi kuwa mwalimu huyu amepitia elimu ya kutosha ili kuwa na cheo hiki. Hili ni kitia moyo kwa mtoto msichana kuwa naye pia anapaswa kusoma awe kama wanawake wengine wasomi katika jamii yake.

Katika *Kisasi Hapana*, mwanamke amesawiriwa kama mvumilivu kupitia kwa mbinu ya picha. Mama na nyanya ya Kido wanavumilia maisha magumu, ugonjwa wa Kido, wanafiwa na nyanya yao, wananyanganywa mifugo wote na hata binti yao Salama anatekwa na kuwaongezea majonzi. Majonzi haya yanadhihirika kupitia picha mbalimbali zilizo kwenye kurasa za 4, 5, 8, 9, 10, na 17.

Mwanamke pia ni mwenye bidii na anafuzu katika michezo kama inavyodhihirika kwenye picha katika ukurasa wa 24 ambapo katika shule ya akina Kido wana timu ya mpira ya wasichana inayocheza hadi kiwango cha kitaifa. Salama pia ameshiriki riadha hadi kiwango cha mkoa. Na Kido anasema kuwa hawa wasichana ni hodari sana na wanajulikana ndani na nje ya eneo lao. Baadhi yao wanajulikana nchi nzima kwa sababu wanachezea timu yao katika viwango vya wilaya, mkoa na taifa (tazama kielelezo 4.3).

Katika riwaya ya *Sitaki Iwe Siri*, mwanamke anasawiriwa kuwa mlezi na hili linaonekana waziwazi wakati Mwalongo anawatunza wajukuu wake kwa uanana na mapenzi. Mwanzoni mwa hadithi kuna picha ya Mwalongo nyanya ya Musa akienda kuwaamsha ili wajitayarishe waende shuleni. Anawapata wakisali. Hili linamfurahisha sana nyanya kwa kuwaona wajukuu wake kuwa wacha Mungu. Baadaye picha inamwonesha nyanya Mwalongo akiwapoeshea wajukuu wake uji ili wanywe waende shuleni.

Mwanamke anasawiriwa kuwa mlezi mwema. Katika picha kwenye ukurasa wa 5, wajukuu hawa wanaonekana wakiwa nadhifu wakielekea shuleni. Hii ni ishara tosha kuwa wanatunzwa vema na nyanya yao Mwalongo. Picha kwenye ukurasa wa 11 inaonesha nyanya Mwalongo akiwa ameketi na wajukuu wake. Hapa wanaonekana kumdadisi kuhusu

masuala mengi. Baadhi ya masuala haya ni kuhusu kifo cha wazazi wao. Nyanya anajitahidi kuwaeleza kwa utulivu. Kwa njia hii nyanya huyu anatimiza wajibu wake kama mzazi mlezi.

Elimu ya mtoto msichana imeangaziwa kupitia picha. Kwa mfano kwenye ukurasa wa 5, Haki na Ukwa wanaonekana wakienda shuleni. Kwenye ukurasa wa 14, wasichana wanaonekana wakicheza shuleni. Ukurasa wa 18 una watoto wasichana pamoja na wenzao wa kiume kwenye gwaride. Kwenye ukurasa wa 24 pia wasichana pamoja na wavulana wanacheza shuleni wakati wa mapumziko. Picha kwenye ukurasa wa 33 inamwonesha nesi akiwahudumia wageni waliofika hospitalini. Picha hizi zinaendeleza maudhui ya elimu kwa wasichana.

### 4.3.7 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo katika Fasihi ya Watoto

Maudhui ya ugonjwa na kifo yameangaziwa kupitia vipengele vya fani kama tashbihi, picha, misemo na nahau.

#### 4.3.7.1 Tashbihi Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo

Tashbihi imetumiwa kuendeleza maudhui ya ugonjwa pale ambapo tunaelezwa kuhusu hali ya Taabu, mwana wa Lena katika *Nimefufuka* ambaye aliachwa kutunzwa na Sikitu baada ya Lena aliyekuwa mamake kufa. Tunaambiwa:

> "Mkojo nao kila siku ni kama mfereji usiofungika" (Uk. 11).

Tashbihi "Mkojo nao kila siku ni kama mfereji usiofungika" inaonesha namna ugonjwa ulivyomwathiri Taabu kiasi cha kukosa kudhibiti mkojo wake. Ugonjwa huu unamfanya mtoto huyu kulia kila mara na hili linamfanya kudhoofika kiafya zaidi. Pia kuhusu hali ya ya ugonjwa wa Jose mwandishi anasema:

> "Jose ni msalaba mzito kama nanga" (Uk. 13).

Tashbihi “Msalaba mzito kama nanga” inaonesha hisia za Sikitu dada ya Jose kuelekea Jose ambaye amekuwa mlevi kiasi cha kumfanya kuwa mgonjwa na kuwa mzigo kwa wazazi wake na wengine waliokuwa na jukumu la kumtunza. Hawezi kujitunza kwa namna yoyote na hivyo kuwa mzigo unaobebwa tu kwa kujilazimisha kama nanga ilivyo mzigo mzito kwa meli ila hubebwa tu kwa kujilazimisha.

Katika *Sitaki Iwe Siri*, mwandishi anatumia tashbihi kueleza kuhusu hali ya watoto wa Mwalongo, Yusufu na Honorota hasa kabla ya kifo chao. Mwandishi anasema:

> “Kutwa kucha, afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng’onda na macho yao kuwaingia ndani” (Uk. 8).

“Wakakonda kama ng’onda” inamaanisha kuwa walidhoofika kupita kiasi kutokana na ugonjwa wa Ukimwi kabla ya kifo kuwafika. Baada ya kifo chao tashbihi inatumiwa kuonyesha jakamoyo la Mwalongo mama yao:

> “Mwalongo alikuwa ameganda kama kigaga pale nje na kuyakazia macho makaburi ya mwanawe na mkaza mwanawe” (Uk. 9).

Kuganda kama kigaga ni tashbihi ambayo imetumiwa kuonyesha kuwa Mwalongo alikuwa amesimama mbele ya makaburi akiwa katika mawazo mazito yenye majonzi akifikiria wanawe.

### 4.3.7.2 Taswira Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo

Taswira imetumiwa katika riwaya ya *Nimefufuka* kuendeleza maudhui ya ugonjwa na kifo. Mwandishi anatuchorea taswira ya uoni kwa kumwonyesha Lena kuwa amekonda, ana mimba ambayo imemkataa na kuwa mwili wake umedhoofika sana. Hii picha inafaa ugonjwa wa Ukimwi unaoelekea kuwa ndio unamsumbua Lena. Hatimaye, ugonjwa huu mbaya unamwangamiza Lena muda mfupi baada ya kujifungua bintiye Taabu. Kwa maelezo ya kitaswira pia tunaelezwa kuhusu Taabu ambaye anahara na kukojoa kama mfereji kwa sababu anaugua ugonjwa fulani hatari unaoelekea kumwangamiza.

#### 4.3.7.3 Nahau Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo

Katika *Sitaki Iwe Siri,* Lena anakutana na kifo chake na nahau inatumiwa kuonesha hili:

> "Aliaga dunia siku chache baada ya kujifungua mwana wa kiume" (Uk. 8).

Kuaga dunia inamaanisha kufa. Lena alikufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi muda mfupi baada ya kujifungua mtoto wake Taabu. Wazazi walijaribu kumwokoa kwa kumtafutia matibabu ya kila aina lakini haikuwezekana.

#### 4.3.7.4 Methali Inavyoendeleza Maudhui ya Ugonjwa na Kifo

Maudhui ya ugonjwa na kifo pia yanaendelezwa kupitia kwa methali. Kwa mfano, hali ya ugonjwa na kilio cha kitoto kigonjwa cha Lena inaonyeshwa kupitia kwa maneno ya Sikitu anaposema: "Hivi majuzi kitoto kimeshikwa na maradhi mbalimbali. Hakiishi kulia. Si usiku si mchana ni Ng'wee! Ng'wee! Ng'wee!" Kwa sababu hii Sikitu anahisi analazimishwa kukitunza kitoto hiki ingawa si chake. Kinachomlazimisha kutekeleza wajibu huu kinaonyeshwa kupitia kwa methali hii:

> "Nakionea sana huruma kitoto hiki, ila nakosa nguvu na namna ya kukisaidia. Nami niweze kupumzika. Damu kweli ni nzito, lakini, kwa nini nitunze matunda ya maisha ya anasa ya Lena" (Uk. 12).

"Damu kuwa nzito" ni mdokezo wa methali inayomaanisha uhusiano wa kiukoo ambao husukuma mtu kutenda mambo mengi kwa watu wa aila yake. Kwa hivyo, Sikitu anakitunza kitoto hiki kwa sababu ya uhusiano wa damu na kitoto. Kitoto hiki ni cha dadake na kwa sababu hii inambidi akitunze.

### 4.3.8 Namna Fani Inavyofanikisha Maudhui ya Ushawishi katika Fasihi ya Watoto

Maudhui ya ushawishi yameendelezwa kwa kutumia nahau na methali. Maudhui haya yameendelezwa kwa kina katika riwaya ya *Nimefufuka.*

#### 4.3.8.1 Nahau Inavyofanikisha Maudhui ya Ushawishi

Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia nahau kuendeleza maudhui ya ushawishi. Kwa mfano Upendo anamshawishi mpwa wake Sikitu kuwa mavazi yatamfanya ajiheshimu zaidi. Sikitu mwenyewe anasema hivi:

> "Mavazi uliyonipa yamenipunguzia uzee. Shangazi siku hizi nimetupa mtindo wa kuvaa kiholelaholela. Nachukua muda kuvaa mavazi ya mtindo wa kisasa hata nikishinda tu nyumbani. Jambo hili linanisaidia kujenga imani katika nafsi yangu" (Uk. 24).

Nahau "Linanisaidia kujenga imani" imetumiwa kuonyesha kuwa mashauri ya Upendo yalimwingia Sikitu hadi akaamua kubadili namna yake ya kuvaa na hivyo kumfanya kuwa na uhakika zaidi.

#### 4.3.8.2 Methali Inavyofanikisha Maudhui ya Ushawishi

Kupitia kwa barua, Upendo anamfunza Sikitu kuhusu maisha. Anatumia methali kadhaa kumpatia mashauri. Anamwambia:

> "Maisha ni safari ndefu, safari ya kupanda na kushuka, iliyojaa shari na shwari, asali na shubiri" (Uk. 17).

Kupitia kwa methali hii "maisha ni safari ndefu safari ya kupanda na kushuka" Upendo anamshauri Sikitu kuwa sharti ajitie nidhamu na kutarajia mema na mabaya maishani. Akifanya hivi hana budi kufaulu maishani. Na matokeo hayo mazuri yanaonyeshwa kupitia kwa methali inayosema:

> "Baada ya dhiki faraja" (Uk. 18).

Faraja hii Sikitu anaipata baada ya kupata kazi na mchumba. Hili linaboresha afya yake na kumfanya kujiamini zaidi.

Upendo pia anamshauri Sikitu na kumshawishi kuwa asitamani mafanikio ya watu wengine. Anamtaka aelewe kuwa kila mtu anapitia magumu fulani ambayo yeye hawezi kuyaelewa. Anasema:

> "Usione waja wanacheka ukadhani daima dawamu wana raha. Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake. Muhimu ni mja kutambua silaha bora, tena halali za kupambana na hali, la sivyo iwe, laiti ningalijua…" (Uk. 17).

Kwa upande mwingine Upendo anatiwa moyo afanye yote awezayo ili ajikomboe kutoka kwa mtazamo mbaya aliokuwa nao uliomfanya kujidharau. Asisikilize yale wengine wanasema. Anamwambia kuwa "Watasema, watasema, watachoka." Kwa hivyo kupitia kwa mashauri haya ambayo Sikitu alipewa kupitia kwa barua, kunakuwa na matokeo mazuri kwani Sikitu anabadilisha msimamo wake kuhusu mambo mengi. Anakubali jina Chaurembo. Anamtunza vyema zaidi mtoto wa Lena. Anakubali kuingia katika mapenzi tena na kupata mchumba ambaye hatimaye wanaoana. Hii ni ishara nzuri ya ushawishi kutoka kwa marafiki.

### 4.3.9 Namna Fani Inavyoendeleza Maudhui ya Umuhimu wa Jina katika Fasihi ya Watoto

Maudhui ya umuhimu wa jina yameendelezwa kwa mbinu ya taswira ya uoni wa jinsi wahusika wanavyobadilika wanapobadilishiwa majina. Kwanza tunaelewa kuwa mtu hupatiwa jina anapozaliwa na mhusika hujinasibisha na jina lake. Katika utafiti huu imedhihirika kuwa jina linaathiri maisha ya mtu ya baadaye. Katika kuonesha maudhui ya umuhimu wa jina, mwandishi wa *Nimefufuka* ametuchorea mhusika aliyepewa jina Sikitu alipozaliwa. Mhusika huyu anapoolewa anashindwa kupata mtoto na kuamua kurudi kwao. Hili linamfanya kuvunjika moyo na kuhisi kuwa hafai. Shangazi yake anapendekeza abadilishiwe jina na kuitwa Chaurembo. Matokeo ya mabadiliko haya ni kuwa mhusika huyu anajiheshimu zaidi, anavaa vizuri na kujipenda. Hili linachangia afya yake na baadaye anapata kazi na mume. Hii ni hatua kubwa maishani kwani aliposhindwa kuzaa na kufukuzwa na mumewe alitamauka na kukosa tumaini lolote maishani na kuamua kuwa hawezi kuolewa tena.

Mtoto wa Lena aliitwa Taabu. Mtoto huyu alizaliwa na mamake akafa muda mfupi baadaye. Taabu anakuwa na afya mbaya na kujikojolea ovyo kutokana na ugonjwa unaomkabili. Shangazi ya Sikitu anapendekeza naye pia abadilishiwe jina na kuwa Shujaa badala ya

Taabu na baada ya badiliko hili afya yake inaboreka na kuacha mazoea yake ya kukojoa ovyoovyo. Anaonekana kwenye picha akiwa na furaha huku akicheza kumaanisha kuwa kuna badiliko chanya katika maisha yake. Vilevile mji wa akina Chaurembo unaitwa Mjibalaa na hivyo hauna maendeleo. Mji huu umejaa watu waliotamauka maishani, wengine ni walevi wa kupindukia,  wana matatizo ya ndoa na wanalalamika kila uchao. Chaurembo anatamani ubadilishiwe jina uitwe Mjiadilifu. Pengine badiliko hili pia litabadilisha mwelekeo wa watu na kuwaletea maendeleo kwa kiasi fulani.

**4.4 Hitimisho**

Katika sura hii tumechunguza tumetoa maana ya vipengele mbalimbali vya fani katika fasihi ya watoto na kuvidondoa kutoka katika vitabu vinne tulivyokuwa tunahakiki. Vipengele hivyo ni tashbihi, taswira, nahau, misemo, methali na picha. Vipengele hivi tumehakiki kwa misingi ya utokeaji wavyo na maswala yanayomulikwa navyo. Katika hatua ya pili tumeshughulikia maudhui yanayopatikana katika riwaya tulizochunguza na tukapata maudhui kama familia, elimu, bidii, nidhamu, ugonjwa, kifo, ushawishi, nafasi ya jinsia ya kike, na umuhimu wa jina. Maudhui haya tumeyaeleza kwa undani kutokana na yalivyojitokeza katika riwaya husika. Hatimaye utafiti huu umeonesha jinsi vipengele mbalimbali vya fani vimefanikisha ujenzi wa maudhui katika riwaya hizo. Tumeonesha jinsi kila kipengele kilivyotumiwa kisanaa kujenga maudhui mbalimbali katika vitabu hivyo tulivyohakiki.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho la tasnifu. Sehemu ya kwanza inatoa muhtasari wa tasnifu nzima kwa kutaja mambo muhimu yaliyojitokeza katika utafiti kulingana na malengo ya utafiti. Katika sehemu ya pili, tumetoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti nyingine za baadaye kuhusu mada zinazokaribiana na utafiti huu katika nyanja ya fasihi ya watoto.

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuhakiki nafasi ya fani katika kufanikisha maudhui katika fasihi ya watoto. Utafiti huu ulichochewa na ukweli kuwa kuna mwamko mpya kuhusu fasihi ya watoto na vitabu vingi vya watoto vilivyoandikwa havijahakikiwa na vionjo vyake kuwekwa wazi. Pia, kulikuwa na uchechefu wa tafiti ambazo zilitafiti jinsi vipengele vya fani vinavyofanikisha maudhui katika kazi za watoto. Vitabu vilivyotafitiwa ni *Kisasi Hapana* cha Ken Walibora, *Nimefufuka* kilichoandikwa na Rebecca Nandwa, *Sitaki Iwe Siri* kilichoandikwa na Bitugi Matundura, na *Wema wa Mwana* kilichoandikwa na Nuhu Bakari.

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia misingi ya utafiti kwa kuangazia usuli wa mada, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti na nadharia iliyoongoza utafiti huu. Katika sura ya pili, tumehakiki maandishi yanayohusiana na madhumuni ya utafiti kwa kuchunguza jinsi watafiti mbalimbali wameshughulikia vipengele vya fani katika fasihi ya watoto, maudhui katika fasihi ya watoto na hatimaye wale waliotafiti uhusiano uliopo kati ya vipengele vya fani na maudhui.

Katika sura ya tatu, tuliangazia njia na mbinu za utafiti kwa kuangazia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa ya vitabu tulivyotafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data,

uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na maswala ya maadili katika utafiti. Katika sura ya nne, tulichanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Tulijadili vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza katika vitabu vya *Kisasi Hapana*, *Nimefufuka*, *Sitaki Iwe Siri* na *Wema wa Mwana*. Vipengele vya fani tulivyodondoa na kujadili ni tashbihi, taswira, nahau, misemo, methali na picha. Kisha tukajadili maudhui ya nidhamu, elimu, familia, nafasi ya jinsia ya kike, ugonjwa, kifo, ushawishi na bidii. Tulipiga hatua na kuonyesha jinsi vipengele vya fani vilivyofumwa ili kufanikisha maudhui katika vitabu vya fasihi ya watoto.

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kuainisha vipengele mbalimbali vya fani za uandishi katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunzia katika shule za msingi nchini Kenya. Tulitimiza madhumuni haya kwa kutumikisha mhimili wa kwanza wa Umuundo, ambapo lugha ya waandishi ilichukuliwa kama kile kitu kizima kwa mujibu wa Umuundo. Utafiti huu ulichunguza lugha ya wasanii na kutambua matumizi ya vipengele vidogovidogo vya lugha kama vile methali, tashbihi, misemo, nahau, picha na taswira. Vipengele hivi mbalimbali vya fani vilitambuliwa, kunakiliwa na kuhakikiwa kwa misingi ya utokeaji wavyo, mazingira vilimojikita na maswala yanayoendelezwa navyo.

Madhumuni ya pili yalikuwa ni kujadili maudhui yaliyoangaziwa katika vitabu vya fasihi ya watoto vinavyotumiwa kufunza katika shule za msingi nchini Kenya. Ili kutimiza madhumuni haya, tuliongozwa na mhimili unaosema kuwa kitu chochote kizima huwa kimeundwa kwa vipengele fulani vidogovidogo ambavyo hatimaye huunda kitu kizima. Vipengele hivi vilichukuliwa kuwa maudhui ambayo yalitambuliwa na kujadiliwa kwa kina. Hatimaye, lengo la mwisho lilikuwa ni kutathmini jinsi vipengele vya fani vilivyotumiwa katika vitabu hivyo vinavyofanikisha maudhui. Hapa, utafiti ulionesha jinsi vipengele vya fani vilivyotambuliwa vinavyochangia katika kuendeleza maudhui

mbalimbali. Kila kipengele cha fani kilichokuwa kimetambuliwa kilijadiliwa ili kuonesha kilivyofanikisha maudhui husika.

## 5.2 Muhtasari wa Vipengele vya Fani Vilivyotumiwa katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto

Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa vipengele vya fani katika fasihi ya watoto ni sawa na vipengele vya fani vinavyotumiwa katika fasihi ya watu wazima. Hata hivyo, waandishi wa vitabu hivi wamejizatiti kutumia vipengele vya fani ambavyo ni sahili ili viwe rahisi kueleweka kwa watoto hawa walioko katika shule za msingi. Kulikuwa na vipengele vingi vya fani vilivyotumiwa katika vitabu tulivyotafiti. Hata hivyo, katika kazi hii tuliteua vipengele sita tu vya fani kwa sababu ndivyo vilivyojitokeza wazi na hivyo kufaa madhumuni ya utafiti. Vipengele vya fani tulivyoteua ni tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Waandishi wote wanne wametumia methali 49. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia methali nyingi zaidi akiwa na methali 20 akifuatiwa na waandishi wa *Sitaki Iwe Siri* na *Kisasi Hapana* ambao wana methali 12 na 11 mtawalia. Mwandishi wa *Wema wa Mwana* ametumia methali 6 tu.

Waandishi tuliotafiti wametumia picha 52 kwa ujumla. Riwaya za *Sitaki Iwe Siri* na *Nimefufuka* zimetumia picha 14 kila moja huku *Wema wa Mwana* na *Kisasi Hapana* zikiwa na picha 12 kila kimoja. Kiasi hiki kikubwa cha picha katika kila kitabu ni thibitisho tosha kuwa picha ni kipengele muhimu cha fani katika fasihi ya watoto tofauti na ilivyo katika fasihi ya watu wazima ambayo huwa na picha chache au hata moja tu kwenye jalada. Picha zote kwenye kazi hizi zina rangi zenye kuvutia ili kuchochea hamu ya watoto na kunatisha kumbukizi yao. Katika utafiti huu imebainika kuwa kuna mwingiliano mkubwa wa picha na vipengee vingine vya fani katika fasihi ya watoto inayowakilishwa na vitabu viteule tulivyochunguza. Aidha picha kama fani zimetumiwa kusisitiza maelezo na ujumbe wa

mwandishi katika kazi za fasihi na vilevile kujalizana na fani nyingine kwa kuweka ujumbe katika maneno mengine kwa lengo la kusisitiza. Pia, picha huongeza mambo mengine ambayo hayajatokezwa wazi zaidi katika msemo wala maelezo yaliyotumiwa. Hatimaye picha huchochea watoto kusoma vitabu vya fasihi walivyoandikiwa, kuteka nadhari yao, kudokeza maudhui katika hadithi husika kwa uwazi na kumwezesha mtoto kupokea mambo mengi kwa wakati mmoja. Pia, zinaeleweka kwa urahisi na hivyo kuwasaidia watoto kupata maana na maudhui yanayoendelezwa nazo. Rangi na urahisi wa kueleweka kwa mawazo makuu huweza kufanya watoto hawa kukumbuka maudhui yanayoendelezwa katika kazi hizi.

Kazi zote nne zimetumia misemo 30. Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ameongoza kwa idadi ya misemo na ametumia misemo 11, wa *Wema wa Mwana* ametumia misemo 9, wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia misemo 7 hatimaye mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia misemo 3. Katika utafiti huu, imebainika pia kuwa misemo mingi iliyotumiwa na waandishi hawa inahusu hali ya afya na ugonjwa ikifuatiwa na misemo inayohusu bidii kazini. Utafiti huu uliainisha taswira 36 zilizojitokeza wazi. Riwaya ya *Kisasi Hapana* imetumia taswira 11, *Sitaki Iwe Siri* ina 10 na katika *Nimefufuka* zilikuwa taswira 9. Hatimaye katika *Wema wa Mwana* tulipata taswira 6. Ingawa kuna uwezekano wa kutambua taswira nyingi zaidi, hizi ni zile taswira zilizojitokeza kwa wazi zaidi.

Kwa ujumla, tashbihi tulizozitambua katika vitabu hivi ni 83. Riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* inaongoza kwa idadi ikiwa na tashbihi 42, *Kisasi Hapana* inafuata kwa tashbihi 24, *Nimefufuka* 9, na kisha *Wema wa Mwana* ikiwa na tashbihi 8. Hii ndiyo fani iliyotumiwa kwa wingi zaidi katika kazi tulizochunguza. Kwa hiyo, mwandishi wa *Sitaki Iwe Siri* ametumia tashbihi kwa wingi kuliko waandishi hawa wengine kwani ametumia zaidi ya nusu ya tashbihi hizi zote, akifuatiwa na *Kisasi Hapana* kwa tashbihi 24.

Kutokana na data tuliyopata, imebainika kuwa *Kisasi Hapana* ni riwaya ambayo imetumia nahau kwa wingi sana ikiwa na jumla ya nahau 20 ikifuatiwa na *Sitaki Iwe Siri* ambayo ina nahau 16. *Nimefufuka* na *Wema wa Mwana* ni riwaya zilizotumia nahau chache zikiwa na 6 na 3 mtawalia. Kwa ujumla basi, waandishi hawa wametumia nahau 45 katika kazi zao. Hii si idadi ndogo na hivyo ni ithibati tosha kuwa hiki ni kipengele muhimu kilichotumiwa kuendeleza kazi hizi.

Vipengele hivi vya fani vimefumwa kwa njia rahisi isiyo na utata na hili linafanya iwe rahisi kuvisoma, kuvielewa, kukumbuka mawazo makuu na kupata mafunzo kutokana na vitabu hivyo.

### 5.3 Muhtasari wa Maudhui Yanayopatikana katika Vitabu vya Fasihi ya Watoto

Vitabu ambavyo tulichunguza katika utafiti huu viliangazia maudhui ambayo yanaafiki masilahi ya watoto. Kwa ujumla, tulitambua maudhui tisa ambayo ni familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, ushawishi, ugonjwa na kifo, bidii, umuhimu wa jina, na nafasi ya jinsia ya kike. Maudhui haya kwa ujumla yamelenga mambo ambayo mtoto anaweza kukumbana nayo katika maisha ya kila siku na hivyo kumwathiri kwa njia moja au nyingine. Haya ndiyo maudhui tuliyoona kuwa yanaandamana na madhumuni yetu ya utafiti na yanahusu maslahi ya watoto.

Kutokana na utafiti huu, ilibainika kuwa waandishi wote wanne wameangazia maudhui ya familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, na nafasi ya jinsia ya kike. Hata hivyo, maudhui ya ugonjwa na kifo yameendelezwa na waandishi wa *Nimefufuka*, *Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri*. Maudhui ya umuhimu wa jina yameendelezwa na mwandishi wa *Nimefufuka* pekee. Hatimaye maudhui ya ushawishi yamemulikwa na waandishi wa *Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri*.

**5.4 Muhtasari wa Jinsi Vipengele vya Fani Vinavyotumiwa Kuendeleza Maudhui katika Fasihi ya Watoto**

Vipengele mbalimbali vya fani vimetumiwa na waandishi wa vitabu vilivyoteuliwa ili kunogesha maudhui kwa njia nzuri. Hata ingawa vipengele vya fani ni vingi, vile vilivyojitokeza kwa uwazi katika riwaya tulizotafiti ni tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Kwa ujumla, maudhui tuliyotambua ni tisa ambayo ni familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, ushawishi, ugonjwa na kifo, bidii, umuhimu wa jina, na nafasi ya jinsia ya kike.

Maudhui ya ushawishi yameendelezwa kwa kutumia vipengele vya fani kama nahau na methali. Maudhui ya umuhimu wa jina yameendelezwa na mwandishi wa *Nimefufuka* pekee na yameendelezwa kwa taswira ya uoni wa jinsi wahusika wanavyobadilika wanapobadilishiwa majina. Maudhui ya ugonjwa na kifo yameangaziwa katika riwaya za *Nimefufuka* na *Sitaki Iwe Siri* pekee kupitia tashbihi, methali, picha, misemo, nahau na taswira ya uoni. Tulipata kuwa watu wahusika wanakufa kutokana na ugonjwa unaoelekea kuwa wa Ukimwi. Maudhui ya nafasi ya jinsia ya kike yameendelezwa na waandishi wote tuliokuwa tunachunguza kwa fani kama vile misemo, nahau, tashbihi, picha na taswira. Mwanamke amechorwa kuwa amekumbatia elimu, amezinduka, ni mwenye bidii, ni mwenye mapenzi ni mshauri mwema na mlezi.

Katika utafiti huu, tulibaini kuwa maudhui ya familia yameendelezwa na vipengele vya fani kama tashbihi, picha, methali, taswira, nahau na misemo. Tashbihi zimetumiwa na waandishi wote wanne katika kuendeleza maudhui ya familia. Katika riwaya ya *Kisasi Hapana* tashbihi tano zimetumiwa kuendeleza maudhui ya familia. Katika *Sitaki Iwe Siri* kuna tashbihi kama “Aliwatunza wajukuu wake kama mboni ya macho” ambayo

imetumiwa kuendeleza maudhui haya. Ilibainika wazi kuwa kuna familia kiini, familia pana, familia ya mzazi mmoja na familia ya ulezi.

Pia, ilidhihirika kuwa picha 11 zimetumiwa na mwandishi wa *Wema wa Mwana* kuendeleza maudhui ya familia. Mwandishi wa *Kisasi Hapana* ametumia nahau kama "Uwafanye adabu waliotukosea, nyanya ametuondokea…. amekwenda jongomeo… ametuacha mkono na endelea kuvuta subira na kuniombea." Hatimaye katika *Sitaki Iwe Siri* mwandishi ametumia misemo mitatu "Nyanya Mwalongo alipiga miundi kwa hatua haba huku akionekana mwenye mawazo mengi, nyanya Mwalongo amewatunza mayatima hawa miaka nenda mika rudi hadi nguvu zimemwisha kwa sababu ya umri wake mkubwa, vifo hivyo vimeutia kovu moyo wake na Yusufu na mke wake waliugua kwa muda mrefu sana na hatimaye kusalimu amri."

Katika kuendeleza maudhui ya elimu, waandishi wametumia misemo, tashbihi, taswira, picha, methali, misemo na nahau. Mwandishi wa riwaya ya *Kisasi Hapana*, Ken Walibora, ameangazia elimu kuwili. Ameangazia elimu rasmi inayohusisha kusoma vitabu na kutagusana na walimu. Huku ya pili isiyo rasmi ikihusu michezo ya baada ya masomo kama riadha na kandanda. Ili kufanikisha haya katika kazi yake ametumia mbinu za tashbihi, misemo, nahau, methali na picha. Riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* imetumia mbinu kama tashbihi, taswira na methali. Huku riwaya ya *Wema wa Mwana* ikitumia taswira pekee. Katika kuendeleza maudhui ya nidhamu, waandishi hawa wametumia tashbihi, methali, misemo, nahau, taswira na picha kwa njia tofautitofauti. Maudhui ya bidii katika riwaya ya *Kisasi Hapana* yamefanikishwa kwa kutumia tashbihi, nahau na picha. Kuna tashbihi kama "nafikiri hata nikila nikashiba naweza kuzivunja kama kijiti kidogo au sio", "Penda kusoma kama vile unavyopenda michezo" na "Nitarudi hivi karibuni. Endelea kuvuta subira na

kuniombea.” Riwaya ya *Sitaki Iwe Siri* imetumia tashbihi, nahau na misemo. Imedhihirika wazi kuwa wahusika wameonesha bidii nyumbani, kazini na shuleni.

Katika kuendeleza maudhui ya ushirikiano, mwandishi wa *Wema wa Mwana* anatumia nahau kutuonesha hali kuwa Baba Juma na Baba Ngoyoni wanashirikiana wanapompeleka Ngoyoni katika shule ya Masomoni. Kwa ujumla basi, riwaya ya *Wema wa Mwana* imetumia nahau na picha kufanikisha maudhui ya ushirikiano. Katika riwaya ya *Kisasi Hapana*, picha na misemo imetumiwa kuendeleza maudhui ya ushirikiano pale ambapo Kido anabebwa kwa baiskeli na jirani yao Bwana Lukoko na kumpeleka kwake baada ya kutoka hospitalini. Mke wa Lukoko naye anampokea kwa ukarimu na kumtunza vema bila kujali kutapika kwake. Mwandishi wa *Nimefufuka* ametumia nahau, methali na tashbihi katika kuendeleza maudhui ya ushirikiano ambapo watu wa ukoo wanachanga pesa kuleta mwili wa Lena nyumbani ili uzikwe. Wanajamii pia wanashirikiana kuzungumza na wazazi wa Lena wakiwashauri ili waboreshe maisha yao. Hatimaye, *Kisasi Hapana* imetumia misemo na picha kufanikisha maudhui ya ushirikiano kwa kuonesha kuwa Kido anapokuwa mgonjwa nyanya yake na mama yake wanashirikiana kumpeleka hospitalini.

### 5.5 Hitimisho la Utafiti

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika wazi kuwa waandishi wote wanne walifanikiwa kujadili maudhui yanayoweza kuafiki watoto. Walijadili maudhui kama familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo, na ushawishi. Hata hivyo, mwandishi wa *Wema wa Mwana* hakugusia maudhui ya ugonjwa na kifo hata kidogo huku mwandishi wa *Nimefufuka* akifaulu kwa kiasi kikubwa kuonyesha umuhimu wa jina kwa kuonyesha jinsi wahusika wanavyoathiriwa wanapobadilishiwa majina. Maudhui haya yanagusia maswala yanayohusu watoto kwa sababu mambo ya bidii, elimu, nidhamu, ugonjwa na kifo ni mahangaiko yao makuu.

Kuhusu vipengele vya fani walivyotumia ili kuendeleza maudhui yao, waandishi hawa wamefaulu kwa viwango tofautitofauti. Wasanii hawa wote wametumia vipengele vya fani kama vile tashbihi, taswira, misemo, methali, picha na nahau. Hata hivyo, mwandishi wa *Kisasi Hapana* amefaulu kwa kutumia nahau, methali na misemo kwa wingi kuliko waandishi hawa wengine watatu. Mwandishi wa *Nimefufuka* kwa upande mwingine amefaulu sana katika mbinu ya methali. Mwandishi wa *Sitaki iwe Siri* amefaulu sana kwa kutumia tashbihi kwa wingi. Kwa ujumla basi, waandishi hawa wamefaulu katika kusuka maudhui yao kwa kutumia vipengele mbalimbali vya fani. Maudhui na vipengele hivyo vya fani walivyotumia vinaweza kuwafaa watoto na kwa sababu hii, waandishi wa riwaya za watoto tulizochunguza wamefaulu kufikisha ujumbe kwa njia mwafaka kwa hadhira lengwa.

**5.6 Mapendekezo ya Utafiti**

Katika utafiti huu, tumejadili vipengele mbalimbali vya fani ambavyo vimetumiwa katika vitabu vya watoto vya *Wema wa Mwana*, *Nimefufuka*, *Kisasi Hapana* na *Sitaki Iwe Siri*. Vipengele vya fani tulivyoteua na kutafiti ni tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Pia, tumejadili maudhui mbalimbali ambayo waandishi wa vitabu hivi wameangazia ambayo ni familia, elimu, nidhamu, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, ugonjwa na kifo, na ushawishi. Hatimaye, tumejadili namna waandishi hawa wanavyotumia vipengele hivyo mbalimbali vya fani kisanii ili kuendeleza maudhui kwa mafanikio katika kazi zao. Hata hivyo, tulipokuwa tunatafiti kazi hizi, tulitambua kuwa kuna vipengele vingi sana vya fani ambavyo wasanii hawa wametumia katika kazi tafitiwa. Hatungeweza kutafiti vipengele hivyo vyote kwa sababu ni vingi mno. Tulitafiti vipengele vya fani kama tashbihi, taswira, misemo, nahau, methali na picha. Hatukuchunguza viwango vingine vya lugha kama sarufi, urefu wa sentensi, rangi ya michoro na kiasi cha

maandishi. Tunapendekeza tafiti nyingine za wakati ujao ziangazie vipengele hivi vya fani katika fasihi ya watoto.

Fani katika fasihi ya watoto ni eneo pana. Hata hivyo, katika utafiti wetu tulichunguza tu matumizi ya lugha na picha. Kwa hiyo, tafiti nyingine zinaweza kuchunguza usawiri wa wahusika, mandhari na usimulizi katika fasihi ya watoto. Hatimaye, tafiti nyingine za kiwingidadi zinaweza kufanywa ili kutambua ni mbinu zipi zinazotumiwa kwa wingi sana na waandishi hawa wa fasihi ya watoto.

Kwa mujibu wa utafiti huu, tuliangazia maudhui kama familia, elimu, ushawishi, ushirikiano, bidii, nafasi ya jinsia ya kike, umuhimu wa jina, na ugonjwa na kifo. Hata hivyo utafiti zaidi unaweza kuibua maudhui mengine. Pia katika tafiti zijazo, watoto wanaweza kushirikishwa ili tuone ikiwa wao wenyewe pia wanaweza kutambua mbinu na maudhui tofauti kwa kutegemea mwonoulimwengu wao.

## MAREJELEO


ALSTBOIMPS (2015). Appoved List of School Text Books and Other Instructional Materials for Primary Schools.

Alembi, E. (2007*). Phases and dynamics in childrens literature in Kenya. In a decade of publishing excellence.* In the 10th Nairobi International Book Fair Booklet. Nairobi: Kenya Publishers Association.

Alembi, E. (2007). *The role of childrens oral literature in socialozation: An analysis of abanyole childrens oral poetry*. Research paper at the International Society for Folk Narrative at Research Conference held at National University of La Pampa in Santa Rosa, Argentina.

Alembi, E. (1991). *An nalysis of style and social significance of Abanyole childrens oral poetry*. M. A Thesis, Kenyatta University (Unpublished).

Anderson, N. A. (2013). *Elementary children's literature.* Pearson: St Petersburg.

Andrea, A. (2011). *Social issues in contemporary African American young adult ficton:* Retrieved from http://is.muni.cz/th/183848/pedf_m/social.

Aries, P. (1962). *Centuries of Childhood*. New York: Vintage Books.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa fasihi ya watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Bakize, L. H. (2018). Riwaya ya Kihistoria ya Watoto: Dafina iliyopuuzwa katika fasihi ya Kiswahili, katika Kandagor, M. & Mukuthuria, M. (wah.) 2018. *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Mandeleo Yake,* 64-75. Dar es Salaam: CHAKAMA/TUKI.

Bakize, L. (2013). Changamoto zinazokabili fasihi ya watoto Tanzania katika Kiswahili. Jarida la Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili vol. 76 uku. 61-70.

Breitsprecher, W. P. (2005). *Education and Library Media* iliyopakuliwa kutoka http://www.breitlinks.com/my_libmedia/children's_genres.htm. Ilipakuliwa 27/01/218.

Bryman, A. (2004). *Social research methods* (2nd edition). Oxford: Oxford University Press.

Cass, J. E. (1967). *Literature and the young child*. London: Longman Group Ltd.

Chakava, H. (1998). *Children and books in Kenya. In Indaba 98 books for children*. Harare. The Zimbabwe International Book Fair Trust. pp. 42-46.

Charo, K. (1976). *Toka Kizazi hadi Kizazi*. Dar es Saalaam: Ndanda EnterprisesTanzania Ltd.

Davies, A. (1973). *Literature for Children.* Portsmouth: Open University Press.

Fokkema, D. & Ibsch, E. (1995). *Theories of literature in the twentieth century. Structuralism, marxism, aesthetics of reception, semiotics*. London: Hurst & Company.

Gachukia, A. & Akivaga, K. (1978). *Teaching of African Literature in Schools.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Gall, D. M., Borg, R. W., & Gall, P. G. (1996). *Education research: An introduction* (6th ed.) New York: Longman Publishers.

Gatere, L. N. (2020). *Usawiri wa familia ya kisasa katika fasihi ya watoto nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Gituku, N. (1990). *Maigizo ya kienyeji ya watoto nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Haji, A. I. (1983). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Haviland, V. (1973). *Children and literature*. London: The Bodley Head Ltd.

Heale, J. (1992). *Bookchat newsletter 1992*: No. 108.

Huck, C. (2001). *Children's literature in the elementary school. (*7*th* ed.). New York: McGraw- Hill Company.

Huck, C. S. (1967). *Children's literature in elementary schools.* (3rd Ed.). New York: Holt Rhinehart.

Hunt, P. (2006). *Children's literature*. New York: Routledge.

Hunt, P. (1994). *An Introduction to Childrens Literature.* Oxford: Oxford University Press.

ILO (2017), *Global Estimates of Child Labour: Results and Trends, 2012-2016*. Geneva(…..)

Karuga, M. N. (2005). *Uhakiki na Upokezi wa Fasihi ya Kiswahili ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Kenya Gazette Supplement (2017). *The Basic Education Amendment Bill, 2017: An Act of Parliament to amend the Basic Education Act and for Connected Purposes.* Kenya Gazette Supliment No. 85 (National Assembly Bills No. 27).

Kelly, K. & Costello, S. (2014). Creating digital comics in response to literature: aesthetics, and aesthetic transactions and meaning. Language arts issue92 vol. 2 pp 103-117.

Kenya Basic Education Act (2012). *The Basic Education Amendment Bill, 2012: An Act of Parliament to amend the Basic Education Act and for Connected Purposes.* Kenya Gazette Supliment No. 111 (National Assembly Bills No. 51).

Khorana, M. (1994). *African literature for children and young adults: An annotated bibliography of English language books 1873-1994.* London: Greenwood Press.

King'ei, K. (2000). *Miale ya uzalendo*. Nairob: Phoenix Publishers.

Koerner, E. F. K. (1971). *Ferdinand de Saussure origin and development of his lingustic theory in western studies of language. A critical evaluation of the evolution of Saussurean principles and their relevance to contemporary linguistic theories*. Berlin: Simon Fraser University.

Kothari, R. C. (2013). *Research methodology: Methods and techniques* (2nd Ed.). New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Lacan, J. (1970). Of structure as an immixing of an otherness prerequisite to any subject whatever. In R. Macksey & E. Donato (eds.). *The languages of criticism and sciences of man: The structuralist controversy*. Baltomore: John Hopkins Press. Pg 186-200.

Leech, N. G. (1969). *Style in fiction: Alinguistic introduction to English fictional prose.* London: Longman.

LibApp. (2018). url:https://libguides.slu.edu/childrens_literature (18/10/2018b12: 55pm).

Lyimo, E. B., Bakize, L. H. & Ngugi, P. M. Y. (2017). Maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Kenya na Tanzania: Mkabala linganishi. African Journals Online. Vol. 80, No. 1.

Marshall, C. & Rossman, G. B. (2006). *Designing qualitative research.*( 4th Ed.). Thousand Oaks CA: Sage Publications.

Matteru, M. D. (1983). *Fasihi simulizi na uandishi wa Kiswahili katika fasihi*: Makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.

Matundura, E. B. (2007). *Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Isiyochapishwa).

Matundura, E., Kobia, J. & Mukuthuria, M. (2013). "Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto" katika Mulika Na. 32 Dar es Salaam: TATAKI.

Mbuthia, M. & Miricho, M. (2017). *The impact of the depiction of children in selected Swahili children stories.* The International Journal of Contemporary Applied Sciences, Vol. 4, No. 1, pp. 2308-1365.

Mbure, S. (1997). *African Childrens Literature or Literature of African Child* in Roul Rangvist and Jurge Martini (eds). Preserving the Landscape of Imagination. Children Literature in Africa. Amsterdam: Matatu. Journal for African culture and Society. No. 17-18. 3-9.

Mdee, S. J., Njogu, K. & Shafi, A. (2019). *Kamusi ya karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mpesha, N. (1996). *Children's literature in Tanzania: Aliterary appreciation of its growth and development*. Phd Thesis, Kenyatta University (Unpublished).

Miricho, M., Sheila, P., Wandera, S. & Nabea, W. (2019). Fasihi ya watoto ya Kiswahili na mshikamano wa kitaifa. Katika Ogechi, N. & Kandagor, M. *Mwanga wa Lugha*. Eldoret: Moi University Press.

Miricho, E. M. (2015). *Usawiri wa Watoto katika Hadithi za Mwepesi wa Kusahau na Likizo ya Mkosi.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (1999). *Research methods: Quantitative and qualitative approaches.* Nairobi: Acts Press.

Muhando, P. & Balisidya, N. (1996). *Fasihi na sanaa za maonyesho*. Dar es Salaam: T.P.H.

Mukami, W. K. (2005). *Uhalisi na mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Mukuthuria, M. (2009). *Maadili ya Utafiti*. Katika D. P. B. Masamba (Mh.) Kiswahili Juzuu la 73: Uk. 110-121. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: TATAKI.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za fasihi simulizi*: Katika *Mulika 21*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. OSW 105: Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Musau, P. & Ngugi, P. M. Y. (1997). *Kiswahili research in Kenyan universitie:Where are we Now?* In R. M. Beck, T. Geider, W. Graebner & I. Heine (eds.). *Swahili Forum VI* No. 51, University of Koln, Germany. 219-229.

Mutua, J. M. (2014). *Fani za fasihi zinazoibua fantasia katika hadithi za watoto za Nyambura Mpesha*. Katika *Nordic Journal of African Studies* 23(4):292-306 (2014).

Namanya, E. (2016). *Dhima ya misemo na nahau katika jamii ya Wakiga wilayani Kabale Kusini, Magharibi mwa Uganda*. Mombasa: Pwani University Press.

Nandwa, J. A. (1994). *Teaching oral literature in the 8.4.4 system: A new integrated approach.* In Meshati Masinjila & Okoth Okombo eds.). Teaching Oral Litertature. Nairobi: Kenya Oral Literature Association (Kola).

Ndalu, E. A., Babusa, H. & Mirikau, S. A. (2019). *Kamusi teule ya Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers LTD.

Ngugi, E. (2018). *Maudhui na mtindo katika ushairi wa watoto: Uchanganuzi wa utenzi wa haki za watoto na mashairi bulbul*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta (Isiyochapishwa).

Ngugi, P. M. (1997). *Childrens literature research in Kenyan universities: Where are we*? International Journal of Arts and Commerce. Vol. 1 No. 2.

Ngugi, P. M. (2011). Ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule za msingi nchini Kenya katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 9 kur 84-94.

Ngugi, T. (1981). *Writers in Politics: Essays*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Njagi, G. M. (2002). *Introduction to the study of literature*. Nairobi: Kenyatta University Press.

Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*: *Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, N. (1978). *African Oral Literature: Fighting Literature*. In Addah Gachukia and Akivaga, K. (eds). Teaching of African Literature in Schools. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nkwera, F. V. M. (1978). *Sarufi na fasihi: Uandishi wa vitabu vya sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Island: IL 61201

Norton, D. & Norton, S. (2010). *Through the eyes of a child: An introduction to Childrens Literature (8th ed.)*. Boston, MA: Prentice-Hall.

Odaga, A. B. (1985). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Ogechi, N. & Ogechi, E. (2002). Educational publishing in African languages, with a focus on Swahili in Kenya. In Nordic of African Studies, 11 (2):167-184

Oiko, F. G. (2017). *Uhakiki wa mtindo katika tamthilia za Arege*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara (Isiyochapishwa).

Okhoba, E. W. (1995). *"Style and Meaning of Abamarachi Childrens Oral Poetry*." M. A. Thesis, Kenyatta University. (Unpublished).

Osazee, F. P. (1991). *Childrens Literature Research in Africa: Problems and Prospects*. In Saur K. G (ed). Childrens literature Research. Munchen: International Resources Exchange.

Pearson, L. (2012). *Childrens and young adult literature database*—Access Card, 1/E.

Saluhaya, M. C. (2013). *Kamusi elezo huru*. Wikipedia.

Scholes, R. (1974). *Structuralism in literature: An introduction.* New York: Yale University Press.

Sengo, T. S. Y. (1987). *Fasihi simulizi: Sekondari na vyuo*. Dar es Salaam: Nyanza Publications Agency.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU LTD.

Senkoro, F. E. M. K. (1984). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Strauss, L. C. (1963). *Structural anthropology*. Claire Jacobson and Brook G. Schoepf: Basic Books, Inc.

Syambo, K. & Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Traore, F. A. (2010). *Childrens literature in African languages: Swahili books for children in Kenya and Tanzania*. Katika The Nordic African Journal.

Truex, D. (1996). *Text based analysis: A brief introduction*. Accessed on 25 August 2015.

Tucker, N. (1981). *The Child and the Book Apsychological and Literary Explanation.* Cambridge: Cambridge University College.

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. (Toleo la pili). Dar es Salaam: TUKI.

UNICEF (2009). *UNICEF Annual Report for Kenya 2009.*

Verma, R. G. (2019). Women writers for children in India: A Kaleidospic view. Feminist Discourses in Indian Context: Assertion, Identity and Agency. In Vandana, S. New Delhi: Authorpress.

Vuuren, K. (1994). *A study of indegenius childrens literature in South Africa*. Masters Thesis. University of Cape Town.

Wafula, R. M. & Njogu K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, M. N. (2011). *"Tradition versus Modernity: Generational Conflict in Vuta Nkuvute, Kufa Kuzikana, Msimu wa Vipepeo and Tumaini.* http://www.ifeas.uni-mainz.de/swaFo/volume18html,27/8/2018.

Wamalwa, S. (2015). *Sifa na umuhimu wa fasihi ya watoto*. Swahilihub. Swamalwa@ke.nationmedia.com

Wambua, M. S. (2001). *Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo*. Tasnifu ya Uzamili (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta .

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya fasihi 1: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Wide-Muwa.

Wamitila, K. W. (2003*). Kamusi ya fasihi. Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi*. (Toleo la Pili). Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Weche, M. O. (2000). *Childrens literature as an image forming force: A case study of Ezekiel Alembis books*. M. A Thesis, Kenyatta University.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho A: Barua ya Utambulisho kwa NACOSTI Kutoka Chuo Kikuu cha Rongo

RONGO UNIVERSITY

OFFICE OF THE DEAN

SCHOOL OF GRADUATE STUDIES

Tel. 0771349741

P.O. Box 103 - 40404
**RONGO**

Our Ref: **AS/MKIS/1002/13**

**Date:** Thursday, October 11, 2018

The Chief Executive Officer,
National Commission for Science, Technology & Innovation,
off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P.O Box 30623-00100,
**Nairobi-KENYA**.

Dear Sir,

**RE: RESEARCH PERMIT FOR MR. MATIN IBRAHIM-AS/MKIS/1002/13**

We wish to inform you that the above person is a bona fide graduate student of Rongo University in the School of Arts and Social Sciences pursuing a Master degree in Kiswahili. He has been authorized by the University to undertake research titled; ***"Nafasi Ya Fani Katika Kufanisha Maudhui Katika Fasihi Ya Watoto".***

This is, therefore, to request the commission to issue him with a research permit to enable him proceed for field work.

Your assistance to him shall be highly appreciated.

Thank you.

Dr. Edward Anino
**Ag. DEAN, SCHOOL OF GRADUATE STUDIES**

RONGO UNIVERSITY
THE DEAN
12 OCT 2018
SCHOOL OF GRADUATE STUDIES
P. O. BOX 103 - 40404, RONGO

Copy to: Vice Chancellor
Deputy Vice Chancellor (Academic and Student Affairs).
Dean, School of Arts and Social Sciences
HoD, Languages, Literature and Linguistics

## Kiambatisho B: Leseni ya Utafiti Kutoka NACOSTI (Ukurasa wa Mbele)

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MR. IBRAHIM MATIN***
**of RONGO UNIVERSITY, 99-40400 Suna Migori, has been permitted to conduct research in *Migori County***

**on the topic: *NAFASI YA FANI KATIKA KUFANIKISHA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA WATOTO***

**for the period ending:**
***26th February,2020***


**Permit No : NACOSTI/P/19/70232/27352**
**Date Of Issue : 26th February,2019**
**Fee Recieved :Ksh 1000**




.............................
***Applicant's Signature***

.............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***

**Kiambatisho C: Leseni ya Utafiti Kutoka NACOSTI (Ukurasa wa Nyuma)**



THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013

The Grant of Research Licenses is guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014.

CONDITIONS

1. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
2. The License and any rights thereunder are non-transferable.
3. The Licensee shall inform the County Governor before commencement of the research.
4. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
5. The License does not give authority to transfer research materials.
6. NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project.
7. The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report within one year of completion of the research.
8. NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.

National Commission for Science, Technology and innovation
P.O. Box 30623 - 00100, Nairobi, Kenya
TEL: 020 400 7000, 0713 788787, 0735 404245
Email: dg@nacosti.go.ke, registry@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI

National Commission for Science, Technology and Innovation

RESEARCH LICENSE

Serial No.A 23294

CONDITIONS: see back page

## Kiambatisho D: Idhini ya Utafiti Kutoka NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone:+254-20-2213471,
2241349,3310571,2219420
Fax:+254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website : www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref: No. **NACOSTI/P/19/70232/27352**

Date: **26th February, 2019**

Ibrahim Matin
Rongo University
P.O. Box 103-40404
**RONGO**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Nafasi ya fani katika kufanikisha maudhui katika fasihi ya watoto"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Migori County** for the period ending **26th February, 2020.**

You are advised to report to **the County Commissioner and the County Director of Education, Migori County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System.

**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:

The County Commissioner
Migori County.

The County Director of Education
Migori County.

*National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001:2008 Certified*